Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 11 Februari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Sammuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya Zabuni ya Kuzalisha umeme wa Dharura ulioipa ushindi Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* ya *Houston, Texas* – Marekani mwaka 2006.

Taarifa ya Serikali kuhusu tatizo la Nishati ya Mafuta Nchini.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Serikali kuhusu uendeshaji wa Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL).*

Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania *(TRL)* unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India.

Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya utendaji wa kazi usioridhisha wa kampuni ya Tanzania *International Container Terminal Services (TICTS).*

Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya uuzwaji wa Nyumba za Serikali.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI - (MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura ulioipa ushindi Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* ya *Houston, Texas* – Marekani mwaka 2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU – (MHE. MOHAMED H. MISSANGA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania *(TRL)* unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India.

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya utendaji wa kazi usioridhisha wa kampuni ya Tanzania *International Container Terminal Services (TICTS).*

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu ya uuzwaji wa Nyumba za Serikali.

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kuhusu hali ya uendeshaji na hatima ya Shirika la Ndege la Tanzania. *(Makofi)*

Na. 149

**Kugawa Jimbo la Mikumi**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Mikumi ni kubwa mno na lina idadi kubwa ya watu wanaoishi katika kata kumi na mbili na vijiji vinavyotenganishwa kwa umbali mkubwa mno kama kilomita 220, kwa mfano vijiji vya Mabwerebwere, Malolo na Uling'ombe; na kwa kuwa hali hiyo husababisha wananchi wa Jimbo la Mikumi wasihudumiwe ipasavyo:-

(a) Je, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi ipo tayari kuligawa Jimbo hilo kuwa Majimbo mawili ili kuwa na uwiano mzuri wa uwakilishi na utoaji wa huduma?

(b) Kwa kuwa Jimbo la Mikumi ni kubwa kuliko Majimbo ya Kilosa na Gairo yakiunganishwa pamoja, Je, Serikali haioni kuwa ni vizuri kupanga upoya baadhi ya kata zilizo katika Majimbo hayo kama vile Mabwerebwere , Masanze, Kilingali , Zombo na Ulaya ili kuibua ufanisi wa uwakilishi ulio karibu na wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Ibara ya 74(6)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekasimiwa mamlaka ya kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika majimbo kwa madhumuni ya kurahisisha shughuli za uchaguzi wa Wabunge.

Aidha, Ibara ya 75(1) na ile ya (4) ya Katiba imeipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi mamlaka ya kuchunguza mara kwa mara mipaka ya majimbo angalau kila baada ya miaka kumi kwa namna itakavyoamuliwa na Tume hiyo.

Mheshimiwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilifanya zoezi la kuchunguza mipaka na kugawa majimbo ya uchaguzi wa Wabunge kwa mara ya mwisho mwaka 1995. Zoezi hilo linatarajiwa kufanyika tena mwaka huu wa 2009 kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2010. Vigezo vinavyotumika kugawa majimbo ni pamoja na:- Idadi ya watu, upatikanaji wa mawasiliano, hali ya kiuchumi kwa kila jimbo pamoja na ukubwa wa jimbo lenyewe.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaainisha bayana vigezo vyote muhimu vitakavyozingatiwa katika ugawaji wa majimbo ya uchaguzi pamoja na kuwatangazia wananchi na wadau mbali mbali ili wapate nafasi ya kutoa maoni yao wakati huo.

Hivyo, Tume ya Uchaguzi itakuwa tayari kupokea maoni yatakayotolewa na wananchi na kwa yale maeneo ambayo yatakidhi vigezo viloivyowekwa, yatapewa kipaumbele katika maamuzi ya kurekebishwa mipaka yake. Napenda kuwahakikishia Wabunge wote, hasa Mbunge wa Mikumi kwamba wadau wa jimbo la Mikumi nao watapata fursa ya kutoa maoni yao ili yaweze kutathminiwa na Tume na iwapo itaonekana kuwa yanakidhi vigezo husika, basi Jimbo hilo litaweza kugawanywa kwa kuzingatia sheria za nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, maoni na ushauri wa kuangaliwa upya mipaka ya kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge utazingatiwa kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kusogeza huduma mbali mbali za kijamii karibu na wananchi ili waweze kujiletea maendeleo na maisha bora kwa urahisi.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake fasaha na mazuri. Pamoja na majibu hayo, nina swali moja dogo la nyongeza. Je, Serikali nayo itakuwa tayari sasa kuchukua fursa ya Tume ya Uchaguzi kuangalia ukubwa wa Majimbo, kupanga utaratibu wa kisayansi zaidi

wa kutoa posho ya usafiri kwa Wabunge Jimboni ili yawiane na ukubwa au udogo wa Majimbo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali hili halihusiani kabisa na swali la msingi. Mheshimiwa Khalifa kwa swali la nyongeza!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Tume mara ya mwisho iliangalia majimbo ya uchaguzi mwaka 1995; hivi anayo habari kuwa kwa upande wa Zanzibar majimbo hayo baada ya 1995 yaliangaliwa tena nay eye amesema hapa kuwa yataangaliwa tena katika mwisho wa kipindi hiki mwaka 2010,

Je, kwa kitendo hicho haitakuwa Tume imeishayaangalia majimbo ya Zanzibar zaidi ya mara mbili katika kipindi hiki cha miaka kumi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nipende kusema hapa kwamba vigezo vinavyoangaliwa kugawa majimbo ya uchaguzi kwa upande wa Tanzania Bara ni tofauti kabisa na vigezo vinavyotumika kugawa majimbo ya uchaguzi kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Ikumbukwe kwamba Uchaguzi Mkuu kwa upande wa Tanzania Zanzibar unahusisha pia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa ajili ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa zoezi lililofanyika ambalo Mbunge analitaja, linafanyika kwa upande wa uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi limeelezea jimbo la Mikumi, na tatizo la jimbo la Mikumi linakaribia kufanana na tatizo la Wilaya ya Bukombe na Jimbo la Bukombe; na kwa kuwa Wilaya ya Bukombe yenye jimbo moja ina watu zaidi ya lakini tano na kitu na kwa hali hiyo inakidhi kabisa kuwa na majimbo zaidi ya mawili.

Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza akawahakikishia wananchi wa Bukombe mtakapogawa majimbo, Wilaya ya Bukombe mtaigawanya iwe na majimbo ili kumpunguzia mzigo Mbunge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maombi mengi zaidi ya 50 ambayo hadi sasa yamepokelewa na Tume ya Uchaguzi, mojawapo ni ombi kutoka Wilaya ya Bukombe na ni kweli kwamba Wilaya ya Bukombe ina wakazi wengi sana zaidi ya wananchi 500,000.

Lakini, wingi wa watu siyo kigezo pekee cha kumhakikishia Mbunge kwamba jimbo hilo litakuwa na majimbo mawili hapo baadae.

Kwa hiyo, Bukombe pamoja na majimbo mengine yataangaliwa kwa kuangalia vigezo vyote vinavyohusika ikiwa pia ni pamoja na ukomo wa hali halisi ya uchumi kuhimili Wabunge wangapi ambao weatakuwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Spika, lakini pia, ukumbi wako pia una ukomo wake.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea kidogo majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa kutoa masahihisho kidogo kwenye swali (b). Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilosa ina majimbo matatu:- Jimbo la Gairo lenye Kata nane, Jimbo la Mikumi lenye Kata kumi na mbili na jimbo la Kilosa la kwangu mimi lwenye kata kumi na saba. Kwa hiyo, si sahihi kuliambia Bunge kwamba kwamba jimbo la Mikumi ni kubwa kuliko Kilosa na Gairo yakiunganishwa pamoja. Kwa hiyo, naomba watakapopeleka maombi waseme ukweli. Asante! *(Kicheko)*

**SPIKA:** La! Haya mambo yanazidi kuwa magumu sasa! Bado tuko Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa wale tu wanaopenda takwimu, ukomo wa ukumbi huu ambao sasa hivi una Wabunge 323, ukomo wa mwisho ni 365. Tunaendelea!

Na. 150

**Ahadi ya Kujenga Kituo cha Afya Himo**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Himo unakua kwa haraka ukiwa na wakazi zaidi ya 30,000; na kwa kuwa ahadi ya kujenga Kituo Kikubwa cha Afya ilitolewa Bungeni mwaka 2006, Serikali iliazimia kutoa shilingi milioni hamsini (50,000,000/=):-

Je, ni sababu gani zinaifanya Serikali isitekeleze ahadi yake hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2006/2007, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 40,000,000/= ili kuanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya wagonjwa wa nje kwenye kituo cha afya cha Himo, kata ya Makuyuni katika mji mdogo wa Himo. Kutokana na wanafunzi wengi waliohitimu elimu ya msingi kufaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2006 na kukosa nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2007, fedha hizo zilibadilishwa matumizi ili kujenga madarasa

ya shule ya Sekondari. Kubadilishwa huko kwa matumizi kulifuata taratibu zote za fedha *(Reallocation Procedures)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za afya, Serikali inatambua kasi ya ukuaji wa mji wa Himo. Ni dhahiri kwamba ongezeko la watu katika mji mdogo huo halina budi liende sambamba na uboreshaji wa utoaji wa huduma za afya. Kama nilivyoeleza hapo awali, kwa mwaka uliopita mabadiliko ya matumizi ya fedha kwa mwaka yalitokana na vipaumbele vya Halmashauri katika kipindi kile. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 nguvu zimeekelzwa katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya kupitia Mpango wa Maalum wa Kitaifa wa Afya ya Msingi (MMAM). Hivyo, Halmashauri itashirikiana na wananchi wakati wa kuandaa mpango kata ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa kituo cha afya cha Himo unaingizwa katika vipaumbele. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2009/2010 shilingi milioni 50 zitatengwa katika ruzuku ya maendeleo ili kuanza ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ambayo sikuridhika nayo sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ahadi iliyotolewa hapa Bungeni ni ya kutoa shilingi milioni 50, na Hanasard ninayo! Pamoja na kamba shule ni muhimu, hata afya ni muhimu vile vile kwa wananchi. Je, Serikali haioni kutotimiza ahadi iliyotoa hapa Bungeni ni kuonyesha kwamba hawathamini wananchi wa jimbo la Vunjo? Swali la pili; Kwa kuwa kituo cha afya hakijajengwa mpaka sasa hivi na mji wa Himo sasa ni mji mdogo kwa kufuatana na Mipango Miji. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kugeuza kile kituo cha afya kuwa hospitali kamili ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge ahadi ile ilitolewa na ndio maana pesa hizi zilitengwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo ya kujenga kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza na wewe ninazo barua zote hapa, nimeziitisha ambazo zilitoa kibali cha kubadili matumizi ya fedha hizi ziende zikajenge shule. Barua hizo ninazo hapa, na kwa vile siwezi kuzisoma, mimi naomba nisome katika maeneo yale ambayo yamepitishwa.

Kwanza, kupitishwa katika kikao cha kamati ya fedha, uongozi na mipango tarehe 30/01/2007.

Pili, kupitihwa katika kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 31/01/2007.

Tatu, kupata kibali cha Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI Na. *LGCSBF/01*…na kuendelea, na kuendelea. Nne, kupata kibali cha Hazina, Kumb.CBC/54/251 na kuendelea, na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, hicho ndicho kilichotokea. Kwa hiyo, taratibu zote hizo, hakuna mahali popote ambapo Serikali imeonyesha kwamba inapuuza suala la kujenga

kituo cha afya. Tunaona kwamba ni muhimu na mimi nakubaliana na Mheshimiwa Bent Kimaro kwamba eneo hili ni eneo muhimu sana. Lakini hivyo ndivyo ilivyokuwa na hili jambo lilianzia na barua za kuomba vibali hivi kama nilivyoeleza ziko hapa.

La pili, ili kuonyesha kwamba tunajali jambo hili linalozungumzwa hapa, kwa sababu hapa tunazungumzia afya za watu, tunazungumzia maisha ya watu ndio maana nimesema kwamba zimetengwa tena milioni 50 katika projections zetu kwa ajili ya kuanzisha hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, sasa yako mawazo yanayokuja hapa yanayosema kwamba tunataka hospitali ya Wilaya, wazo hili ni wazo zuri sana Mheshimia Kimaro. Hili jambo linahusu bajeti, bajeti ni mpango wa Serikali unaonyesha matumizi ya pesa na namna zitakavyopatikana. Kwa hiyo, ikiletwa hapa na ikaonekana kwamba ni priority katika Halmashauri ile, kazi hiyo itafanyika kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na. 151

**Ujenzi wa Barabara za Vijijini**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujenzi wa barabara Wilayani na Vijijini ni pamoja na ujenzi wa madaraja:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga/kukarabati barabara ya Managha (Aori) – Riroda – Hoshan hadi Bonga?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga madaraja muhimu kwenye makorongo ya Hoshan na Endanachan?

(c) Je, Serikali Kuu inasaidiaje pale ambapo Serikali za Mitaa – Halmashauri zinapokosa uwezo wa kujenga madaraja muhimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Managhat (Aori) – Riroda – Hoshan hadi Bonga ni barabara inayopita kwenye makorongo makubwa matatu ambayo yanahitaji kila moja kujengewa daraja ambalo linakadiriwa kugharimu si chini ya shilingi milioni 700.

Hivyo, gharama za kujenga madaraja tu ni zaidi ya shilingi bilioni mbili ambazo kutokana na ufinyu wa bajeti ya Halmashauri pamoja na Serikali haitawezekana kuyajenga madaraja hayo kwa sasa. Kwa mwaka 2008/2009 kupitia fedha za Mfuko wa Barabara inaifanyia matengenezo ya muda maalum sehemu ya barabara ya Riroda - Managhat kwa shilingi milioni 28.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wialaya itajenga madaraja kwenye makorongo ya Hoshan hadi Bonga kwa awamu. Naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Babati ione uwezekano wa kuweka daraja moja kwenye Bajeti yake ya mwaka 2009/2010.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inazisaidia Halmashauri zinapokosa uwezo wa kujenga madaraja na miundombinu inayohitaji gharama kubwa pale Halmashauri husika zinapoijulisha Serikali na Serikali kuwa na uwezo wa kifedha. Utaratibu unaofanyika ni kuwasilisha maombi maalum Hazina ili kuona uwezekano wa kupata fedha kwa shughuli husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Babati kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 iliijulisha Serikali kuhusu daraja la Rugina lililokuwa kero kwa wananchi wa vijiji vya Gichameda na Magaga na wakaomba shilingi milioni 145 na Serikali baada ya kuyachunguza maombi hayo kuridhia iliwapatia Halmashauri shilingi milioni 132 za ujenzi wa daraja hilo ambalo limekamilika Januari 2009 na kuondoa kabisa kero ya wananchi wa maeneo hayo.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza kabisa nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali langu ni hivi. kwa kuwa ubora au uzuri wa barabara za vijijini zinazopitika wakati wote wa mwaka ni muhimu katika kuondoa umaskini vijijini; na kwa kuwa bajeti ya Serikali au Halmashauri zetu ni ndogo kukidhi haja hiyo.

Je, Serikali haioni umuhimu kisera kwamba Serikali Kuu ichukue jukumu la kujenga madaraja makubwa yale muhimu kwa kuwa Serikali za Mitaa haziwezi kutimiza haja hiyo?

Kwamba Serikali Kuu sasa ichukue jukumu la kujenga madaraja yote muhimu, yale madaraja makubwa ili kuhakikisha kwamba tunaweza kuwafikia wananchi kule vijijini kwa barabara zinazopitika?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nakei kama ifuatavyo:-

Kama ilivyokuwa katika maeneo mbali mbali na kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa maeneo yote yale ambayo miundombinu yake hasa madaraja yanaenda juu ya uwezo wa Halmashauri husika, Serikali Kuu iko tayari, imeishafanya hivyo na itaendelea kuwa tayari kuchukua jukumu hilo la kutenga fedha kwa ajili ya

ujenzi huo. Muhimu Halmashauri ifuate taratibu na kuijulisha Serikali Kuu ili tuweze kuweka kwenye bajeti za Serikali Kuu. *(Makofi)*

Na. 152

**Kuhusu Uharibifu wa Mazingira Unaofanywa na Kiwanda cha Ngozi Njoro – Manispaa ya Moshi.**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa Kiwanda cha Ngozi kilichojengwa katika Kata ya Njoro kinatoa harufu mbaya sana ambayo huathiri sana hali ya hewa kwa maisha ya wakazi wa Kata ya Njoro, Kaloleni na ni wazi kuwa hali hiyo kiwanda kinachafua mazingira:-

(a) Je, ni lini watalaam wa mazingira watakifanyia utafiti ili kujua sababu za kiwanda kutoa harufu mbaya kiasi hicho?

(b) Kwa kuwa harufu inayotoka ni mbaya kupindukia, kwa nini kiwanda hicho kisifungwe hadi hapo hali hiyo itakaporekebishwa ili kunusuru hali ya afya kwa wakazi wa maeneo niliyoyataja?

(c) Je, ni madhara gani yanayowapata wakazi hao kwa kuvuta hewa hiyo mbaya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Watalaam kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa MAZINGIRA (NEMC) na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi walikitembelea kiwanda hicho tarehe 23 Januari, 2009. Ziara nyingine ya aina hiyo ilifanyika tarehe 9, Februari, 2009. Lengo la ziara hizi ilikuwa ni kufanya tathmini ya hali ilivyo kiwandani baada ya uongozi wa kiwanda kuagizwa kuchukua hatua za kukabiliana na kero ya harufu mbaya. Katika ziara hizo ilibainika kuwa kiwanda kinakabiliwa na tatizo la uchakavu wa mitambo na pia mtambo wa kusafisha majitaka kiwandani haukidhi viwango vya ubora wa maji. Hata hivyo, hali ya utoaji harufu mbaya imedhibitiwa ipasavyo baada ya kiwanda kufanya yafuatayo:-

· Taka/masalia ya vipande vya ngozi vimeanza kuzolewa na manispaa.

· Motor za kuzungusha rotter za kuingiza hewa katika visima vya majitaka *(oxidation ponds)* zimetengenezwa.

· Mifereji ya kutoalea maji ndani ya kiwanda kwenda visimani imezibuliwa.

· Visima vya mwisho vya kupokelea maji yaliyochujika vimechimbwa zaidi ili kuongeza kina.

· Maua/miti maalum imepanwa kando ya visima vya majitaka ili kuboreshsa mandhari.

· Ukarabati wa aina mbali mbali ya miundombinu ndani ya kiwanda unaendelea.

(g) Mheshimiwa Spika, iwapo hali hii itaendelea kama ilivyo sasa, hakuna sababu ya kukifungia kiwanda hicho. Hata hivyo, watalaam wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Kituo cha Uzalishaji bora wa Viwanda *(CPCT)* watakwenda hapo kiwandani ili kuwasaidia kuandaa mpango endelevu wa matumizi ya ya rasilimali na uzalishaji bora.

(h)Mheshimiwa Spika, iwapo kiwanda kitaendelea kutoa harufu mbaya kwa muda mrefu, wananchi wangeweza kupata matatizo na athari mbali mbali ukiwepo uchovu wa akili, kupungua kwa uwezo wa kuona vizuri, kuwa na kichefu chefu, ukosefu wa usingizi, kupumua kwa shida na kuumwa kichwa. Lakini vile vile kiwango cha gesi kikiongezeka huweza kusababisha kuwashwa na macho, uchovu wa mwili, kupoteza kwa hamu ya kula na kukosa usingizi.

Nachukua fursa hii kusisitiza umuhimu wa viwanda ambavyo vimeanzishwa kabla ya ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004, kukamilisha taarifa zao za ukaguzi wa mazingira na kuziwasilisha Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza;

Mheshimiwa Spika, kwanza nimeridhika na majibu aliyotoa Waziri ni mazuri lakini kuna jambo moja dogo tu ambalo ningependa Waziri anihakikishie, baada ya kufanya ukaguzi katika kiwanda hiki halafu ndiyo hatua zinazozungumzwa sasa zikachukuliwa nilikaa na Manispaa kuwauliza kwa nini kiwanda hiki hakifanyiwi *EIA* ili tuweze kujua ni kiwango gani kiwanda kile.

Mheshimiwa Spika, Manispa waliniambia gharama ya kufanya *EIA* ni kubwa mno na Manispaa haiwezi kulipa, lakini njuavyo mimi mwenye kiwanda ndiye anayelipa gharama zile;

Je, Manispaa ni sahihi au siyo sahihi?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa kwa jitihada zake za kutembelea katika kiwanda kile na vile vile niseme tu kwamba kiutaratibu kiwanda hiki ni kiwanda cha zamani kimeanza tangu mwaka 1969, kwa hivyo kiwanda hiki hakiko katika viwanda ambavyo vinatakiwa vifanye *EIA*, *EIA* inafanyika katika vile viwanda ambavyo vinaanza baada ya sheria 2004, kiwanda hiki kinatakiwa kifanyiwe ukaguzi yaani *Environmental Auditing* na ndiyo nimesema hapa kwamba viwanda vile vyote ambavyo vimeanza kabla ya sheria ya mazingira ya mwaka 2004 vinatakiwa kisheria kutengeneza taarifa zao za

ukaguzi wa mazingira ili kuonesha kwamba shughuli zao za uendeshaji haziendi kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo sisi tutasimamia kwa karibu kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara.

Na. 153

**Vikwazo vinavyoukabili Muungano**

**MHE. MWANAHAMIS KHAMIS SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa Bunge la Bajeti mwaka 2008 Serikali ileleza kuwepo kwa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuwepo kwa vikao vya kujadili namna ya kutatua vikwazo vinavyokabili Muungano:-

(a) Je, vikwazo hivyo ndivyo vinaitwa kero?

(b) Je, Serikali inawza kutoa mfano wa vikwazo vinne ambavyo vinajadiliwa na havijapata ufumbuzi?

(c) Je, kwa uzoefu uliopo, ni kweli kuwa Taasisi ya Bunge na BLW hazina ulazima wa kuelewa hatua zinazofikiwa kila baada ya miezi mitatu au sita?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanahamis Said Mbunge wa viti maalum lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Katika kuhakikisha kwamba Muungano wetu unaendelea kudumu na kushamiri, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameteua Kamati ya pamoja ya SMT na SMZ chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais inayojadili na kutoa ufumbuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu Muungano wetu.

Masuala haya ya Muungano yanayojadiliwa yamekuwa yakipewa majina tofauti na wananchi pamoja na wanasiasa, lengo likiwa ni kupata ufumbuzi wake. Miongoni mwa majina hayo ni kama vile vikwazo vya Muungano, Kero za Muungano, matatizo ya Muungano, changamoto za Muungano na kadhalika. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba vikwazo vya Muungano ndiyo vinavyoitwa kero za Muungano.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia sasa masuala yote yaliyokuwa yamewasilishwa zikiwa ni kero zimeshajadiliwa, nyingine zimeshapatiwa ufumbuzi na nyingine zipo katika hatua za mwisho za kupatiwa ufumbuzi. Vikwazo vinne ambavyo bado ufumbuzi wake haujapatikana lakini vimo katika mchakato ni hivi vifuatavyo:-

(i) Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

(ii) Asilimia ya Mgawanyo na misaada kwa wahisani.

(iii) Namna ya kuchangia shughuli za Muungano.

(iv) Mapato kutokana na hisa za SMZ katika Bodi ya Afrika ya Mashariki.

(c)Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo ulazima wa kutoa taarifa za utekelezaji kwa Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi . hata hivyo, taarifa zimekuwa zikitolewa kila wakati kupitia kipindi cha maswali na majibu Bungeni, wakati wa vikao vya Bunge la Bajeti na pia kila mara baada ya vikao vya kamati ya pamoja.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza; Kwa kuwa ameeleza kwamba kuna baadhi ya mambo yameshapatiwa ufumbuzi wa uhakika juu ya Muungano,

Je, anaweza kutuambia ni yapi ambayo tumekwishapata uhakika hasa na kukubaliana kwamba haya sasa hayana matatizo yeyote?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, mafanikio yapo mengi lakini naomba nizungumze machache tu kama mfano.

Mheshimiwa Spika, kwanza tumefanikiwa kuwa na sheria moja juu ya uvuvi wa bahari kuu, sheria imeundwa sasa mapato yanagawanywa kati ya bara na viziwani hilo ni muhimu sana, pili sasa hivi sheria ya haki za binadamu ambayo zamani ilikuwa haifanyiki Zanzibar imekubalika yanafanyika Zanzibar pamoja na pemba na Unguja.

Mheshimiwa Spika, tatu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inashirikishwa kikamilifu katika shughuli za Afrika Mashariki na sasa hivi tayari miradi minane imepelekwa tayari kwa ajili ya kupata ufadhili au mikopo kutoka huko. Kingine ni kwamba sasa hivi sheria zote za Muungano ni lazima zipitishwe na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuidhinishwa, hayo ni baadhi ya mambo ambayo tumekubaliana kati ya SMT na SMZ.

**MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, kwa kuwa hizi kero zinazozungumzwa za Muungano kimsingi hasa zimo ndani ya Katiba na makubaliano ya Muungano kutokana na muda mrefu na wakati umebadilika, kwa mfano kutumia jina la Tanzania kwa madhumuni ya Tanzania Bara pekee hasa katika Wizara ambazo si za Muungano.

Je, ni kwa nini hasa hatutaki kubadilisha Katiba ili kuondoa haya matatizo yote kwa sababu kubadilisha vipengele vidogo vidogo bado kero zitaendelea kuwepo.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)**: Mheshimiwa Spika, Serikali ya Muungano haina tatizo kubadilisha Katiba na kila baada ya wakati inabadilishwa kwa mujibu wa matakwa na matashi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi wengine wote.

Mheshimiwa Spika, hili ambalo Mheshimiwa Mnyaa amelizungumza bado Serikali ya Muungano na Zanzibar si tatizo kwao kwa wakati huu.

Na. 154

**Kuongeza Mapato kutokana na Utalii**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya awamu ya nne imepania kuongeza mapato yake kupitia utalii.

Je, ni tahadhari gani zimezingatiwa kuhakikisha kuwa utalii ni endelevu na unazingatia hifadhi ya mazingira na kwamba unakuwa endelevu

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya madhumuni ya sera ya taifa ya utalii ni kukuza na kuendeleza utalii Ikiolojia na jamii (*ecotourism*), vile vile kukuza utalii kwa njia inayoratibiwa ili kuvutia wawekezaji binafsi na kuleta maendeleo endelevu ya utalii.

Aidha sura ya tano ya sera Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 imeainishwa mikakati ya kuendeleza utalii ikiwa ni pamoja na utalii unaozingatia mazingira na kipekee sehemu ya 5.2 inasisitiza sharti la Wawekezaji kufanya tathimini za athari za mazingira *EIA* kabla ya uendelezaji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha nmipango ya maendeleo hususan uwekezaji katika sekta ya utalii unakuwa endelevu, Wizara yangu kupitia mamlaka zake zinazosimamia maliasili katika sehemu zao, imekuwa ikiandaa na kufanyia mapitio ya mpango wa Jumla wa uendeshaji *General Management Plan* katka maeneo mbalimbali ya hifadhi za taifa mamlaka ya Ngorongoro na mapori ya akiba, hususani pori la akiba la Selous.

Mheshimiwa Spika, aidha shughuli zote za uwekezaji kwenye maeneo ya ardhi na miundombinu yake lazima zizingatie na zifuate na kukidhi viwango vya tathmini ya

athari za mazingira *Environmental Impact Assessment* kama inavyofafanuliwa kwenye sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 na kutambuliwa na sheria ya utalii ya mwaka 2008

**MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa majibu mazuri, naomba kuuliza maswali ya nyongeza.

(i)Kwa kuwa, utalii wa Tanzania hususani Tanzania Bara unategemea zaidi rasilimali za wanyamapori na kwa vile ongezeko la binadamu limekuwa kubwa sana hapa nchini na linagongana na mahitaji ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori hawa; Je, Serikali inazingatiaje suala hili la kujaribu kutafutia utatuzi wa mgongano huo?

(ii)Kwa kuwa, mgongano kati ya ongozeko la binadamu na uhifadhi wa wanyamapori ni kubwa zaidi maeneo ya kaskazini mwa nchi kuliko kusini mwa Tanzania, Je, Wizara ina mikakati gani ya kuondoa wingi wa Watalii kaskazini na kuhakikisha kwamba utalii unaongezeka sasa kusini ili tupunguze uharibifu wa mazingira katika hifadhi zilizo kaskazini mwa nchi.

**NAIBU MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na ongezeko la binadamu na migongano mikubwa ya uhifadhi, au maeneo yaliyohifadhiwa na wananchi yameongezeka, katika kutatua tatizo hili hivi karibuni Wizara ilileta mapendekezo ya sheria hapa Bungeni ya uhifadhi wa wanyamapori ambayo Bunge lako liliridhia, katika sheria ile tulikusudia kuya-*address* matatizo haya ambayo yamekuwepo na ninaamini sheria hiyo itakapopata saini ya Mheshimiwa Rais na kuwa sheria na kanuni zake kuandaliwa, matatizo mengi tuliyonayo kwa hivi sasa yatakwisha.

Mheshimiwa Spika, katika ku- *diversity tourist destinations* Wizara yangu ina mpango wa muda mrefu wa kutangaza maeneo mbalimbali ya vivutio tulivyonavyo, lakini kabla ya kuanza kuyatumia maeneo haya tumekuwa tukisisitiza sana uboreshaji wa viashiria au vivutio vya wageni hasa miundombinu na uwekezaji kwenye sekta ya malazi *accommodation facilities* na hili kwa sasa hivi linakwenda vizuri mikoa ya kusini sasa barabara zake nyingi zimeshafunguka na ukanda wa nyanda za juu kusini barabara zake ni nzuri, na utakapokamilika uwanja wa ndege wa Songwe tunaamini kwamba upande huo utaweza kufunguka.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo miundombinu baada ya kuwa imeshaboreka kama inavyoelekea sasa hivi naamini upande wa kusini wa nchi yetu utapata wageni wengi zaidi kuliko ilivyokuwa kabla.

Na. 155

**Uwindaji haram,u kwenye Mbuga za Wanyama**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa Bunge la Bajeti la mwaka 2008 wabunge walitaka kujua sababu za kushamiri kwa uwindaji haramu kwenye mbuga za wanyama nchini ikiwa ni pamoja na kiasi cha meno ya tembo yaliyokamatwa mkoani Iringa mnamo mwezi April 2008 wakitajwa wahusika na hatua zilizochukuliwa dhidi yao, na kwa kuwa Serikali haikutoa takwimu zozote:-

(a)Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kudhibiti uwindaji haramu?

(b)Je, ni kiasi gani cha meno kilikamatwa na meno haya yana thamani gani?

(c)Je, ni akina nani wahusika na hatua gani za kisheria zilichukuliwa dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swai la Mheshimiwa Godfrey Zambi Mbunge wa Mbozi Mashariki lenye sehemu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jukumu la ulinzi wa wanyamapori dhidi ya uwindaji haramu ni la Wizara ya maliasili na utalii, wadau wote wa uhifadhi wanyamapori , Halmashauri za Wilaya na wananchi wenyewe. Katika kutekeleza jukumu hili Wizara yangu huendesha doria za kawaida za msako katika maeneo mbalimbali nchini kwa madhumuni ya kuzuia wanyama wasiuawe na kukamata majangili waliohusika pamoja na kuokoa nyara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya kupunguza idadi ya wanyama wanaouawa na kukamata majangili, bado zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili Wizara yangu zikiwemo upungufu mkubwa wa watumishi na uhaba wa vitendea kazi muhimu.

Aidha, Wizara yangu imebuni mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo kwa kuongeza nguvu katika intelijinsia na kuongeza doria za anga katika mapori na pia kuwashirikisha wadau na wananchi watoa habari kwa karibu.

Aidha Muswada wa Sheria mpya ya Wanyamapori uliopitishwa na Bunge lako Tukufu unategemea kutoa nafasi ya kuimarisha zaidi kikosi dhidi ya ujangili na kuwashirikisha wananchi kulinda rasilimali za wanyamapori kwa njia ya kutenga maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori(*WMAs*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Julai 2008, meno mawili ya tembo yalikamatwa katika kizuia cha Polisi cha Igumbilo kilichopo Wilayani Iringa kwenye barabara kuu ya kutoka Iringa kuelekea Morogoro. Meno hayo yalikuwa na uzito wa kilo 29 na thamani ya Tsh. 1,945,900.00 na yalikamatwa na Polisi wa kituo cha Iringa Mjini, yakiwa yanasafirishwa kwenda Dar es Salaam.

Watuhumiwa watano waliohusika walikamatwa na kufunguliwa mashitaka, kesi namba CC/310.2008 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Iringa. kesi hiyo bado inaendelea kusikilizwa na watuhumiwa wako nje kwa dhamana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali haya yafuatayo:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Spika, sababu ambazo pia Mheshimiwa Naibu Waziri pia amekiri kwamba zinasababisha kikosi kile kinachopambana na wawindaji haramu kinakosa vitendea kazi muhimu kama magari pamoja na upungufu wa askari.

(i)Je, Wizara inachukua hatua gani za dharura kuhakikisha kwamba tunakabiliana na hali hiyo ili kuokoa wanyama wetu wasiendelee kuawawa ovyo.

(ii)Kwa kuwa, Muswada wa sheria ya wanyamapori ambao tumeupitisha juzi tunategemea uwe sheria baada ya Mheshimiwa Rais kuusaini, lakini kumekuwa na uchelewaji wa sheria hizihata baada ya kusainiwa kuanza kutumika kwa sababu tu kanunui huwa zinachelewa sana kutengenezwa, Je Wizara hii imejiandaa namna gani kuhakikisha kwamba kanuni ambazo zitaongoza utekelezaji wa sheria hii zinatungwa mara moja ili baada ya sheria hii kusainiwa ianze kutumika mara moja.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mhehsimiwa Spika, kwanza kabla ya kujibu maswali yake naomba nimshukuru sana kwa concern ambayo amekuwa akionesha kwenye suala zima la uhifadhi wa rasilimali wanyamapori na ninaamini kwa jitihada hizi pamoja na Wabunge wengine na wananchi wengine tutafanikiwa kwa pamoja kupunguza matatizo yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, jitihada ambazo tunafanya sisi kama Wizara kwa sasa hivi ni kwamba katika kipindi cha miaka michache iliyopita tulikuwa na matatizo makubwa ya vitendea kazi, tumekuwa tukiongeza Bajeti kwenye eneo hili na kwa mwaka uliopita tuliongeza bajeti ya eneo la wanyamapori karibia mara moja na nusu ya bajeti ya mwaka uliotangulia.

Kwa kufanya hivyo tumeweza kununua vifaa vichache zikiwemo silaha za kisasa ambazo zinatumika na vikosi vyetu, ingawa hali haijawa nzuri sana lakini tutaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, jibu ambalo tunategemea linaweza likasaidia sana ni kuanzishwa kwa mamlaka ambayo imependekezwa kwenye kifungu cha 8 cha sheria mpya ya wanyamapori ambayo Bunge lako liliridhia hivi karibuni. Tunaamini baada ya sheria hiyo kuwa imeanza kutumika mambo ambayo yanajitokeza sasa hivi yataweza kupata jibu.

Mheshimiwa Spika, kuusu uandaaji wa kanuni ni kweli tulikuwa tunajua kwamba tatizo tulilonalo ni kubwa na sheria inahitajika haraka kwa hivi Wizara tayari ilishaanza

kuandaa rasimu za kanuni na tunategemea katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja baada ya sheria kupitishwa kanuni hizi zitakuwa zimekamilika.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali la nyongeza;

Kwa kuwa, vipo vizuizi mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya kukagua mazao ya misitu pamoja na kuangalia nyara za Serikali, na kwa kuwa imegundulika kwamba baadhi ya nyara ambazo zinakamatwa nchi za nje, mfano mwaka jana kuna kontena limekamatwa likiwa na vipusa au meno ya tembo  na kwa kuwa kwenye aiport zetu pamoja na bandari pia uchunguzi wa kuhakikisha kwamba vitu kama hivyo havisafiri kinyume na sheria.

Serikali inatuambia nini kwamba vitu vinavyokamatwa nje kama nyara za Serikali na meno ya tembo vinasafirije  mpaka kukamatwa nje wakati Serikali haijui?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, pamoja na ukaguzi kufanyika mara kwa mara ieleweke kwamba majangili au watu wanaosafirisha nyara kinyume cha sheria ni watu ambao wanatumia mbinu mbalimbali, kwa hivyo mara nyingine inatokea kwamba nyara zinakuwa zinafichwa katika mazingira ambayo ukaguzi unakuwa si rahisi kuziona, unakuta mara nyingine nyara zinakuwa zimewekwa kwenye *sealed containers* ambazo zina bidhaa zingine na inakuwa siyo rahisi kuhisi kuhisi kwamba kunaweza kukawekwa nyara na watu kama hawa unaweza ukakuta kuna *documents* zinazoonesha kwamba makontena yale yamechukua bidhaa tofauti na nyakati nyingine wanakuwa documents ambazo ni *forged* kwa hiyo wanapopita kwenye vituo wanaonyesha vibali ambavyo kwa haraka haraka unaweza ukaona kwamba ni halali lakini kumbe ni *forged documents*

Mheshimiwa Spika, mbinu zinazotumika ni nyingi lakini tumejipanga na tunashirikiana na wenzetu kupitia *RUSAKA agreement* kwa hapa Afrika lakini pia kwenye mkataba wa *CITES* ambao pia tubafabya kazi kwa pamoja kwa maana hiyo mtu anaweza akakwepa hapa na akaweza kukamatwa sehemu nyingine kama ilivyotokea kwenye kontena ambalo lilikamatwa Taiwan miaka michache iliyopita.

Na. 156

**Kuimarisha Kituo cha Polisi cha Nyanguge**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kkuwa, Mji Mdogo wa Nyanguge Jimboni la Magu unakua haraka na umezungukwa na mialo mingi ya uvuvi na hivyo kusababisha matukio ya mara kwa mara ya uharibifu; na kwa kuwa kituo cha Polisi cha Nyanguge hakina nyumba hata moja ya askari, hakina ghala la silaha, gari wala pikipiki:-

Je, kwa nini Serikali haijaona umuhimu wa kuiimarisha kituo hicho, ambacho kipo katikati ya mji wa Magu Mwanza na hivyo kuwa ni cha muhimu sana kuimarishwa ili kusogeza zaidi huduma kwa wananchi wanaotaabika sana hivi sasa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji mdogo wa Nyanguge ulioko katika Jimbo la Magu unakua haraka na umezungukwa na mialo mingi ya uvuvi ambayo ni Nyakasenge, Mwanchimwa, Mwangomba, Deke na Maneto na kwamba kituo hicho hakina hata nyumba moja ya kuishi askari wala gari au pikipiki.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kukiimarisha kituo hicho kwa kujenga majengo ya Ofisi na nyumba za kuishi askari. Hata hivyo kwa sababu ya ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya maendeleo ya Jeshi la Polisi itatuwia vigumu kujenga kituo na nyumba za kuishi askari katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha ulinzi kwa kufanya doria na operesheni kwa lengo la kuhakikisha usalama wa maisha na mali za wananchi wa eneo hilo unadumishwa ili kuwawezesha kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na kwamba anatambua umuhimu wa kukiimarisha kituo hiki na kwamba anakubaliana na mimi kwamba Mji mdogo wa Nyanguge unakua haraka na unazungukwa na shughuli za uvuvi na zinginezo, lakini pamoja na kutambua ukweli huo ni kwamba Serikali haiwezi kukiimarisha kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, Waziri atatufanyia msaada mkubwa sana akikipandisha kituo hicho kwa kutupatia *investigation register* badala ya *report book* peke yake kwa sababu ya matukio yalivyo mengi.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba kituo hiki kipatiwe *investigation register* badala ya *report book* peke yake?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimepokea ombi hilo kutoka kwa Mheshimiwa Limbu nitawasiliana na IGP ili kuangalia ni namna gani tunaweza kuboresha kituo hicho katika hali hiyo aliyouliza na katika njia yeyote ile nyingine ambazo tunaweza tukafanya ili kuimarisha ulinzi katika Wilaya ya Magu.

Na. 157

### Gharama za Washtakiwa

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Wilaya ya Kahama, wananchi hufikisha mashataka katika Ofisi za Serikali za Kata na Tarafa, ambayo hupelekea watuhumiwa kuwekwa ndani na wakati mwingine kufikishwa Mahakamani.

Kwa kuwa Wilayani hapo wananchi wamekuwa wakitakiwa kuchangia fedha kwa ajili ya mafuta ya Polisi kwenda katika maeneo ambayo vifo vya kutatanisha vimetokea:-

(a) Je, ni nani anahusika kugharamia gharama za chakula na kuwahifadhi wahalifu katika mahabusu yaliyopo katika Ofisi za Kata, Tarafa; na ni nani anahusika kugharamia usafiri wa watuhumiwa kati ya mwananchi aliyetoa mashtaka au Serikalini?

(b) Je, ni nani anahusika kugharamia mafuta ya gari la Polisi kwenda kwenye eneo la tukio la mauaji kati ya Serikali na mwananchi wa eneo ambalo mauaji yametokea

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James D. Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, anayehusika kugharamia chakula na kuwahifadhi watuhumiwa katika mahabusu zilizoko katika Ofisi za Kata au Tarafa ni Mkuu wa Polisi wa Wilaya husika.

Iwapo Mtendaji wa Kata au Tarafa atagharamia chakula cha Mahabusu atatakiwa kuwasilisha maombi ya kurudishiwa fedha alizotumia kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya husika ambaye naye ataandaa nyaraka za kuomba kupatiwa fedha hizo kutoka kwa Mkuu wa Polisi wa Mkoa na hatimaye kurudishwa kwa Watendaji wa Kata au Tarafa.

Hata hivyo pale ambapo mtuhumiwa atakuwa amefikishwa Mahakamani na kukosa dhamana, huwekwa mahabusu ya Ofisi ya Mtendaji wa Kata au Tarafa na gharama za chakula zitalipwa na Mtendaji huyo na gharama hizo atarudishiwa na Mkuu wa Gereza wa eneo hilo baada ya kukamilisha taratibu husika.

(b)Mheshimiwa Spika, jukumu la kugharamia mafuta ya gari la Polisi kwenda kwenye eneo la tukio mara yanapotokea mauaji ni la Serikali na siyo wananchi wa eneo lilikotokea tukio.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika nimpongeze Mheshimiwa Waziri majibu mazuri ingawaje kwenye maeneo husika hayatekelezeki haya anayoyataja labda ajionee mwenyewe akitembela huko.

(i) Kwa kuwa, Wilaya ya Kahama na Wilaya ya Bukombe zina matukio mengi sana ya uhalifu na ndiyo maana imeelekeza mahabusu wengi kuwekwa katika ofisi za vijiji, Kata, na hata Tarafa, na kwa kuwa hali hiyo inasababisha kukosekana kwa amani ya wananchi wa maeneo hayo.

Je, Serikali inakubaliana na mimi kwamba inaweza ikaunda Kanda maalum eneo la Bukombe, Kahama au Kanda ya Ziwa ifanane na Dar es Salaam kwa ajili ya kupambana na ujambazi huu lakini pia hapo hapo bajeti ya mafuta katika Wilaya ya Kahama na Bukombe iongezwe?

(ii) Kwa kuwa katika gereza la Kahama, mahabusu wengi waliopo pale na wafungwa, wengi wa mahabusu kesi zao zinacheleweshwa sana na mimi nilitembelea pale muda si mrefu, na hii inatokana na upelelezi kuchelewa.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuunda *task force* ya kwenda kusaidia upelelezi wa kesi katika Wilaya hizo ili usumbufu katika gereza hilo la wananchi wa Wilaya ya Bukombe na Kahama wapate ahueni?

**SPIKA:** Majibu kwa maswali ninayoyaona matatu hayo, kuna kuundia Kanda Maalum, kuongezewa mafuta na kuunda *Task Force.*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2009 mimi pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria tutafanya ziara rasmi katika Mkoa wa Shinyanga, tutaendelea kutembelea maeneo mbalimbali akiwemo Kahama na Bukombe, tutaangalia hayo matatizo kwa ukaribu, na baada ya kutoka huko tutayapatia majibu.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imetoa majibu kwamba huwa Polisi wana-*refund* wale wahusika na suala hili halitekelezeki; na kwa kuwa hao watendaji wa Tarafa na Kata wamekuwa wakifanya kazi nyingi mbalimbali zinazowahusu Polisi, na kwa kuwa wamekuwa wakutumia gharama zao kwa muda mrefu sana na bila kurudisha. Je, Serikali ina mpango gani sasa hivi wa kuwaacha watendaji wa Tarafa na Kata wafanye kazi zao badala ya kufanya kazi za Polisi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ningependa kutokubaliana na Mheshimiwa Mwanawetu kwamba hiyo *refund* haitekelezeki. Suala la *refund* linatekelezeka ni suala la kufuata utaratibu. Nitachomwomba Mheshimiwa Mbunge ni pale ambapo anaona kuna tatizo katika hiyo *refund process* waje kwetu kama Wizara tufuatilie na wenzetu ili tuhakikishe kwamba hizo fedha zinarudi katika eneo husika.

Na. 158

**Mikopo kwa Wananchi wa Jimbo ya Nyang'hwale**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, Serikali ilitamka na kuthibitisha kuwa katika mgao wa awamu ya kwanza fedha za ujasiriamali toka Jimbo la Nyang'hwale hawakupata mgao huo wa awamu ya pili:-

Je, hadi sasa swali hili linapojibiwa ni wajasiriamali wangapi wameshapata mkopo huo na ni shilingi ngapi zimeshakopeshwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, swali lake kama ifuatavyo:-

Wakati nilipokuwa nawasilisha majumuisho ya majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwenye hotuba ya Wizara yangu kwenye Kikao cha Kumi na Mbili cha Bunge lako Tukufu ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Musalika, nilieleza kuwa Serikali imeshatoa maelekezo kwa Benki Kuu kutoa fedha kwa ajili ya kuwakopesha wajasiriamali wa Wilaya ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza ikiwa ni pamoja na Jimbo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza kwa ufupi kuwa utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Benki Kuu tayari imetekeleza maelekezo ya Serikali kwa kufanya yafuatayo:-

(a)Benki imeshatoa fedha za mikopo kwa Benki na Asasi za fedha zilizokubali kusimamia utoaji wa mikopo kwa wananchi wa Wilaya ambazo ziliainishwa kufaidika katika awamu ya pili, (Wilaya zilizokosa kabisa na zile zilizopata mgawo chini ya kiwango).

Hadi sasa ni Benki ya Biashara ya Akiba (Akiba *Commercial Bank*) mabayo imejitoa katika utekelezaji wa mpango huu na tayari Benki Kuu, imeshachukua hatua ya kutafuta benki/Asasi nyingine itakayochukua nafasi ya Benki ya Akiba *Commercial Bank* kwa Wilaya ya Rungwe na Longido na kuhakikisha kuwa wananchi wa Wilaya hizo wanaendelea kupata mikopo kama ilivyokusudiwa.

(b)Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2008 jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4,198,741,950 ilishatolewa kwa wananchi wa Wilaya lengwa yaani kwa maana ya awamu ya pili takribani 44 kupitia *SACCOS* na Vikundi.

(c) Benki Kuu imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kama gawiwo kwa Wilaya na maeneo ambayo yalikuwa na mahitaji maalum na kuainishwa na Serikali kupewa kipaumbele hapo awali. Benki inaendelea kutathmini benki/ Asasi za fedha mahiri za kuhudumia maeneo hayo ikiwa ni pamoja na eneo la Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, napenda kumweleza Mheshimiwa Musalika kuwa ombi lake la fedha za mikopo kwa ajili ya wananchi wa Nyang'hwale halijasahaulika. Benki ikishakamilisha taratibu muhimu za kupata benki/Asasi za Fedha kwa maeneo yote yaliyoainishwa wananchi wa maeneo hayo wataanza kupata mikopo kufuatana na taratibu za mikopo chini ya Mpango huu. Tunamwomba Mheshimiwa Musalika awaeleze wananchi wa Nyang'hwale kuvuta subira na waendelee kujiandaa kwa kuwa na miradi inayokidhi masharti ya mikopo na kuimarisha *SACCOs* na vikundi vyao kwa kuweka akiba zitakazowawezesha pia kukidhi masharti ya kupata mikopo mara watakapofikiwa.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu marefu sana yasiyo na matumaini ya karibu kwa wapiga kura wangu na yasiyoingia akilini kwa kweli. Napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

La kwanza, kwa kuwa ahadi ya Serikali kuwapa wananchi hao ambao hawakupata awamu ya kwanza ilitolewa mwaka 2007; na kwa kuwa mwaka 2007 hiyo na mwaka 2008 mpaka sasa hivi ni mwaka wa tatu, na mimi nilikwishauliza na hili ni swali la nne na bado Serikali inaahidi; na kwa kuwa wananchi tayari wanayo michanganuo, wanavyo vikundi, *SACCOS* na watu binafsi wapo wamejiandaa kusubiri fedha hizi.

Je, Serikali, Naibu Waziri anaweza kutwambia kwamba utekelezaji wa hili upo kwenye kasi gani, kwa sababu siyo kasi mpya wala siyo kasi ya zamani, ni kasi ipi na lini watapata hizo hela wananchi wa Nyang'hwale?

La pili, kwa kuwa Mfuko huu wa mabilioni ya JK ulitangazwa na Serikali na Waheshimiwa Wabunge tulielekezwa tukawahamasishe wapiga kura wetu na *SACCOs* nyingi sana zimeundwa. Lakini kwa kuwa hali halisi ilivyo Mfuko huu hautoshi ni mdogo na ni chini pengine ya asilimia 5 ya watu ambao wamejiandaa kwa Mfuko huu kupokea ndiyo wanapata.

Je, Serikali ipo tayari kubadilisha mfumo wa Mfuko huu pengine ili uchangiwe na wadau mbalimbali kama vile Mifuko ya KR *one* ili wananchi wengi zaidi waweze kupata hasa wakulima wadogo wadogo ambao ndiyo mizizi ya uchumi wa nchi?

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kazi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kinachofanyika na Benki Kuu na Serikali kwa ujumla kwa Jimbo la Nyang'hwale ni kama *special case* kwa sababu Benki Kuu na taratibu huu

kwa ujumla fedha zilikuwa zinaenda Kiwilaya, lakini makosa yaliyofanyika katika Wilaya ya Geita ndiyo hiyo ilituletea matatizo haya.

Kwa kweli fedha hazitolewi Kijimbo *in such*, na ndiyo maana katika mgao wa kwanza, awamu ya kwanza Wilaya ya Geita ilipata milioni 837 kama wangekuwa wameziweka kwenye utaratibu mzuri kwa Majimbo matatu kila Jimbo lingeweza kupata zaidi milioni 200. Lakini kwa sababu utaratibu kwa Wilaya ya Geita haukwenda vizuri, Jimbo la Nyang'hwale likawa na matatizo hayo.

Sasa sisi tunajaribu kurekebisha na mimi ninamhakikishia kwamba kwa sasa taratibu zinakwenda vizuri ili na Jimbo hilo ambayo kwa kweli limepunjwa na Majimbo mengine ya Wilaya ya Geita waweze kupata hizo fedha, na mimi nina hakika kwa sababu tumependekeza wapate milioni 100 hivi karibuni na kwamba *PRIDE* ndiyo waende kule kuhudumia nadhani hili litafanyika haraka iwezekanavyo.

La pili, kwamba tubadilishe mfumo huu. Mimi nasema kwa sasa Serikali inajaribu kutathmini jinsi ambavyo awamu ya kwanza na ya pili ya Mfuko huu ulivyokwenda. Serikali itaendelea kupata mawazo mbalimbali namna ya kuboresha mfuko huu au kuuongezea.

Lakini kwa sababu ni *revolving fund* tunategemea kwamba mfuko huu uwe endelevu na kama kutakuwa na mfumo mpya utaongezea.

Na. 159

**Soko la Ajira kwa Vijana**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

(a) Je, ni vijana wangapi na ngazi ipi au vikundi vipi toka shule za msingi, sekondari, Chuo Kikuu, Vyuo vya Ufundi wanachangia kwenye soko la ajira kila mwaka?

(b)Je, ni vijana wangapi kwa sasa hivi walimaliza Elimu ya Sekondari, Vyuo vya Elimu ya Juu na Chuo Kikuu ambao hawana ajira hadi tarehe 30 Machi, 2006 wakiorodheshwa kwa makundi yao, na je, ni sababu gani za msingi zinafanya ajira hasa kwa vijana hawa waliohitimu Vyuo vya Juu iwe ngumu, na Serikali ina mikakati gani ya muda mrefu ya kupambana na tatizo hilo ambalo lisipodhibitiwa itakuwa ngumu zaidi hapo baadaye?

(c) Pamoja na kuwa na Serikali hutoa kama kasma kwa Idara mbalimbali za Serikali, je, Serikali inaweza kutoa kauli ya uwezo wake wa kuajiri kwa kila mwaka kwa kila kikundi ni kiasi gani, uwezo wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ni kiasi gani, uwezo wa sekta binafsi hasa makampuni ni kiasi gani, na ni vijana wangapi wanaweza kujiajiri kwa kuwezeshwa katika sekta isiyo rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba, kwa wastani vijana 334,652 waliohitimu elimu ya msingi kwa mwaka 2007 hawakuendelea na elimu ya sekondari. Vijana 80,685 waliohitimu kidato cha nne hawakuendelea na elimu ya kidato cha tano na vijana 3,186 waliohitimu kidato cha sita hawakuendelea na elimu ya Vyuo vya Elimu ya Juu.

Vijana 26,518 walihitimu mitihani inayotolewa na *VETA* kwa ngazi mbalimbali, na vijana 475 walihitimu elimu ya Ufundi. Hivyo basi, jumla ya vijana 474,936 waliingia kwenye soko la ajira mwaka 2007 kutoka elimu ya msingi, sekondari, ualimu, na elimu ya *VETA.*

(b) Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijaweka utaratibu wa kuwafuatilia wahitimu wa shule na vyuo (*Trace study*) ili kujua hali halisi ya ajira zao pindi wanapohitimu Vyuo na shule. Hata hivyo, matokeo ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2006 yanaonesha kwamba jumla ya vijana 1,398,677 kama asilimia 13.4 hawana kazi ambao kati yao vijana wa kiume ni 598,015 au asilimia 12.3 na wa kike ni 800,662 kama asilimia 14.3.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mikakati ya Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi ni kama ifuatavyo:-

1. Kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008, Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 pamoja na programu ya Kukuza Ajira ya mwaka 2007 ambazo zimezingatia maeneo ya vipaumbele kwenye sekta mbalimbali katika kukuza ajira.

2. Serikali kwa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, imeweza kutoa mikopo (mabilioni ya Kikwete) kwa Mikoa yote nchini ili kukuza uchumi hususan kuongeza ajira. Takriban wajasiriamali 44,256 walipata mikopo hiyo hadi Juni, 2008.

3. Kutoa vivutio mbalimbali vya uwekezaji kutoka nje na ndani ya nchi kwenye sekta zenye uwezo wa kuongeza fursa nyingi za ajira.

4. Kuanzisha Wakala wa Huduma ya Ajira na kuongeza vituo vya Huduma ili kuwafikia vijana wengi zaidi na hivi sasa tayari tawi la Kituo cha Wakala wa Huduma za Ajira kimefunguliwa huko Mwanza ukiacha kile cha Dar es Salaam na mipango ipo mbioni kuja kufungua Arusha, Mbeya, Mtwara na Dodoma.

5. Katika kuwajengea vijana uwezo wa kukua kiuchumi hasa kujiajiri katika sekta isiyo rasmi, Wizara yangu imeendelea kutenga fedha za kuwakopesha vijana. Kwa mwaka 2007/2008 jumla ya Wilaya 97 zilikopeshwa jumla ya shilingi milioni 364,591,208. Hata hivyo, kwa mwaka huu wa fedha, Wizara imebuni utaratibu wa kuwakopesha vijana kupitia katika Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*) ambapo kila Wilaya imeainisha *SACCOS* mbili za vijana na hela zimeanza kupeleka tayari.

6. Kuhamasisha Jamii kuanzisha Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (*SACCOS*) nchi nzima kama njia ya kuiwezesha jamii kupata mikopo yenye masharti nafuu.

(c) Mheshimiwa Spika, utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi unaonesha kwamba Serikali na Taasisi zake ina asilimia tatu ya wafanyakazi kati ya wafanyakazi wote nchini ni milioni 16,627,133. Kilimo kinaongoza kwa kutoa ajira nyingi nchini (75.1%) ikifuatiwa na sekta isiyo rasmi (10.1%). Aidha, utafiti huo unaonesha kwamba jumla ya vijana walio kwenye sekta isiyo rasmi ni 975,782 sawa na 58% ya watu wote walio katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa waajiri wote nchini kuwapa vijana kipaumbele kwa suala la ajira kwa kuwa vijana ni nguvu kazi inayopaswa itumike kikamilifu kwa ustawi wa Taifa letu.

Vilevile kwa kuwa ajira ni suala mtambuka, kila mdau anawajibika kusaidia kupunguza tatizo la ajira hususan miongoni mwa vijana.

Serikali imeweka mazingira mazuri ili vijana wengi waweze kujiajiri katika sekta isiyo rasmi. Mfano wa karibuni kabisa ni ujenzi wa jengo linalojengwa na *NSSF* Jijini Dar es Salaam yaani Machinga *Complex* ili kuwapatia vijana walio katika sekta isiyo rasmi eneo zuri la kufanyia biashara zao.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, Waziri atakubaliana nami kwamba vijana ni msingi na nguzo ya Taifa lolote leo na hata Taifa la kesho.

Sasa katika hali hiyo kwa kuwa, hiki kiasi cha fedha na watu waliofikiwa kwa Mfuko walioita wa mabilioni ya Kikwete ni 44,000 tu. Hivyo kwa hesabu ya haraka haraka itachukua zaidi ya miaka 20 kuwafikia vijana wetu.

Lakini pia fedha inayotengwa kwenye Wizara ni shilingi milioni 364 kwa Wilaya 97. Je, tunaweza tukaanza mkakati wa aina gani kuwawekea hao vijana wetu pamoja na jitihada alizoeleza Naibu Waziri ambazo nafikiri haziwagusi na haziko *coordinated* ili

ziweze kuwafikia hao vijana wetu wote na ziweze kuwanufaisha hasa wale ambao wapo kwenye maeneo ya vijijini ambao kweli tunawaambia wana ajira kwenye ardhi, lakini hawana mashamba wapo kwenye maeneo ya biashara, lakini kazi wanazofanya ni labda zile za biashara ya kutwa. Tuwe na mkakati gani wa Kitaifa kuwasaidia vijana hawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kwa kifupi la kwanza limekuwa refu pia.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, la pili, katika hali ya kawaida tunaona kwamba sekta binafsi kweli ndiyo inayoajiri na ndiyo Naibu Waziri ametoa msukumo; kwa kuwa mishahara yao ni midogo na kuna ushahidi wa manyanyaso mbalimbali ambayo hata juzi niliyauliza hapa na Waziri anayehusika akaniambia ni suala la Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Je, Wizara itaweka mkakati gani kuhakikisha kwamba kwenye sekta binafsi vijana wetu wanaangaliwa na wanapata ajira kwa mujibu wa sheria zilizopo na zinasimamiwa kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI, WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza la mikakati tufanye mimi nadhani kama nilivyoeleza hii mikakati tuliyoiweka ya mabilioni ya JK ya Mfuko wa Vijana ni baadhi tu ya mikakati ambayo kwa kweli itawasaidia sana vijana. Idadi kweli ni ndogo lakini mimi naamini kabisa kwamba kuna mikakati mingine katika sekta zingine ambapo zinaweza zikawapa vijana ajira na hasa kwenye kilimo.

Yeye mwenyewe amezungumzia suala la kilimo kwamba huko vijijini vijana wanatakiwa waboreshewe hali ya kilimo Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeweka mikakati ambayo siyo tu kuboresha kilimo kwa maana ya watu wengi kufikiwa lakini vile vile na kuweka na utalaam kwa maana ya nyenzo za kisasa za kilimo. Mimi nina hakika vijana wakihamasishwa kuendelea kwenye sekta ya kilimo, sekta ya viwanda na hata sekta ya miundombinu ambapo vijana wanapata ajira kwenye ujenzi wa barabara na kadhalika tunaweza tukafikia lengo letu. Itachukua muda ni changamoto kubwa lakini nina hakika mbalimbali ambayo Serikali imeweka tutafanikiwa.

Kuhusu mishahara midogo kwenye sekta binafsi kama ambavyo tunajua hili suala tumelishughulikia tuna sheria suala ambalo linafanyika sasa ni kusimamia hizi sheria na vile vile bodi ya mishahara ambayo imeanzishwa inafanyakazi yake. Hivi karibuni Serikali itakuja kutoa maelezo namna gani sasa ile mishahara kima cha chini katika sekta binafsi kwenye maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa yametolewa yataboreshwaje. Kwa hiyo, hili Serikali inalishughulikia vile vile.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea kidogo kwenye jibu zuri alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba tunachoomba kama Wizara ni taarifa pale ambapo unapoona sheria za kazi hazitekelezwi sawa sawa. Kwa hiyo, kama kuna tarifa sahihi atuletee Mheshimiwa Mbunge sisi tutafuatilia. Tunavyo vitengo vya kufuatilia kuhakikisha kwamba haki inatendeka.

Lakini vile vile kuna malalamiko mbalimbali hata hata kwenye Chama cha Madereva, kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hamuwalipi madereva wenu kwa mishahara ya kima cha chini. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kwamba sasa muanze kulipa madereva wenu mishahara stahili kama sheria inavyotaka. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika maelezo ya ziada katika swali hili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ambayo yametolewa na Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda ningependa kutoa majibu ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ambayo inaweza ikaajiri vijana kwa wingi zaidi hasa wanaoishi vijijini ni sekta ya kilimo. Kwa hiyo, swali kwamba kuna mikakati kuna mikakati gani ndiyo linahitaji kupata maelezo hapa. Tunayo mikakati ya kuboresha kilimo kwa maana ya kupeleka teknolojia kwa sababu vijana hawapendi kutumia jembe la mkono.

Napenda kutumia fursa hii kusema kwamba Wizara yangu kupitia Mfuko wa Pembejeo, tunaanzisha sasa mkakati wa kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana wanaolima ili kuwapa *power tillers* kuwawezesha ya kwamba tufanye kilimo chao kiwezo kuwa rahisi kuliko hivi sasa.

Katika Mkoa wa Kigoma wamekwishaanza. Na kuna vikundi vya vijana ambao wamejiunga na kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, wanapelekwa JKT kwa miezi michache wanafundishwa maarifa ya kilimo halafu wanapewa Mikopo hii ili iweze kuwaendeleza. Tunadhani mkakati huu utaweza kutoa ajira kwa vijana wengi wanaoishi vijijini na kuwawezesha kujiendeleza zaidi kuliko hali nyingine yoyote nyingine.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu.

Na. 160

**Hesabu za Serikali za Mitaa Kuendana na Viwango vya Kimataifa**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Hesabu za Serikali Kuu zimetengenezwa kufuata viwango vya kimataifa vya mahesabu *Cash Basis IPSAS* na kwa mujibu wa *PFA 2001 Section* 25 ni jukumu la Mhasibu Mkuu wa Serikali kutengeneza hesabu hizo na kwa kuwa Serikali za Mitaa (LGA) zinapata karibu asilimia 80 -90 ya mapato kutoka Serikali Kuu (Hazina).

(a) Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hesabu za Serikali za Mitaa zinakubaliana na asilimia 100 za viwango vya kimataifa vya utunzaji wa mahesabu?

(b) Je, ni sheria gani inayowalizimu Serikali za Mitaa kutekeleza viwango vya kimataifa?

(c) Je, ni jukumu la nani kuhakikisha kwamba kuan uwiano huo wa pamoja na kutekeleza matakwa hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami, Mbunge wa Nkasi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba asilimia kubwa ya mapato ya Serikali za Mitaa hutoka Serikali Kuu. Kutokana na hali hii mhasibu Mkuu wa Serikali ana jukumu la kusimamia matumizi hayo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba hesabu za matumizi ya fedha hizo zinaandaliwa katika viwango vya kimataifa vya hesabu za Serikali *(International Public Sector Accounting Standard- IPSAS).*

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa tayari wanaandaa hesabu zao katika mfumo huu ambao unajumuisha kutambua madeni au matumizi ya wakati uliopita kwenye hesabu za wakati husika. *(The Accrual Principle).*

(b)Mheshimiwa Spika, sheria zinazolazimu Serikali za Mitaa kutekeleza viwango vya kimataifa ni zile ambazo zinatumika katika uandaaji wa hesabu za Serikali Kuu.

Hivyo kitachofanyika ni kupendekeza maboresho katika sheria ya fedha ya Srikali za Mitaa ya mwaka 1997 na kuingiza vipengele vikavyopelekea sheria hii itambue viwango hivyo kama tunavyofanya katika sheria ya fedha Na. 6 ya usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, kama ilivyorekebishwa mwaka 2004.

(c)Mheshimiwa Spika, hadi sasa hakuna chombo maalum cha fedha cha kitaifa kinachosimamia uandaaji na uhuishaji wa Hesabu za Fedha za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, isipokuwa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na Umma.

Hata hivyo ikiwa wakati utafika wa kuwa na chombo maalum kitacholeta ubora na manufaa zaidi katika taratibu zilizopo za uandaji wa hesabu za mapato na matumizi ya fedha katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, basi chombo kama hicho kitaundwa. Hivi sasa juhudi zinafanywa ni kutunga sheria mpya ya kumpa Mhasibu Mkuu wa Serikali madaraka ya kusimamia hesabu za mapato na matumizi ya fedha ya Serikali za Mitaa.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na yanayoridhisha naomba niulize kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Serikali za Mitaa wanatumia sheria ya fedha yaani *Local Authority Financial Memorandum and Accounting Manual* ya mwaka 1997 na kwa mtindo wake huo hauendani na mtindo wa *IFRS*.

Mheshimiwa Spika, ili kuwepo na uhakika na uwiano wa mahesabu haya je, Serikali itakubaliana nami kuwa marekebisho ya fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 iletwe mwaka huu?

La pili kwa kuwa mifumo yote hii miwili katika Serikali panapokuwa na mifumo miwili inatumika kwa pamoja na hii inakuwa inatoa mianya mingi na visingizio vingi vya fedha ya Serikali na fedha ya umma kutumika ovyo.

Je, mtindo kama huu utakomeshwa lini haswa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIAH S. SUMARI:** Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kujibu nimpongeze sana kwa kiwango ambacho anafuatilia jambo katika mkutano huu wa 14.

Mheshimiwa Spika, hili ni swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kuhusu jambo hili hili. Kwa hiyo. ninadhani kuna mahali panapomkera na nitamuomba aniambie tutakapomaliza haswa ni wapi panapomkera. Lakini nijibu maswali yake basi mawili kama ifuatavyo.

Kwanza ni kweli sheria inayotumika sasa hivi na Serikali za Mitaa katika kuwaandali mahesabu ya Halmashauri na wilaya zetu ya mwaka 1997 kwa kiwango fulani ina kizani na *International Financial Reports in Standards IFRS* hiyo tunakubali.

Hiyo imepelekea matumizi haya ya sheria hii yetu ya hesabu za Halmashauri na wilaya imepelekea yale mahesabu kutokuwa ya viwango vya kimataifa Serikali inaelewa jambo hili lakini sio tu jambo la viwango.

Lakini ni vilevile umuhimu wa kuwapa wahasibu wetu kwenye ngazi ya Halmashauri elimu ya kuhusu matumizi mazuri ya *IFRS* ambako ndiko tunakokwenda.

Pili kuwepo na mifumo miwili ambayo inatumika katika kuandaa hesabu hizi, tunakiri ndiyo hiyo ni moja ya matatizo tuliyonayo na ndiyo sababu tuko njia kurekebisha sheria hii ya 1997 kwanza ifanane na sheria ya fedha ya umma ya mwaka 2001 kama nilivyosema lakini vilevile ili iowane na *IFRS*.

Lakini vilevile ili basi itimize viwango vilivyowekwa vya *International Public Sector Accounting Standards* na tukifika hapo nadhani hesabu zetu zinazotengenezwa na Halmashauri pamoja na wilaya zitakuwa za viwango ambavyo vinaridhisha.

Na. 161

**Uanzishwaji wa Bima ya Mazao**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia themani (80%) ya Watanzania ni wakulima:-

Je, Serikali yetu ina mpango wa kuanzisha Bima ya Mazoa kutokana na majanga mbalimbali ya uharibifu wa mazao kama vile Mafuriko, Ukame, Moto, Wadudu na Wizi ili wakulima waweze kufidia hasara hizo kupitia mfuko wa Bima ya mazao.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Dewji, Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utaratibu wa mkulima kuwa na kinga ya bima dhidi ya uharibifu wa mazao kutokana na majanga kamavile mafuriko, ukame au wadudu waharibifu umezoeleka zaidi katika nchi zilizoendelea kiuchumi.

Katika Bara la afrika, nchi nyingi ikiwemo Tanzania zimekuwa na majaribio ya kuanziasha bima ya aina hiyo kwa lengo la kutoa kinga kwa wakulima. Kwa baadhi ya nchi ambako utaratibu huo unafanyika uzoefu umeonesha kuwa mazingira ya kibiashara ya bima hii huwa si ya kuwavutia wafanyabiashara binafsi wa bima kama ilivyo kwa bima ya moto au bima ya magari ambazo zimezoeleka.

Mheshimiwa Spika, tokea mwaka 2006, Idara ya Bima imekuwa ikifanya utafiti juu ya uanzishwaji wa Bima ya mazao kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa wakulima wa zao la mahindi na karanga katika wilaya ya Mbulu na Babati Mkoa wa Manyara. Kwa kuzingatia maelezo na mazingira yaliyotolewa ni dhahiri kwamba inahitajika kufanya utafiti wa kina kabla haijafikia uamuzi wa kuanzisha bima ya mazao pamoja na kuchagua aina ya mfumo utakaotumika katika kutekeleza utaratibu huo. Matarajio yetu ni kwamba utafiti huo ukikamilika Seriakli itashauriwa ipasavyo kuhusu aina za mfumo wa Bima utakaotumika ili kutoa kinga ya bima kwa wakulima wetu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumuulioza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mhimiwa Spika, kwa kuwa wakulima wa Mkoa wa Singida, wameamua hasa kujikita katika suala zima la kilimo. Na kwa kuwa, wakulima hawa wanakabiliwa na kero mbalimbali.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakuwa tayari kuja Singida ili aweze kuongea na wakulima hawa na kutatua kero zao?

Kwa kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba suala hili linafanyiwa utafiti na kwa kuwa najua sio rahisi kuniambia muda muafaka wa utafiti huu. Je, Mheshimiwa naibu Waziri atakuwa tayari kuongeza jitihada za utafiti huu ambao najua utazaa matunda kwa wakulima ili majibu yaweze kupatikana haraka?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge mutaona nimepitiliza kidogo muda wa maswali kwasababu tulivyoanza kulikuwa na uwasilishwaji wa Hati nyingi sana zilizochukua takribani dakika 10, kwahiyo najaribu kuzifidia hizo kwa kuendelea hivi sasa. Mheshimiwa naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, napenda kijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza mualiko wa kwenda Singida kuzungumza na wakulima nadhani nitajitahidi kwa kushirikiana na wenzangu wa Kilimo ili tuweze kufika na kuzungumza na wakulima; kuelewa matatizo yao na hususan katika hili zoezi zima la kuanzisha bima kwa ajili ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka nimjibu Mheshimiwa Diana Chilolo, ni kwamba kupitia Ofisi yangu tutajitahidi sana kuharakisha utafiti huu uweze kukamilika kwa wakati ili tuweze kupata majibu yatakayotuwezesha kuanzisha au kutokuanzisha kwa bima hii ya wakulima.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata nimeamua kwamba lijibiwe kwa maandishi kwasababu kwa maudhui yake baada ya kuliona jibu linaweka bayana suala la madeni baina ya jirani na sisi; kitu ambacho pengine kinaweza kuwa na athari katika mahusiano yetu.

Kwa hiyo nimeona ni vyema Waheshimiwa Mutayapata haya na hata itakapowafikia wenzetu wa vyombo vya habari tunatumaini kwamba watatumia hekima kwasababu ni jambo la ndani la kudaiana baina ya ubalozi wa *DRC Kigoma* na nchi yetu; kwahiyo litagawiwa kwa maandishi.

Tunaendelea Waheshimiwa, sasa ni zamu ya, nalo lilikuwa refu hilo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, swali linaulizwa na Mheshimiwa Gaudence Kayombo wa Mbinga Mashariki.

Na. 163

**Sheria ya Zao la Kahawa**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya zao la Kahawa (2001) inaitaka Bodi ya Kahawa kuangalia ubora wa zao la kahawa toka miche ya kahawa hadi hatua inapouzwa:-

(a) Je, ni kwanini hadi sasa Bodi ya Kahawa inashughulikia zao hilo wakati wa kuuza tu?

(b) Je, ni kwa nini mpaka sasa wakulima wa kahawa hawajaandikishwa?

(c) Je, ni kwanini kahawa ya Mbinga inauzwa *ex-Makambako* badala ya *ex-Mbinga.*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Spika, (a),·Bodi ya Kahawa haishughulikii zao la kahawa wakati wa kuuza tu bali inashughulikia kahawa kuanzia miche shambani, maandalizi, baadaya kuvuna na ndipo wakati wa mauzo.

Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya inatoa elimu ya kilimo bora cha kahawa kwa wakulima kupitia wakaguzi, yaani *inspectors* wake ambao wapo kila Wilaya inayolima kahawa.

·Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti, *TaCRI*, inahimiza wakulima kutumia miche ya kisasa ya kahawa. Aidha, Bodi inakusanya ushuru wa 0.75% kutoka mauzo ya minadani ambayo inapelekwa *TaCRI* kugharimia utafiti wa miche bora na usambazaji kwa wakulima.

·Kwenye ngazi ya maandalizi ya usindikaji Bodi inaidhinisha matumizi ya teknolojia mpya yoyote inapoingizwa na kukagua viwanda vya kubangulia na kukoboa kahawa kabla ya kutoa leseni kwa yeyote anayefanya kazi au shughuli hiyo.

- Kwenye usimamizi wa biashara Bodi inatoa leseni za ununuzi wa kahawa na kuvikagua vituo vyote vinavyotumika kununulia kahawa kwa kutumia wakaguzi wa Bodi ya Kahawa. Kwa kushirikiana na maafisa ugani wa Halmashauri.

- Kwenye soko Bodi inaendesha na kusimamia bei wakati wa mnada. Pamoja na minada Bodi inasimamia mauzo ya moja kwa moja nchi za nje pamoja na kutoa leseni zake.

- Bodi pia inasimamia na kudhibiti usafirishaji wa kahawa nje katika Bandari zetu za Tanga na Dar-es-Salaam ambapo inahitajika kutoa hati ya ubora na uwasili, *Certificate of Origin*, ambavyo vinahitajika kusindikiza mzigo wa kahawa nje.

Mheshimiwa Spika, Bodi inatekeleza hayo katika kutimiza majukumu yake yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Zao la Kahawa ya mwaka 2001.

(b) Mheshimiwa Spika, Ni kweli kwamba wazalishaji wote wa kahawa nchini wanatakiwa watambuliwe kwa kuwa na usajili. Hadi sasa Bodi haijatekeleza jukumu hili kutokana na ufinyu wa Bajeti kwani zoezi lenyewe linahitaji ukusanyaji wa taarifa sahihi za kila Mkulima juu ya kilimo chake na mahali alipo hii ikiwa ni pamoja na kumpatia kitambulisho cha Mkulima wa Kahawa. Yote haya yanahitaji fedha nyingi, hata hivyo Bodi imebuni utaratibu mpya utakaowezesha kuanza usajili wa wakulima wa kahawa wa mwaka 2009 kwa utaratibu wa kushirikiana na Halmashauri kwa kutumia bajeti za kilimo, yaani *DADPS.*

(c) Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi kirefu Mbinga kumekuwa na udhaifu wa Miundombinu ya kuwawezesha wasafirirsahji wa Kahawa nje kuifanya biashara hiyo kwa uhakika bila wasiwasi wa kucheleweshwa kuwahi meli Bandarini. Hii inatokana na kukosekana kwa lami kwenye kipande cha barabara kati ya Songea na Mbinga ambako miaka ya nyuma ilikuwa inashindwa kupitika wakati wa masika.

Hivyo ikaamuliwa kwamba kahawa ya Mbinga iuzwe *ex-Makambako* kwavile kuna miundombinu ambayo huwezesha biashara ya kahawa kufanyika kwa haraka na kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Miundombinu hiyo ni reli, *TAZARA*, barabara ya lami hadi Dar-es-Salaam, bandarini, maghala ya kutosha kuhifadhi kahawa safi na umeme wa uhakika.

Miundombinu hiyo inawezesha wanunuzi wa kahawa ya Mbinga kufanya biashara ya kahawa hiyo kwa uhakika. Hatahivyo kwa kuwa kwa wakati huu miundombinu hiyo inayoendelea kuboreshwa kule Mbinga mara itakapokamilika kahawa hiyo itauzwa *ex-Mbinga.* Utaratibu huu utwapunguzia wakulima mzigo wa gharama za usafirishaji na hivyo kuongeza kipato chao.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza naomba niishukuru Serikali kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa pale ambapo Mheshimiwa Waziri, alitembelea Mbinga na kuwaahidi wananchi wa Mbinga kwamba watashirikiana na Serikali kufufua Chama Kikuu Cha Wilaya, *CHAMBEFAA*,

lakini pia Serikali kwa kutimiza ahadi yake ya kulipa deni la shilingi milioni 106 na laki sita kwa wakulima ambao walikuwa wamekopwa na chama chao cha msingi. Lakini pia kwa ahadi ya sasa ya Serikali ya kufanya *registration* ya hao wakulima.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili. La kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba tatizo la kufanya hii kahawa ikauzwa *ex-Makambako* lilikuwa ni barabara. Na kwa kuwa, barabara hiyo sasa inapitika wakati wote, wa masika na wa jua kali; Mheshimiwa Waziri, sasa yuko tayari kuruhusu kahawa ya Mbinga ikauzwa *ex-Mbinga?*

Mheshimiwa Spika, la pili. Kwa kuwa, tafsiri ya *farm gate prices* kama ilivyo katika sheria imeleta shida sana kule Wilayani Mbinga. Katika miaka ya nyuma wale wakulima waliokuwa wanauza kahawa yao mnadani walikuwa wanakatwa kule mnadani na wale waliokuwa wanauza Mbinga walikuwa wanakatwa Mbinga.

Katika Msimu uliopita Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga iliamua makato hayo yote yafanyike kule mnadani Moshi; Je, Serikali sasa ipo tayari kutoa tafsiri katika hizo halmasahauri ili kuwe na mfumo mmoja unaoeleweka na watu wote kuridhika?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee shukrani alizozitoa kwa Serikali kuhusiana na ahadi tulizozitoa za kukisaidia Chama Kikuu cha Ushirika Cha Mbinga kiweze kufanya kazi. Shughuli hiyo inaendelea na tunataka kuhakikisha kwamba tunachukua hatua za haraka kukisaidia ili mfumo wa ununuzi uwe wa ushindani zaidi katika Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuruhusu hii biashara kufanyika *ex-Mbinga* na kwamba barabara inapitika; ni kweli sasa barabara inapitika lakini tungependa ipitike vizuri zaidi. Na kwasababu upo mpango wa Serikali wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami, sisi tunadhani utakapokuwa umekamilika huo biashara ile itavutia wanunuzi zaidi na kufanya Mbinga iwe kituo cha ununuzi kuliko hali ilivyo hivi sasa. Kwasababu ingawa barabara ile inapitika lakini bado sio nzuri sana, mimi nilipita hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kodi ile *ex-farm gate,* ni kweli Sheria ya Serikali za Mitaa inataka ushuru huo utozwe kwa mnunuzi palepale anaponunua, *ex-gate.* Lakini tatizo ambalo limetokea pale Mbinga ni kwamba wanunuzi wengi wanakwepa ile kodi ndio maana Halmashauri inalazimika kuwafuata Moshi kwenye mnada ambako hawawezi kukwepa. Kwahiyo hili tunashauriana na Serikali za Mitaa na Wizara ya Biashara ili tuweze kukubaliana ni mfumo gani ambao utawasaidia.

Lakini kubwa zaidi ni kuboresha zaidi mfumo wa ununuzi na kuwafanya wanunuzi wanaopewa leseni kule Mbinga wawe waaminifu na kuwafanya wajue wana wajibu wa kulipa kodi kwa ajili ya Halmashauri yao kwa maendeleo ya Wilaya na maendeleo ya zao la kahawa.

Na. 164

**Sheria ya Kudhibiti Bei ya Mafuta**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, bei ya mafuta katika soko la Dunia imekuwa ikipanda na kushuka kwa nyakati tofauti:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwa na Sheria inayodhibiti bei ya mafuta kwenye soko la ndani, sheria ambayo itawiana na mabadiliko ya bei ya mafuta katika soko la dunia, hasa pale bei ya mafuta inaposhuka kwenye soko la dunia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Bunge lako Tukufu imepitisha Sheria mpya ya Mafuta ya Mwaka 2008 mwezi Aprili, 2008. Sheria hii pamoja na mambo mengine inaipa nguvu ya kisheria Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, *EWURA*, kuingilia kati udhibiti wa bei ya bidhaa ya bei ya mafuta ya petroli pale inapoonekana hakuna ushindani wa haki katika soko la bidhaa hizo humu nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii mpya inatoa uwezo kwa *EWURA* kutangaza bei mpya kufuatana na mabadiliko ya gharama inazolipia kampuni inayoagiza mafuta na vigezo vingine husika. Kwa kiwango kikubwa gharama za kuingiza mafuta nchini zinabadilika kufuatana na bei ya mafuta katika soko la dunia pamoja na thamani ya shingi ikilinganishwa na dola ya Marekani, kwavile mafuta hununuliwa kwenye soko la dunia kwa kutumia dola za marekani. Katika kudhibiti bei ya bidhaa za mafuta *EWURA* hutumia kanuni za *EWURA* za kupanga bei ya mafuta ya petroli za mwaka 2009, *Petroleum Products Price Setting Rules*, 2009 na fomula ya kukokotoa bei ya mafuta ya petroli, *Petroleum Price Setting Template.*

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali hivi karibuni imechapisha katika gazeti la Serikali namba 5 la tarehe 9 Januari, 2009 Kanuni zinazoipa *EWURA* mamlaka ya kuingilia kati na kupanga bei ya mafuta ya petroli elekezi nay a kikomo. *EWURA* itapanga bei za mafuta ya petroli na itaingilia kati hatua hiyo endapo mojawapo ya vigezo vifuatavyo vitatokea; bei ya bidhaa za mafuta ya petroli kwa wastani zitazidi bei ya kikomo kwa 7.5% *price gauging,* itathibitika kuwa kampuni zinazofanya biashara ya mafuta zimekula njama ya kupanga bei, *Price fixing* na kunapotokea hali ya hatari, *state of emergence*. *EWURA* itaendelea kufuatilia bei za bidhaa ya mafuta na kuingilia kati pale patakapokuwa na ulazima wa kuafanya hivyo kama ambavyo imefanya kuanzia Januari 2009 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, kanuni hizo hutoa adhabu kali kwa watakaokiuka ikiwa ni pamoja na faini ya shilingi milioni tatu na kifungo cha muda usiopungua miaka mitano.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mhesimiwa Spika, nina maswali mawili. Kwa kuwa *EWURA* imekuwa imetumia kigezo cha *price gauging.* Na kwa kuwa, baadhi ya wafanyabiashara huweka bei hiyo iliyopangwa na *EWURA* kwenye mabango yao lakini wakati uleule bei wanayouza ni tofauti. Je, *EWURA* inafahamu hilo na ni hatua gani imezichukua?swali la pili. Kwa kuwa wananchi wanaposikia kwamba bei ya mafuta imeshuka wanakuwa na matumaini kwamba hata bei ya usafiri na usafirishajki nayo itakuwa nafuu. Je, huoni kwamba kuna haja *EWURA* ya kukaa na *SUMATRA* ili kuweka sawa haya mambo wakati bei ya mafuta inaposhuka na nauli nazi zinashuka? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika kwanza kabisa naomba kurejea kwamba ndani ya muda mfupi tu ujao Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atasimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu na kutoa Kauli ya Serikali itakayozungumzia hali ya biashara ya bidhaa za mafuta hivi sasa. Sasa kwa kuwa, ninafahamu kwamba masuala haya mengi ya biashara ya mafuta mengi kuna mambo mtambuka kusema kweli jambo moja linaweza kuathiri biashara ya mafuta kwa namna mbalimbali; ninaomba tufanye subira kidogo ili kwenye Kauli ya Serikali ya Mheshimiwa Waziri, maelezo ya kina zaidi yatatoka kuliko haya ninayoweza kuyatoa sasahivi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ufupi ni kama *EWURA* imeshatoa bei elekezi na kuna bei ya kikomo ya juu na bei ya chini, sasa ikiwa mfanyabisahara huyu kwenye bango lake ametoa bei ile ya *EWURA* lakini ukienda pale kwenye pampu bei anayokuuzia ni bei tofauti, hapo ni dhahiri kabisa anakuwa amekiuka taratibu na anastahili adhabu kwa mujibu wa sheria na kanuni ambazo *EWURA* wamejiwekea. Hili la pili kwamba kwa kuwa bei za mafuta zimeshuka kwa kubanwa na *EWURA* sasa *SUMATRA* na *EWURA* wakae pamoja; mimi ninalikubali na ninadhani ni wajibu wetu sisi Serikali kuwasiliana na Wizara husika inayosimamia masuala ya *SUMATRA* ili kuangalia namna ambavyo wao wanaweza kufanya kazi ya pamoja na kuhakikisha kwamba maslahi mapana yanapatikana kwa wananchi wa Tanzania.

**SPIKA:** Asante Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa sasa ni matangazo na kama kawaida tutaanza na wageni. Wapo wageni wa Waheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Salum Hamis Salum, ambao ni Waheshimiwa Madiwani idadi yao ni 22 wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu na wanaongozwa na Mheshimiwa Pius Machungwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri na Mheshimiwa Nkoba Machibya, Makamu mwenyekiti wa Halmashauri; ningeomba wasimae. Nadhani ni wale na wana mavazi rasmi kabisa ya Halmashauri ya Meatu. Karibuni sana Bungeni, tunafurahi sana tunapowaona Waheshimiwa Wenzatu, Madiwani mukija hapa kuona shughuli za Bunge. Karibuni na tunawatakia mema katika kazi zenu.

Mgeni wa Mheshimiwa Ahmedi Ali Salum, ambaye ni Katibu wake Jimbo la Solwa ni Bwana Denis Mayunga; yule pale. Asante sana karibu sana. Basi leo tumepata bahati ya kuwa na wageni kutoka mkoa mmoja tu wa Shinyanga, basi. *(Makofi).*

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, anaitisha kikao leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi namba 133; kwahiyo Kamati ya Sheria Ndogo, saa 07.00 mchana ukumbi namba 133. Mheshimiwa Wilason Massilingi, Mwenyekiti wa Katai ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo mukutane saa 6.00 mchana leo ukumbi namba 231; Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, saa 6.00 mchana ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Abdisalam Issa Khatib, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara mukutane leo saa 5.00 asubuhi ukumbi namba 227.

Huo ndio mwisho wa matangazo ya kawaida na sasa yapo matangazo ambayo ni yangu mwenyewe, Spika. Naomba nitoe taarifa kuhusu hoja binafsi na huu ni utaratibu naomba muuzowee tu, siku za zamani hoja binafsi zilikuwa zinakufa kifo cha sirisiri, hujui ni nini kimetokea.

Kuanzia sasa tutakuwa tunatoa taarifa ni nini kimetokea. Kulikwa na hoja binafsi ya Mheshimiwa Halima James Mdee, kuhusu mgogoro wa ardhi eneo la Boko-Chasimba. Hoja hiyo iliondolewa kwenye Kamati baada ya kupata uhakika, Spika amepata uhakika kwamba suala hili liko Mahakamani na hususan lipo Mahakama ya Rufaa.

Pili ni hoja ya Mheshimiwa Wilson Massilingi, hukusu uwajibikaji kwenye tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Halmashauri zetu zile. Mheshimiwa Massilingi baada ya mashauriano aliona muda wake sio muafaka kwahiyo aliiondoa kwa kuniandikia dokezo. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, alileta hoja ya kufanya mabadiliko katika Vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa kifupi alivyokuwa anataka yeye ni kwamba ukubwa wa Serikali yaani idadi ya Wizara, huo ukubwa wa serikali uwekewe ukomo ndani ya Katiba. Baada ya kupeleka kwenye Kamati na Kuzingatia ushauri wa Kamati, nimeridhika kwamba hoja ya Mheshimiwa Hamad inaingiliana na mchakato wa kurekebisha Katiba chini ya Ibara ya 98 ya Katiba ambayo inaelekeza, marekebisho ya Katiba ya Nchi yafanyike kwa Muswada Maalum sio kwa ombi tu la Mbunge kuleta na hili muzingatie.

Sasa atakayeleta dokezo tu tubadili Katiba nitamkatalia palepale kwasababu Ibara ya 98 sasa iko wazi na Kamati imeshanishauri jambo hili likae hivyo sasa. Na isitoshe jambo kubwa kama hili linahitaji utafiti zaidi kwahiyo nimeizuwiya hiyo hoja ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ya mabadiliko ya Katiba haiwezi kuja.

Na ya mwisho ni hoja ya Mheshimiwa Dokta Wilbroad Slaa, kuhusu dhana ya hisia zake kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani aliingilia mchakato wa

Zabuni ya Vitambulisho Vya Taifa. Kamati imenishauri na nimekubali kwamba ni busara ili mradi huu usiendelee kuchelewa kwa kupuigwa mikwara ya kila namna basi mchakato wa Zabuni ya Vitambulisho vya Taifa uendelee hadi mwisho, suala hili tuko nyuma sana na ni lazima likamilike. Baada ya kukamilika kama Kamati itapenda kuendelea na kazi ya kuangalia ni nani alikosea na hivi, bado Bunge lipo tunaweza kuzingatia kwa wakati huo. Hii ndio taarifa ya Spika, kuhusu Hoja Binafsi zote zilizoletwa mbele yangu. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wabunge, nizungumzie haya yanayotukabili hivi punde, nayo ni Taarifa za Serikali, hatuna tatizo na Kauli za Serikali, lakini kuna Taarifa za ambazo zimewasilishwa chini ya Kanuni ya 37, ambayo ni kuwasilisha kwa hati. Na Kanuni ya 37 kwa taarifa yenu tu kwa rejea, Hati inaweza kuwasilishwa Bungeni wakati wa Vikao vya Bunge na (a) Waziri au (b) Kamati yoyote ya Bunge, hayo ndio yametokea kabla ya kipindi cha maswali.

Mawaziri wamewasilisha Hati na Wenyeviti wa Kamati husika wamewasilisha hati. Sasa utaratibu huu unazingatia Mamlaka muliyonipa ya kuamua namna bora ya uendeshaji wa suala lolote ambalo liko mbele ya Bunge. Tungeweza zote zikawa Kauli tu na kwahiyo hazina mjadala kabisa. Tungeweza tukazigeuza zikawa taarifa ambazo zinataka hoja iamuliwe, hilo nalo lingewezekana. Lakini baada ya kutazama maudhui yaliyomo katika Hati za Waheshimiwa Mawaziri na pia kwasababu nilipeleka hati hizo zijadiliwe na Kamati na nimeshauriwa ipasavyo nimeona utaratibu tutakaoufuata sasa ni kwamba Waziri muhusika atawasilisha hoja yake kwa maelezo na baada ya hapo wale wenzetu ambao ni Kamati waliozipitia hoja hizi nao sasa watatoa maoni kwa maelezo mbele hapa.

Kwa maana hiyo basi chini ya Kanuni ya 37 (9) noisome, “*Mjadala unaweza kuzingatia kila jambo lililomo katika Hati, isipokuwa kama Spika kwa kuzingatia uendeshaji bora wa shughuli za Bunge ataamua vinginevyo.*” Nimeziangalia hizi taarifa, nimeona ni kama kile wanachoita Waingereza, *Work in progress.* Na kwahiyo ni kupoteza muda tu kusema tuzijadili sasa kwasababu hazijafika kwenye ile hatima yake. Kwa maana hiyo tuyachukue kwamba maelezo ya Wenyeviti wa Kamati yanatuwakilisha sisi, sasa hiyo haizuwii wakati mwingine kwenye mkutano ujao wowote, uwe wa 15, wa 16, Mbunge kuleta hoja sasa ili tuzame zaidi katika moja au zaidi ya taarifa zilizopo. Kwahiyo Mawaziri watawasilisha, Wenyeviti wa Kamati au Wawakilishi wa Wenyeviti watatoa maoni ya Kamati na hapo tutatulia. Tutakuwa tumetimiza wajibu wetu kwa hatua hii tuliyofikia. *(Makofi).*

Taarifa moja inayohusu Mgodi wa Kiwira. Waheshimiwa Wabunge, mutakumbuka katika Mkutano wetu wa 12 wa Bajeti tarehe 09 Julai, 2007 wakati Waziri wa Nishati na Madini alipowasilisha makadirio yake. Waziri alipokuwa anajibu hoja za waheshimiwa Wabunge aliahidi kwa maneno yafutayo na ninayanukuu kutoka *Hansard.*

Waziri alisema, ninanukuu, “*kwa kuzingatia mambo yalivyokuwa mengi tulidhani busara zetu zilituongoza kwamba haitakuwa sawa kulichangia jambo hili na mambo mengine ambayo tunayaongelea hapa kwenye Bajeti kwa ujumla; tunaahidi kulisemea*

*kwa kulitolea kauli ndani ya Mkutano wa Bunge unaoendelea na tutawasiliana na wewe,"* nadhani ni Spika, *"tulilete hapa kwa muda muafaka,"* hilo jambo la Kiwira.

Sasa imepita muda na ilikuwa leo tuweze kupokea taarifa lakini nimepokea sasa taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini yenye kurasa kubwa hivi kumbe wenzetu hawa katika shughuli zao za kawaida za kutembelea maeneo ya sekta yao walikwenda hadi kiwira na wameandika taarifa ambayo nayo inazua masuala ambayo Serikali itahitaji muda ili kuweza kuyajibu. Kwa hiyo nimeahirisha hilo na leo nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu mgodi wa Kiwira ili katika wakati muafaka tuweze kupata maelezo.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo maelezo kuhusu hoja binafsi na taarifa za leo. Ninazo taarifa za ziada au kukumbusha tu, Mheshimiwa Dr. Slaa ameendelea kuniandikia kuhusu maelekezo yangu kwamba athibitishe kwamba kuna vijana waliofeli kidato cha sita ambao wanapewa leseni ya ualimu.

Mimi nadhani Mheshimiwa Dr. Slaa asiendelee tu kutoa tafsiri tulitumia neno labda, tulifanya hivi kwa mujibu wa kanuni zetu uamuzi ni wa Spika, siongozwi na tafsiri ya Mbunge, uamuzi ni wangu mimi. Itakuwa fujo kama Mbunge atang'ang'ani anachosema yeye ndivyo kiwe. Kwa mujibu wa kanuni zetu kama ruling ya Spika hukubaliani nayo wewe Mbunge basi unakata rufaa kwenye Kamati ya Kanuni na Spika anajitoa ili Naibu Spika aendeshe kikao cha kuangalia hilo.

Sasa hilo halijafanyika kwa hiyo bado ninadai mimi nimesikia na nimeelewa hivyo nimechukua hansard kweli kuna maneno pale yanaashiria kwamba hata kama si moja kwa moja ulikusudia kusema kuna wanaofeli kidato cha sita na bado wanapewa leseni za kufundisha. Sasa narudia kuelekeza kwamba hilo lifikishwe basi kwa Wizara husika ili Serikali iweze kuchukua hatua pengine kumetokea udanganyifu ili tuweze kulimaliza hili. Ningeomba Mheshimiwa Dr. usiliendeleze kwa njia yoyote nyingine. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge nimearifiwa na Katibu naona hili ni jambo nzuri nilitolee taarifa kwamba shirika letu la *LPF* baada ya kuwa mgogoro wa jengo letu lile karibu ya geti pale ule mgogoro kwisha, kuna makubaliano ya awali na *LPF* na limepimwa kiuhadisi kwamba jengo lile linaweza kuhimiri gorofa nyingine tatno. Kwa kuzingatia hilo tunaendelea na mchakato na Serikali ili ikiwezekana jengo lile sasa pamoja na kuweka vitu kama *gym* liweze kutumika kama ofisi za Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Kwa hiyo, natoa taarifa hiyo ya awali ili kuendelea kupata baraka zenu kwa harakati hizi za kuimarisha ofisi za Wabunge. *(Makofi)*

Mwisho nina ujumbe tu kwa magazeti fulani fulani Waheshimiwa Wabunge si mmeona kumezuka katika miaka miwili hii au kuchipua lakini kinachochipua ni chenye neema labda tuseme basi yamejitokeza magazeti ni aina yakitoto kabisa magazeti haya inaelekea watu fulani wenye fedha wameamua kama kupashana habari hivi kutukanana.

Kwa hiyo utaona yana mambo madogo madogo yasiyo na maana ni upotoshaji mtupu yamekuwa mengi tu na mfano mmoja ni jana gazeti linazungumzia mambo machafu machafu lakini limeweka ukurasa mzima picha ya Bunge, tunapeleka ishara gani wa wananchi na hata nje ya nchi yetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo mimi naomba sana Serikali mimi sidhani kama Sheria ya Magazeti haiwezi kutumika kushughulika na vitu hivi na nasema hivi kwa sababu sura nchi sasa inachafuka mtu anapokuja kutoka nchi jirani mathalani wanaojua kiswahili anakuta gazeti linazungumza mambo kama hayo tunayoyaona. Anatutazamaje Watanzania sasa, tunaonekana wote ni watu wa ajabu kwa sababu gazeti ni kitu cha kuelimisha, kuburudisha na kuweza kutoa ukweli.

Mimi nasema magazeti au utitiri wa magazeti ambayo hayana maana yoyote hayana matangazo sijui yanalipwaje, ndiyo maana nasema ni watu wenye fedha fedha wanaamua tu kutukana wenzao na kutupiana matope na hivi.

Sasa mchezo huu unaathari kwa nchi kwa sababu kinachochafuka ni Tanzania sio mtu mmoja mmoja, kwa hiyo kama kawaida yangu mimi ufyatuka tu nikasema lakini ndivyo nilivyo sasa kwa hiyo na mara nyingine ni vizuri kuwa na watu wa namna hii ambao wanaiona jamii wanasema mambo. (*Makofi*)

Baada ya maneno hayo Waheshimiwa sasa namuita Katibu tuingie katika hatua nyingine.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Taarifa ya Serikali Kuhusu Tatizo la Nishati ya Mafuta Nchini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na kama tulivyowasilisha mezani kwako asubuhi hii leo, naomba kutoa taarifa ya Seriakali kuwa Bunge lako Tukufu kuhusu biashara ya mafuta ya petroli nchini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kulishukuru Bunge lako tukufu kwa kunipa fursa hii ya kutoa taarifa hii kuhusu hali ya biashara ya mafuta ya petrol hapa nchini. Kamat tunavyofahamu mafuta ya *petrol* ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu kwani viwanda vyombo vya usafiri na huduma nyingine hutegemea mafuta na bidhaa zake. Bei ya mafuta inapopanda bei zingine nyingine hupanda pia. Kwa mfano bei za usafiri bei za vyakula bei za bidhaa za viwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania bado haijagundua mafuta ya petrol, na hivyo bidhaa hizo huagizwa kutoka nje ya nchi. Fedha nyingi hutumika katika kuagiza bidhaa hiyo kwa mfano kuanzia Januari, 2008 hadi Septemba, 2008 Tanzania ilitumia Dola za Kimarekani bilioni 1.75. Kiasi hiki kingelikuwa kikubwa zaidi kama tusingebahatika

kugundua gesi asilia ambayo inatumika kama *fuel* mbadala wa kuzalisha umeme na kwa matumizi katika viwanda takribani 21 jiji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008, gesi asilia iliyotumika kwenye kuzalisha umeme na viwandani ni kiasi cha futi za ujazo kama bilioni 23.5 iliyookoa kiasi cha dola za Marekani milioni 550 ambazo zingetumika kuagiza mafuta. Biashara ya mafuta ya petroli vile vile inachangia kwa kiasi kikubwa kwenye kodi ya Serikali. Aidha, bidhaa za petrol zinachafua mazingira na ni hatari kwa maisha ya viumbe hai na watu kama ilivyotokea hivi karibuni nchini Kenya jambo ambalo linasikitisha sana, ambapo watu takribani wapatoa 127 walipoteza maisha baada ya mlipuko wa gari la mafuta lililopata ajali. Kwa kuzingatia unyeti wa bidhaa hii ubora na uendeshaji wa biashara ya mafuta imewekwa chini ya udhibiti wa *EWURA.*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini, ili kuelewa biashara ya mafuta ya petroli inavyoendeshwa nchini ni vizuri kufafanua mfumo wa uagizaji na usambazi wa bidhaa hiyo.

Mfumo wa uagizaji ndiyo uti wa mgogo wa biashara ii ya mafuta hasa katika kuhakikisha kuwa mafuta yanapatikana sehemu zote za nchi kwa wakati wote na kwa bei stahiki. Mfumo uliopo hivi sasa umeweza pamoja na kuhitaji ufanisi katika maeneo mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hii katika maeneo yote nchi na kwa wakati, tangu kuruhisiwa kwa biashara ya soko uria hadi sasa nchi haijakubwa na upungufu wa bidhaa hii wala kushuhudia misururu mirefu kwenye vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, uagizaji wa mafuta, inakisiwa kuwa mahitaji ya mafuta ya petroli nchini takribani tani milioni 1.7 mwaka, mafuta mengi yanayoingizwa hapa nchini uagizwa kutoka nchi za Mashariki ya Kati yaani *Arabian Gulf*. Kwa mwaka 2008, makampuni 24 ndiyo yaliyohusika moja kwa moja na uagizaji wa mafuta hapa nchini. Makampuni hayo yanaagiza mafuta yaliyosafishwa kulingana na ukubwa wa soko wanalomiliki yaani *market share*. Utaratibu huu wa makampuni mengi kuagiza mafuta kila moja kwa wakati wake, unachangia msongamano wa meli bandarini, hivyo kuongeza gharama za malipo za ucheleweshaji yaani *demurrages charges*.

Mheshimiwa Spika, sheria mpya ya kusimamia biashara mpya ya petroli yaani *petroleum supply act* ya mwaka 2008 inatambua uagizaji wa mafuta ya petroli kwa njia ya pamoja yaani *bulk procurement* ili kuleta ufanisi katika uagizaji wa mafuta, *EWURA* imemuajiri mtaalam wa kutayarisha kanuni na taratibu za *bulk procurement* kampuni inayoitwa *petroleum development cooperation* ya Uingereza iliyopatikana kwa njia ya zabuni.

Mshauri huyo anategemewa kutayarisha makabrasha ya zabuni pamoja na kusimamia angalau uagizaji wa pamoja wa shehena za awali kwa lengo la kuipa uzoefu taasisi itakayochaguliwa kusimamia zoezi hili.

Mpango huu unatarajiwa kuleta ufanisi katika ushindani, kupungua kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa kwa kuwa shehena itakuwa kubwa pamoja na kupungua kwa

gharama za usafirishaji wa bidhaa kwa kuwa shehena itakuwa kubwa pamoja na kupungua kwa gharama za *demurrage charges*. Utaratibu huu pia utarahisisha usimamizi wa ubora wa bidhaa na utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za mahitaji ya nchi na pia utaziba mianya ya ukopweji kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombuni ya mafuta, zaidi ya asilimia 90 ya mafuta ya petrol yanayotumika nchini huingizwa kupitia bandari ya Dar es Salaam na yanapakuliwa kupitia Kurasini yaani Kurasini *Oil Jetty*, ambayo ni maarufu kama *KOJ*. Kiasi kinachobakia kinaingizwa nchini kupitia bandari za Tanga, Ziwa Victoria na kwa kutumia barabara kupitia Sirari mkoani Mara.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu ya kupakulia mafuta kwenye bandari ya Mtwara ni suala muhimu kiuwekezaji na kiuchumi. Hivyo ili kuboresha huduma za mikoa ya Kusini Serikali inafanya jitihada za kuvutia wawekezaji katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gati la kupakulia mafuta gafi, single buyor morering limechakaa na kuhitaji ukarabati mkubwa, kwa sasa gati hili linatumika kupakulia mafuta ya Zambia.

Hata hivyo mamlaka ya Bandari yaani *TPA*, ina mpango wa kujenga gati jipya lenye uwezo wa kufunga meli kubwa zenye ujazo wa zaidi ya laki moja. *Gati* ya sasa inatumika kwa kupakulia mafuta gafi tu, ikilinganishwa nah ii mpya ambayo itatumika kupakulia mafuta aina yote yaani *multi-product SBM* gafi na yaliyosafishwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna makampuni kumi yenye matenki ya kuhifadhia mafuta yaani storage deports yenye ujazo wa tani 394,553 pia yako maghala manne ambayo yanamilikiwa na kampuni za *BGP Camel Oil* na *Word Oil* yawepo katika hatua za mwisho za ujenzi jijini Dar es Salaam.

Hifadhi za mafuta nje ya Dar es Salaam zinauwezo wa kuweka tani 93,393 kwa wakati mmoja. *TIPPER* inakarabati hifadhi yake ya mafuta. Ukarabati unategemea kukamilika ifikapo April mwaka huu 2009 ambapo uwezo wa kuhifadhi mafuta utaongezeka kutoka tani 102,846 hadi tani 150,000.

Ujenzi wa maghala mapya na ukarabati wa *TIPPER* utakapokamilika, nchi itakuwa na hifadhi ya mafuta ujazo wa tani 545,533 mahitaji ya nchi kwa mwezi yanakisiwa kuwa kiasi cha ujazo 150,000. Kwa hiyo hifadhi hiyo inaweza kutosheleza mahitaji ya nchi kwa zaidi ya siku 90.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hivi karibuni Baraza la Mawaziri lililofanya mkutano wake hapa jijini Dodoma tarehe 9 Februari, limeridhia *TIPPER* kuwa mwendeshaji wa ghala la forodha, yaani *TIPPER uel Bonded WareHouse*, kwa lengo la kuwa hifadhi ya mafuta, kudhibiti mapato ya Serikali pamoja na kuongeza ufanisi wa soko la bidhaa za mafuta kwa kupunguza gharama za uendeshaji

na hivyo kushusha bei kwa watumiaji. TRA inatasimamia uingizaji na utoaji wa mafuta pamoja na ukusanyaji wa kodi.

Hatua hii itapunguza uwezekano wa upungufu wa ghafula kwani wa mafuta kwani, makampuni yataweza kuhifadhi mafuta kabla ya kuyalipia kodi. Kodi italipwa wakati mafuta hayo yatakapotoka nje ya *bonded warehouse* kwa matumizi ya hapa nchini. Kwa kuweka mafuta kwenye hifadhi hiyo dharura itakapotokea mafuta hayo yataweza kuazimwa na hivyo hii inaweza kutumika kama *fuel strategic reserves.*

Mheshimiwa Spika, takwimu za *EWURA* zinaonyesha kuwa kuna vituo vya mafuta yaani *retail* au *outlets* zaidi ya 900 hapa nchini, vituo hivyo vinamilikiwa na aidha makampuni ya mafuta au watu binafsi. Matatizo ya ujenzi holela wa vituo na viwango vya ujenzi yanashughulikiwa na *EWURA* kwa kushirikiana na wadau wengine hususan Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Baraza la Mazingira la Taifa yaani *NEMC* Halmashauri za Jiji na Manispaa.

Pia shirika la viwango la taifa *TBS* na *EWURA* wako katika hatua za mwisho za mchakato wa kuweka viwango vya vituo vya mafuta yaani *petrol stations* na magari ya kuhifadhia mafuta ya petroli yaani *depots*. Hivi karibuni *EWURA* wakala wa vipimo *weights and measures agency* na *TBS* waliendesha zoezi la kukagua mita za kupima mafuta kwenye vituo vya kuuzia mafuta. Zoezi hili lililoanzia Dar es Salaam na limeendelea kufanyika nchi nzima kwa madhumuni ya kuhakikisha upimaji sahihi na kudhibiti kupunjwa kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa usambazaji wa mafuta kutoka kwenye maghala ya kuhifadhi kwenda kwenye vituo ufanyike kwa kutumia malori. Hii imetokana na kudorora kwa usafiri wa reli na kutokuwa na mfumo wa bomba yaani *pipe line*, yaani kimsingi vina gharama nafuu ikilinganishwa na usafiri wa barabara. Aidha, viwango vya magari vya kubebea mafuta ya petroli pia vinatayarishwa na *EWURA* kwa kushirikiana na *TBS.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa bidhaa za petroli, ilikuhakikisha kuwa ubora wa bidhaa za petroli unaendana na viwango vya kimataifa vilivyopitishwa na shirika la viwango la Taifa yaani *TBS EWURA* inaendesha ukaguzi wa kushtukiza kama nilivyosema hapo awali na kuchukua sampuli za mafuta kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta. Matenki ya magari ya usafirishaji mafuta na kwenye vituo vya kuuzia mafuta. Kampeni za kupambana na uchakachuaji zimefanywa kuanzia mwezi Mei, mwaka 2007 hadi sasa ambapo *EWURA* ilichukua sampuli 370 za mafuta kutoka vituo 200 vya kuuzia mafuta.

Chanzo kikuu cha uchakachwaji wa mafuta ni tamaa ya mafuta isiyo halali inayotokana na kuuza mchanganyiko wa deseli na Chanzo kikuu cha uchakachwaji wa mafuta ni tamaa ya mafuta isiyo halali inayotokana na kuuza mchanganyiko wa deseli ya mafuta taa kama mafuta halisi ya diseli. Kodi ndogo inayotozwa kwenye mafuta ya taa ndiyo hamasa ya uchakachuaji na kuuza mchanganyiko maalum kwa bei ya mafuta ya *diesel*. Kitendo hiki huleta faida ya wastani kwa shilingi 500 kwa lita. Mojawapo ya

suluhisho la swali hili ni kuianisha kodi za Serikali katika bidhaa za mafuta na kuondoa tofauti kubwa iliyopo kwenye mafuta kwenye ya diesel na mafuta ya taa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuweka viwango vya juu zaidi vya faini kwa wanaobainika kuchakachua mafuta. Jitihada za kutoa elimu kwa umma kuweka viwango na masharti ya ujenzi wa vituo vya mafuta yanayozingatiwa zitasaidia kwa kiwango kikubwa. Sheria imeainisha viwango vya adhabu kwa wanaopatikana kwa mara ya kwanza wenye mafuta machafu ikiwemo kuwafungia kituo yasafishe na kulipa mafuta faini ya shilingi milioni tatu.

Wanaopatikana kwa mara ya pili wanalipa faini ya shilingi milioni tano na kufungiwa kitu kwa miezi 12. Mara ya tatu hunyang'anywa leseni moja kwa moja. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 wafanyabiashara 108 wametozwa faini vituo 70 vimefungiwa kwa muda mfupi kabla hawajatimiza masharti na vituo 6 vimefungiwa kwa miezi 12 kutokana na kosa la pili la uchakachuaji. Vile vile depot 6 zilifungwa kwa muda na kutozwa faini. Sheria mpya ya petroli ya mwaka 2008 imeongeza adhabu hiyo kwa kosa la kuchakachua na kutokuwa na vifaa vya usalama kwenye sehemu za biashara na kuuza bidhaa za petrol bila kibali kwa shilingi milioni 10 au kifungo cha miaka 5 au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kutokana na jitihada za *EWURA* na Serikali kudhibiti kero hii kiwango cha uchakachuaji wa mafuta kimeshuka, kutoka asilimia 70 kwa wastani mwanzoni mwa mwaka 2007 hadi asilimia mwishoni mwa mwaka wa 2008 na mapambano bado yanaendelea. (*Makofi*)

*EWURA* inabuni mbinu za kisasa na kuongeza ujuzi na teknolojia ya kisasa katika kupambana na vitendo vya uchakachuaji mafuta vinavyotia hasara Serikali, kuibia watu fedha na kuharibu mali yao. Wigo wa ukaguzi ssa umepanuliwa ili kuhusisha magari yanayosafirisha petroli. Vilevile ukaguzi wa mafuta ya kulainisha yaani (*engine oil*) unazidi kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa mafuta mwishoni mwa Desemba, 2008 na mwanzoni mwa 2009, mwishoni mwa mwezi Desemba, 2008 na mwanzoni mwa mwezi Januari 2009, hususan wakati wa Sikukuu ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwenye baadhi ya maeneo nchini, kulitokea uhaba wa mafuta aina ya petroli.

Upungufu huu uliojionyesha zaidi katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam, ulisababishwa na mambo kadhaa yaliyojitokeza kwa wakati mmoja upungufu huo ulitokana na sababu zifuatazo kwa muhtasari.

(a) Kasi ya kupungua kwa bei ya mafuta iliyosababishwa na kuporomoka kwa uchumi duniani. Wakati bei ya mafuta inapokuwa imetulia, mafuta yanaweza kuhifadhiwa kwa kiasi kikubwa na kuweza kuuzwa kwa bei inayoingiza faida.

Wakati bei inapopungua haraka thamani ya mafuta yaliyohifadhiwa hushuka haraka na hivyo wafanyabiashara wanaepuka kuhifadhi mafuta kwa muda mrefu. Wale

watakaokuwa na bidhaa kwenye hifadhi inabidi wapunguze bei ili washindane na wafanyabiashara walioleta mafuta yabei ya chini hivyo kuuza kwa hasara.

(b) Mafuta ya aina ya petroli tu ndiyo yaliyokosekana. Takwimu za matumizi ya aina mbalimbali za bidhaa ya mafuta zinaonesha kuwa Tanzania inatumia zaidi ya mara tatu mafuta ya aina ya dizeli kuliko ya aina ya petroli. Dizeli inatumika kuendesha mitambo mikubwa kwenye migodi magari makubwa ya usafiri na pia inatimika viwandani. Petroli hutumika zaidi mijini na kwenye magari madogo.

Kwa hiyo waagizaji wengi huleta dizeli zaidi kuliko petroli. Katika kipindi hiki ambacho kiasi cha shehena za mafuta mbalimbali zilizoingia nchini zimepungua, uleta na uhifadhi wa mafuta ya petroli umeonesha kupungua zaidi.

(c) Pia wasiwasi waliokuwa nao wafanyabiashara wakati wa mchakato wa EWURA wa kuanza kupanga bei ulichangia katika kuhifadhi kiasi kidogo cha mafuta.

(d) Uagizaji mdogo wa mafuta kuliko kawaida kulikojionyesha katika mwezi wa Desemba. Takwimu zilizopatikana zinaonyesha kuwa kati ya tarehe 5 Desemba, 2008 hadi tarehe 27 Desemba, 2008 hapakuwa na meli iliyoleta mafuta aina ya petroli. Kwa hiyo mafuta yaliyokuwa kwenye hifadhi yalipungua kwa kiasi kikubwa. Hii hali ilisababishwa na hali iliyoelezwa hapo juu na ilipelekea kukosekana ka mafuta ya petroli katika baadhi ya vituo.

(e) Tatizo la uhaba wa mafuta pia lilitokea katika nchi za jirani za Kenya na Uganda aidha, nchi za Rwanda na Burundi ambazo zinategemea bandari za Dar es Salaam na Mombasa kuingiza bidhaa zao za mafuta nazo pia zilikubwa na tatizo hilo. Taarifa kutoka kwa waagizaji wa mafuta na wenye meli za kusafirisha mafuta zinaeleza kuwa hali hii ilitokana na uharamia wa kuteka meli zinazopita Pwani ya Afrika Mashariki na hasa maeneo ya Somalia. Hili limesababisha meli kuhitaji kusindikizwa na meli za ulinzi na kusababisha kuchelewesha kwa safari zilizopangwa hali hii inafanya meli zifike bandari kwa pamoja na hivyo kusababisha msongamano wa meli katika bandari hizi kwani zinasafiri kwa pamoja na hivyo kusababisha msongamano wa meli katika bandari hizi kwani zinasafiri kwa pamoja kwa ajili ya kupata ulinzi.

Msongamano huu huchelewesha upakuaji na kuzidi kuleta upungufu wa bidhaa. Kwa mfano, mnamo mwezi wa Januari, 2009 wakati kulikuwa na meli nne za bidhaa ya mafuta ya petroli zilizokuwa zinasubiri bandari Dar es Salaam, kupakuliwa kulijitokeza upungufu wa mafuta ya petroli jijini.

(f) Sababu kubwa zaidi kuliko zote iliyokuza tatizo la upungufu wa mafuta ni hofu ya watumiaji wa mafuta baada ya wananchi kupata taarifa za uwezekano wa kuwepo kwa upungufu wa mafuta nchini. Hofu ndiyo ilisababisha wananchi wanunue mafuta kwa wingi isivyo kawaida na hivyo kuongeza kasi ya kupungua akiba ya mafuta iliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na *EWURA* na wadau wengine kama mamlaka ya bandari *TPA,* mamlaka ya mapato *TRA,* makampuni ya mafuta walihakikisha mafuta yaliyokuwa kwenye meli bandarini yanapakuliwa na kusambazwa haraka ili kudhibiti hali ya upungufu uliokuwepo.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na kujizatiti kwa wadau husika, hali ya mafuta ya petroli kwa sasa hivi na siku zijazo itakuwa nzuri nay a uhakika. Kufikia tarehe 6 Februari, 2009, akiba ya m afuta iliyokuwepo hapa nchini kwa aina zote za mafuta ni kiasi cha lita milioni 132.

Mafuta haya yatakidhi matumizi ya nchi kwa kati ya siku 10 mpaka 41 kulingana na aina ya mafuta kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mtapata taarifa hii na mtaona kuna jedwali ambalo limeainisha kila aina ya mafuta na muda ambao inategemewa kuwepo. Jedwali lililoambatanishwa linaonyesha viwango vya mafuta na muda wake wa siku za matumizi.

Mheshimiwa Spika, lakini aidha napenda kusema kuna meli ambazo tayari ziko bandarini zikisubiri zaidi ya hizi lita milioni 132 tayari ziko bandari kuna meli ambazo ziko tayari bandari zikisubiri kuegeshwa katika gati ya *KOJ* kwa ajilli ya kupakua. Meli hizi ni pamoja na meli hizi ni pamoja na meli ya kampuni ya *BP* inayoitwa *Histria Ivory* a*nd Hellas Symphony* na ya *Engeni St. Johannis* meli hizi zina jumla ya petroli lita milioni 10.9, mafuta ya taa pamoja na ya ndege lita milioni 10.1 na dizeli lita milioni 14.16. Kwa kiasi cha mafuta yaliyopo kwenye ghala za kampuni na mafuta yanayotegemewa hususan yaliyo tayari hapa bandarini hatutegemei kuwepo upungufu wa mafuta ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi ya Februari na Machi, makampuniya *Oryx, Oilcom, Engen, BP, Total, Gapco* na *Gapoil* na *Chevron* yanatarajia kuagiza lita milioni 162 za mafuta aina mbalimbali. Kati ya mafuta hayo dizeli ni lita milioni 78, petroli lita milioni 47, mafuta ya taa lita milioni 19 na mafuta ya ndege lita milioni 26.

Kiwango hiki kitaongezeka baada ya makampuni mengine kuwasilisha tawkimu zao za matarajio ya uagizaji, tunasema hili kwa sababu ni utaratibu wa kawaida makampuni kuendelea kuwasilisha taarifa zake *EWURA.*

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu hatua za kuhakikisha kuna mafuta ya kutosha nchini, hatua za muda mfupi, ili kuhakikisha kuwa nchini inaendelea kupata mafuta ya kutosha muda wowote na kwa bei stahili, hatua zifuatazo zinaendelea kutekelezwa katika muda katika muda mfupi.

(a) *EWURA* itaendela kusimamia uwekaji wa takwimu za hifadhi ya mafuta nchini, yaani *petroleum products stock position* kwa kushirikiana na makampuni ya mafuta ili kujua hali halisi ya utoshelezaji wa akiba iliyopo nchini kwa wakati wote.

Hii itawezesha *EWURA* kutoa tahadhari kwa Wizara ya Nishati na Madini kwa makampuni wakati hifadhi ya mafuta itakapopungua na kuwa chini ya makadirio ya wiki tatu ya matumizi ya mafuta yaliyoko nchini.

(b) Makampuni yanatakiwa kuwasilisha kwa EWURA mipango thabiti kwa vipindi vya mwezi mmoja matarajio ya miezi mitatu na mpango wa mwaka wa uagizaji mafuta.

(c) Kuyataka makampuni yanayoagiza mafuta k wa kusimamiwa na mamlaka ya bandari kuwa na mpangilio ambao utahakikisha kuwa hakuna mlundikano wa meli bandarini. *TPA* pia imeombwa wakati wote kutoa kipaumbele kwenye gati kwa meli za mafuta kupakua shehena za mafuta. Hii pia itapunguza gharama za *demurrage* kwenye bei za mafuta.

Mheshimiwa Spika, hatua za muda wa kati na mrefu, mikakati ya muda wa kati na mrefu ya kuhakikisha kuwa nchi inaendelea kuwa na akiba ya mafuta ya kutosha muda wote na kwa muda bei stahili ni pamoja na:-

(a) Serikali kupitia mamlaka ya udhibiti wa Nishati na Maji *EWURA* inaandaa utaratibu wa uagizaji wa mafuta kwa wingi na kwa pamoja na kwa mahitaji ya nchi nzima. Mfumo huu wa uagizaji wa mafuta utatumia zabuni za kimataifa ambapo waagizaji watashindana ili kupata bei nafuu kadri inavyowezekana. Sambamba na bei nafuuu katika ununuzi, gharama za usafirishaji zinatarajiwa kupungua.

Tarehe 26 Januari, 2009, *EWURA* ilikamilisha mchakato wa kumpata mtaalam mshauri yaani *consultant* kama ambavyo nimemtaja hapo awali ambaye atasaidia kuandaa mfumo huo na *bid documents*, pamoja na taratibu zinazohusika ikiwemo kuandaa rasimu za kanuni za uendeshaji wa mfumo huo.

Kampuni iliyoshinda zabuni hiyo inaitwa *petroleum development consultant* ya Uingereza. Hatua inayofuata ni kuingia mkataba wa kazi hiyo na kuanza kazi rasmi. Mtaalam mshauri aliyechaguliwa anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo katika kipindi cha miezi minne kuanzia sasa na mfumo huu unatarajiwa kuanza kutumika Julai, 2009.

(b) Kuwa na mfumo wa kuweka mafuta ya akiba hapa nchini yaani *fuel strategic reserves*. Mfumo huu umeanishwa katika kifungu cha 30 cha sheria ya petroli ya mwaka 2008. Chini ya kifungu hiki, Shirika letu la maendeleo ya petroli Tanzania *TPDC* imepewa jukumu la kuanzisha na kusimamia akiba ya mafuta ya dharura hapa nchini.

Serikali inaangalia namna ya kuiwezesha *TPDC* kuanza utaratibu huu sambamba na matakwa ya Sheria husika. Kuchelewa kuanzishwa kwa *strategic reserves* kumetokana na masuala ya Bajeti.

(c) Kuwa na vyanzo mbadalai vya nishati kama vile matumizi ya gesi asilia katika magari, katika viwanda na majumbani na pia kutumia gesi katika uzalishaji wa umeme badala ya mafuta.

(d) Kuyataka makampuni yanayoagiza mafuta na yenye maghala hapa Dar es Salaam, kule Dar es Salaam, kuwe na Bomba zaidi ya moja la kupokelea mafuta kutoka kwenye meli.

Kwa sasa kuna makampuni yenye bomba moja ambalo hutumika kushusha mafuta aina zote kwa zamu. Hali hii hukawiza meli bandarini kwa muda mrefu zaidi, na kuchelewesha meli nyingine na kuongeza *demurrage charges*.

(e) Kuwa na mipango mahususi ya ukarabati wa Gati kubwa ya kupakulia mafuta, yaani *Single Buoy Mooring (SBM)* kukamilika kwa gati hii kutaiwezesha nchi kuagiza shehena kubwa za mafuta na hivyo kuwa na uhakika wa kuwa na mafuta muda wote na kwa bei nafuu kwa sababu gharama za usafirishaji hupungua kadri meli inavyoongezeka ukubwa. Hatua hii pia itaiwezesha nchi kuwa na miundombinu mbadala ya kupokelea mafuta kinyume na sasa ambapo tegemeo ni gati la *KOJ* peke yake.

Nchi inaweza kupata uhaba mkubwa endapo *KOJ* itashindwa kufanya kazi hii kwa sababu moja au nyingine na jambo hili kwa kweli hatuliombei litokee.

(f) Kuwa na mipango thabiti ya kuboresha miundombinu ya kuwa na usafirishaji wa mafuta kwa njia ya reli kama hatua ya muda mfupi na pia kuwa na mfumo wa usafirishaji kwa njia ya bomba la mafuta kwa mtazamo wa muda mrefu. Hatua hizi zitawezesha usambazaji mafuta kuwa wa kutegemewa na wa kuaminika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea udhibiti wa bei za mafuta ya petroli nchini kuhusiana na Soko la Biashara ya bidhaa ya petroli la kimataifa ambapo bei inapangwa na nguvu za soko yaani *global supply and demand balance*. Upatikanaji na mahitaji ya dunia. Itakumbukwa kwamba mwezi Julai mwaka 2008 bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia ilifikia dola la Kimarekani 147 kwa pipa, kupanda huku kwa bei ya mafuta kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukuaji wa uchumi wa dunia ulioanza tangu mwaka 2002 wakati pipa la moja lilipokuwa linauzwa kwa wastani wa dola 20. Marekani ya Kaskazini na Bara za Ulaya ndizo nchi zilizokuwa zinaongoza kwa mahitaji ya mafuta ya petroli, katika miaka ya karibuni uchumi wa nchi za China, India na pia Brazil umekuwa unakua kwa kasi kubwa na hivyo kuongeza mahitaji makubwa ya petroli duniani jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limechangia kupanda kwa haraka kwa bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ghafi imechangia kwa kiwango kikubwa na inakwenda sambamba na bei ya mafuta yaliyosafishwa, vilevile bei ya mafuta yaliyosafishwa huchangia asilimia kubwa ya bei ya mafuta hapa nchini, hivyo uwezo wetu wa kupanga bei kinyume na bei ya dunia ni changamoto kubwa kwani bidhaa hii

huagizwa kutoka nje kwa asilimia 100. Kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia hadi kufikia kiasi cha dola 147 kwa pipa la mafuta ghafi mwezi Julai, kulichangia sana kupanda kwa bei ya bidhaa hapa Tanzania hadi ilipofikia wastani wa Sh. 2,000/= kwa lita.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya udhibiti katika bei. *EWURA* ni mdhibiti katika sekta ya mafuta ya petroli na majukumu ya kusimamia shughuli za kiuchimi, ubora wa bidhaa na miundombinu pamoja na bidhaa husika. Kwa vile soko la petroli lina ushindani wa kutosha na lina watoa huduma wengi, bei ya bidhaa hupangwa na nguvu ya soko. Inapotokea nguvu ya soko inashindwa kufanya kazi ipasavyo na tabia za ukiritimba zikaanza kujionyesha waziwazi, Sheria ya petroli inaruhusu *EWURA* kuingilia kati na kurekebisha vikwazo vinavyozuia nguvu ya soko kufanya kazi.

Kwa mfano, hali iliyojitokeza katika soko la bidhaa za mafuta hapa nchini baada ya bei ya bidhaa za petroli kuporomoka katika soko la dunia kuanzia katikati ya mwezi Julai, 2008 bei hiyo haikupungua kwa kasi hiyo kwa walaji wa hapa nchini, iliilazimu *EWURA* kuingilia kati. Kwa mujibu wa Sheria ya *EWURA* na Kanuni bora za udhibiti, *EWURA* imelazimika kuweka baadhi ya vigezo vitakavyotumika kupima ushindani katika soko. *EWURA* ilifanya mchakato wa haraka ili kuweka nyenzo zitakazotumika katika kupanga bei elekezi katika mazingira ya soko huria. Vigezo hivyo vilijadiliwa na kukubaliwa tarehe 9 Januari, 2009 *notes* ya Serikali Na. 5 ilichapishwa kwenye gazeti la Serikali kuipa nguvu ya kisheria *EWURA* kupanga bei elekezi ya bidhaa za petroli. *Notice* hiyo imefafanua kuwa *EWURA* itahusika katika kudhibiti bei kama mojawapo ya haya itatokea.

Kuwepo ushahidi wa kutosha wa watoa huduma kula njama za kupanga bei, yaani *price fixing* badala ya kushindana, bei kwa wastani ilikuwa zaidi ya asilimia 7.5 juu ya bei elekezi itakazotolewa na *EWURA*, *(Price gorging)* na kuwepo hali ya hatari, yaani *state of emergence*. *EWURA* imekamilisha mchakato wa mabadiliko haya na kuanza kupanga bei elekezi na bei ya kikomo katika biashara ya mafuta ya jumla na rejareja. Katika zoezi hili *EWURA* imefuata taratibu za kisheria ikiwemo ushirikishwaji wa wadau kupitia mchakato wa tafutishi.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* bado ni changa na inahitaji kujenga uwezo, bado haijawa na ofisi za kanda Mikoa, kwa hiyo itashirikiana na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya zote za Tanzania Bara na Ofisi zote za Wakala wa Vipimo ili kuhakikisha kwamba bei za mafuta zinazowekwa na *EWURA* kwa kila Makao Makuu ya Mkoa zinafuatwa. Wananchi wanaombwa kushiriki kwa kudai risiti ya malipo kila wanaponunua mafuta na wakiona bei inazidi kikomo elekezi na wanashauriwa kutoa ripoti kwa waliotajwa hapo juu kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, bidhaa za mafuta ya petroli zinatoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi zote duniani. Upatikanaji wa uhakika wa mafuta na kwa bei stahili vitachochea kukua kwa uchumi wa nchi yetu. Akiba ya mafuta yaliyopo nchini kwa sasa ni nzuri. Aidha, *EWURA* itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa soko

ikiwemo bei na akiba ikiwa ni pamoja na mipango ya kila kampuni ya kuagiza mafuta ili kuhakikisha kuwa kuna akiba ya kutosha ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, usalama wa watu na vyombo vya usafiri ni jambo muhimu katika usfirishaji wa mafuta ya petroli. Serikali inachukua nafasi hii kuwaasa wenye vyombo vya usafirishaji wa mafuta wahakikishe viko katika hali nzuri na kwamba watumiaji wa vyombo hivyo wanakuwa makini na waangalifu ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kutumia fursa hii kuwahimiza wafanyabiashara ya mafuta kuendelea kuheshimu Sheria na taratibu zinazoongoza biashara ya mafuta nchini. Serikali inawaahidi na itaendelea kutoa ushirikiano kwa wafanyabiashara waaminifu. Aidha, ninapenda kuwatahadharisha wafanyabiashara wa mafuta wasiokuwa waaminifu kwamba Serikali haitawavumilia hata kidogo na wala haitasita kuwachukulia hatua kali stahiki ili kulinda maslahi ya umma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa taarifa hiyo iliyo kamilifu kwenye suala hilo. Sasa kauli inayofuata ni ya Mheshimiwa ….

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni ya 37 (4) napenda kutoa hoja kwamba hati hii ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu ipangiwe muda wakati wowote utakaoona unafaa ili tuweze kuijadili na Wabunge wote washiriki.

**SPIKA:** Ahsante. Nimeipokea na ninaafiki hivyo, tutaitafutia muda katika Mkutano ujao ili iweze kujadiliwa. Sasa ni zamu ya Kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Mheshimiwa Waziri karibu!

## TAARIFA YA WAZIRI WA MIUNDOMBINU KUHUSU KAMPUNI YA NDEGE YA TANZANIA *(AIR TANZANIA COMPANY LIMITED-ATCL)* KWENYE BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA; TAREHE 11 FEBRUARI, 2009:

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa taarifa kuhusu Kampuni ya Ndege ya Tanzania – *ATCL* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Mkataba kati ya *ATCL* na Shirika la Ndege la Afrika Kusini *(SAA)* kusitishwa hapo mwezi Agosti, 2006, Serikali ilichukua hatua za kuteua Bodi na Menejimenti mpya ya *ATCL,* kazi ambayo ilikamilika Februari, 2007.

Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 iliisaidia *ATCL* kupata ndege mbili za kukodi aina ya *Boeing 737-200* pamoja na kutoa fedha shilingi bilioni 13.0 ili kuwezesha Kampuni kuendelea na shughuli zake wakati ikijiandaa na kupanga mikakati ya kujiendesha na kuacha kuitegemea *SAA.*

Wakati wa kuvunja Mkataba kati ya *ATCL* na *SAA*, Kampuni ilikuwa na ndege tatu aina ya *Boeing 737-200,* kati ya hizo, ndege moja ilikuwa ni mali ya *ATCL* na mbili zilikuwa za kukodi. Mwezi Septemba, 2008, ndege hiyo ya *ATCL* iliuzwa kutokana na uchakavu. Kwa sasa *ATCL* inazo ndege nne kama ifuatavyo:-

Ndege ndogo mbili aina ya *Bombadier Dash 8 Q300* zenye uwezo wa abiria 50 kila moja, ndege moja ya *Airbus A320* yenye uwezo wa abiria 150 na ndege moja aina ya *Boeing* 737-200 yenye uwezo wa abiria 104. Ndege mbili ndogo ni mali ya Kampuni wakati ndege za *Airbus A320* na *Boeing* 737-200 ni za kukodi. Ndege ya *Boeing 737-200* kwa sasa iko katika utaratibu wa kurejeshwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango Mkakati *(Stategic Plan)* wa *ATCL. ATCL* iliandaa Mpango Mkakati na *kuuwasilisha* Serikalini kwa ajili ya kupata fedha. Mpango huo ulionyesha kwamba mahitaji ya muda mrefu ya ATCL yanafikia Dola milioni 507.7. Mahitaji hayo ni pamoja na ununuzi wa ndege tisa za aina mbalimbali kwa matumizi ya safari za ndani na nje ya nchi, mafunzo kwa marubani na wahandisi pamoja na kubadili mifumo mbalimbali ya uendeshaji ili kuwezesha Kampuni kuhimili ushindani kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA).

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji ya *ATCL* kuwa makubwa na Serikali kutokuwa na fedha za kutosha ili kutekeleza Mpango wa kuimarishaji Kampuni, Serikali ililazimika kutafuta mwekezaji ambaye angekuwa tayari kushirikiana na Serikali kuendeleza *ATCL* kwa kutoa fedha za kutekeleza Mpango huo wa kampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Ubalozi wetu nchini China, mwezi Februari, 2007, tuliweza kupata Kampuni ambayo ilionyesha kuwa ipo tayari kununua asilimia 49 ya hisa za Serikali ndani ya *ATCL*. Kampuni hiyo kwa jina inaitwa *China SONANGOL International Limited (*CSIL*)* na Makao yake Makuu yako Hong Kong. *China SONANGOL International Limited (*CSIL*)* tayari imewekeza katika nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo Angola, Msumbiji na Ghana.

Baada ya mazungumzo ya awali kati yake na Wizara, Uongozi wa Kampuni hiyo ulikuja nchini mwezi Machi, 2007 na kutiliana saini Makubaliano ya

Biashara kati yake na Kampuni ya Ndege ya Tanzania. Aidha, mwezi Februari, 2008, Kampuni hiyo na *ATCL* zilitiliana saini Hati ya Makubaliano *(Memorandum of Understanding*). Hati hizi mbili zilizotiwa saini zinaonyesha maeneo mbalimbali ya uwekezaji pamoja na kuainisha majukumu ya pande zote mbili katika kuendeleza *ATCL*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutiliana saini Hati ya Makubaliano kati ya mwekezaji na *ATCL*; mwezi Mei, 2008, Wizara ya Miundombinu iliomba idhini ya Serikali kwa kuwasilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri Na.17/2008 ili Kampuni ya *China Sonangol* iweze kununua asilimia 49 ya hisa za Serikali ndani ya *ATCL*. Baraza la Mawaziri lilitoa uamuzi kwamba *ATCL* iundwe upya kwa kuuza hisa hadi asilimia 49 kati ya hisa 100 za Serikali ndani ya *ATCL* kwa mwekezaji huyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusu mwekezaji, kwa sasa kazi zifuatazo zinafanywa ili kukamilisha mchakato wa kuwezesha Kampuni ya *CSIL* kununua asilimia 49 ya hisa za Serikali ndani ya *ATCL*.

Nyaraka muhimu zitakazowezesha uuzaji wa hisa hizo ambazo zimekamilika; Nyaraka zilizokamilika ni Mkataba wa Uuzaji wa Hisa (*Share Sale and Purchase Agreement).* Mkataba wa Wanahisa (*Shareholders Agreement*) na *"Memorandum and Articles of Association"* ya Kampuni itakayoundwa.

Kazi ambazo zinaendelea ni Kukamilisha mahesabu ya *ATCL,* kazi ya kuhakiki Mahesabu ya *ATCL* yanayoishia Juni, 2008 inaendelea na inafanywa na Kampuni ya *Price Water House Coopers*. Kazi hii inategemewa kukamilika ndani ya mwezi Februari, 2009; Kufanya tathmini ya mali na madeni ya *ATCL,* kazi ya tathmini ya mali na madeni ya *ATCL* imeanza tarehe 13/1/2009 na inafanywa na Kampuni ya *Ernst & Young*.

Kazi hii itachukua wiki sita (6) kukamilika; Kazi ambayo bado haijafanywa ni kufanya tathmini ya Menejimenti ya *ATCL (Management Diagnosis).* Kazi hii inatarajiwa kufanywa na Kampuni ya *Aerogestion* ya Ufaransa kwa gharama za mwekezaji. Mkataba ulishasainiwa na kuwasilishwa kwa mwekezaji pamoja na ankara ya malipo. Kazi itaanza mara baada ya mwekezaji kutoa malipo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Kampuni ya *CSIL* imefanya yafuatayo:-

Kutoa amana (*deposit*) kwa ajili ya ndege saba (7) ambazo *ATCL* inatarajia kuzipata kuanzia mwaka 2012. Jumla ya Dola za Marekani milioni 2.5 zimetolewa kwa shughuli hiyo; Kutoa amana ya kukodisha ndege aina ya *Airbus A320* na kulipia gharama za wahandisi wa ndege hiyo kutoka Mauritius. Kiasi cha Dola 500,000 zilitumika katika dhamana na Dola 279,000 kwa ajili ya gharama za wahandisi.

Kulipia ndege mbili aina ya *Bombadier Dash 8 Q-300* ambazo sasa zinamilikiwa na *ATCL* na tayari zinatoa huduma. Jumla ya Dola za Marekani milioni 16.2 zimetolewa na CSIL kwa shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, kusimamishwa kwa ndefe za *ATCL* mwezi Desemba, 2008. Tarehe 10 Desemba, 2008, Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* ilisimamisha huduma zake ndani na nje ya nchi kutokana na Kampuni kushindwa kutimiza masharti ya usalama wa ndege zake kama yalivyotakiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*Tanzania Civil Aviation Authority)* na hivyo kunyang'anywa cheti cha uendeshaji *(Air Operator's Certificate).*

Mheshimiwa Spika, kunyang'anywa kwa cheti cha uendeshaji kulikofanywa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga kulikuwa ni hatua ya mwisho kwa Mamlaka baada ya kujaribu kuzuia hali hiyo isitokee, kwani Muda wa cheti kilichokuwepo ulikuwa umemalizika tangu mwezi Mei, 2008 na *ATCL* walitakiwa wapate cheti kingine kwa kuhuisha cheti kilichopo. *ATCL* waliomba kupatiwa cheti kipya, lakini Mamlaka ya Usafiri wa Anga ilishindwa kutoa cheti kipya kutokana na *ATCL* kutotimiza masharti ya Kanuni za Usafiri wa Anga za mwaka 2006, badala yake *TCAA* ilitoa cheti cha muda mfupi hadi Agosti, 2008 na kutakiwa kuyafanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa.

*ATCL* haikuweza kurekebisha kasoro zilizoainishwa na *TCAA* hadi ilipofika Agosti, *TCAA* iliiongezea *ATCL* muda zaidi hadi Oktoba, 2008. Mwezi Novemba, 2008, wakaguzi wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO)* waliifanyia ukaguzi Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga hapa nchini pamoja na baadhi ya mashirika ya ndege ikiwemo Kampuni ya Ndege ya Tanzania. Mashirika mengine yaliyokaguliwa ni *Precision Air, Coastal Travel* na *Tanzanair*.

Kwa kutumia Ripoti walizozipata kutoka *TCAA* kuhusu *ATCL* wakaguzi hao waligundua kuwepo kwa kasoro kadhaa ndani ya *ATCL* na waliitaka Mamlaka ya Usafiri wa Anga kusimamia kikamilifu Sheria na Kanuni za Usafiri wa Anga za 2006. Wakaguzi hao walitoa muda wa siku kumi kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga kuhakikisha kwamba kasoro zilizoainishwa kuwepo ndani ya *ATCL* zinarekebishwa na kama hazitarekebishwa, *ATCL* ichukuliwe hatua zinazostahili kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo ikiwa ni pamoja na kusitisha cheti cha uendeshaji cha *ATCL*.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wa *ICAO* walieleza wazi kwamba endapo muda wa siku kumi utamalizika bila *TCAA* kuchukua hatua zinazotakiwa, *ICAO*, kwa kutumia mamlaka ya kisheria iliyopewa chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Usafiri wa Anga, itaiweka Tanzania kwenye orodha ya nchi ambazo zimeshindwa kusimamia usalama wa usafiri wa anga kikamilifu *(black listed states).*

Mheshimiwa Spika, Athari za Nchi Kuwekwa Kwenye Orodha ya Nchi Zisizotekeleza Masharti ya Usalama wa Anga. Kutokana na Ripoti hiyo ya *ICAO* na tishio lililotolewa kwamba endapo hatua zinazotakiwa kuhusu *ATCL* hazitachukuliwa, Tanzania itawekwa kwenye orodha ya nchi ambazo zimeshindwa kusimamia usalama wa usafiri wa anga. Wizara ya Miundombinu ilikaa na *TCAA* na kubaini kwamba zipo athari ambazo nchi itapata endapo *TCAA* haitachukua hatua zifaazo kuhusu *ATCL*. Baadhi ya athari hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Tanzania itawekwa kwenye "*website*" ya *ICAO* na hivyo dunia nzima kujua na kuamini kwamba Tanzania siyo nchi salama katika usafiri wa anga.

(b) Wasafiri wanaokuja nchini wataacha au kusita kupanda ndege zote zinazotoa huduma ya usafiri wa anga nchini zikiwemo ndege za *ATCL* na pia ndege za mashirika mengine ambazo zimesajiliwa nchini.

(c) Mashirika yanayotoa huduma kwenye viwanja vyetu vya Kimataifa kama vile *KLM, BA, Qatar Airways, Emirates* na mengineyo yatasita kutua kwenye viwanja hivyo au kutoa masharti kwa Serikali kabla ya kutua.

(d) Bima za ndege zinaweza kupanda kwani nchi itaonekana kutokuwa na uwezo wa kusimamia usalama wa usafiri wa anga na hivyo kuonyesha kuwepo kwa hatari kubwa kwa ndege kuja na kufanya kazi Tanzania. Ni dhahiri kwamba uchumi wa nchi utaathirika kwani, watalii na wafanyabiashara wataacha au kusita kuja nchini mwetu Tanzania.

(e) Ilionekana pia kwamba muda wa siku kumi uliotolewa na *ICAO* usingetosha kwa *ATCL* kuondoa kasoro zilizokuwa zimeainishwa. Hivyo *TCAA* ililazimika kuchukua hatua za kuinyang'anya *ATCL* cheti cha uendeshaji *(Air Operator's Certificate)* tarehe 8 Desemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kufafanua kwamba kusitishwa kwa cheti cha uendeshaji cha *ATCL* hakuna maana kwamba ndege za *ATCL* zilisimamishwa kutokana na ubovu au kutokuwa na usalama. Kasoro ambazo ziliainishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ni zile zinazohusiana na usahihi wa nyaraka *(documentation)* pamoja na kuwepo kwa programu zinazotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Usafiri wa Anga za 2006. Hizi ni pamoja na programu za mafunzo kwa marubani, programu za matengenezo ya ndege, ukaguzi katika karakana ambazo ndege zinatengenezwa na mambo kama hayo. Ndege za *ATCL* ni nzima na hazina athari yoyote katika kuendeshwa kwake na marubani wake wana sifa zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kusitishwa kwa cheti cha uendeshaji, Wizara ya Miundombinu iliunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kuharakisha mchakato wa kuiwezesha *ATCL* kurejeshewa cheti cha uendeshaji kwa kupitia Nyaraka na Programu zilizokuwa na dosari kama zilivyoainishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga.

Timu hiyo ilibaini kwamba ili *ATCL* iweze kurejeshewa cheti chake ilitakiwa ikamilishe kwa ufasaha nyaraka kumi na tano na kutekeleza Programu tano. Aidha gharama za zoezi hilo ni Dola za Marekani 273,000. Kwa kushirikiana na wataalamu wa *ATCL* na Serikali kutoa fedha zilizotakiwa, Timu ilikamilisha zoezi hilo kwa usafaha na Mamlaka ya Usafiri wa Anga kurejesha cheti cha uendeshaji tarehe 30 Desemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba *ATCL* ilirejeshewa cheti chake, tarehe 30 Desemba, 2008, Kampuni haikuweza kuanza kutoa huduma mara moja kwani ilihitaji

fedha za uendeshaji kabla ya kuanza tena safari. *ATCL* iliwasilisha Serikalini ombi la shilingi bilioni 7.1 ambazo Serikali ingelazimika kuzitoa kwa matumizi ya miezi mitatu.

Serikali baada ya kuchambua maombi ya *ATCL* na kuona uhalali wake, ilitoa shilingi bilioni 4.5 katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ya shilingi bilioni 2.5 ilitolewa tarehe 3 Januari, 2009 na zilitumika kulipia madeni mbalimbali ya *ATCL*. Fedha hizo zilitumika pia kulipia mishahara ya wafanyakazi wa *ATCL* kwa mwezi Desemba, 2008 kiasi cha shilingi milioni 322. Awamu ya pili ya shilingi bilioni 2.0 ilitolewa tarehe 22 Januari, 2009 na *ATCL* ilianza kutoa tena huduma za usafiri wa anga tarehe 23 Januari, 2009. *ATCL* imeanza na vituo vya ndani vya Mwanza, Kilimanjaro, Tabora, Kigoma, Mtwara na Zanzibar kwa kutumia ndege mbili aina ya *Bombadier Dash* 8-Q300 zenye uwezo wa abiria 50 kila moja. Huduma za nje ya nchi ikiwemo safari za Johannesburg na Hahaya, Moroni, hazikuanza kutokana na ndege mbili kubwa kutakiwa kupelekwa kwenye matengenezo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu iliunda Kikundi Kazi *(Task Force)* ili kuchunguza kwa undani matatizo ya *ATCL* na kupendekeza hatua za kuchukuliwa. Kuundwa kwa Kikundi Kazi kunatokana na ukweli kwamba kwa muda mrefu *ATCL* imekuwa na matatizo mengi ya uendeshaji na usimamizi wa rasilimali zake. Kikundi Kazi kilianza kazi tarehe 29 Desemba, 2008 na ilipewa wiki tatu kukamilisha kazi hiyo. Aidha, Kikundi Kazi kilipewa hadidu za rejea zifuatazo:-

(a) Kubaini kwa ufasaha matatizo yanayoikabili Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL);*

(b) Kuchunguza kwa kina vyanzo vya matatizo yanayoikabili *ATCL* (kama yalivyobainishwa hapo juu);

(c) Kupitia mikataba ya ajira ya watendaji wakuu wa shirika na kubainisha mapungufu au kasoro katika ajira hizo kama zipo;

(d) Kupitia mikataba ya ukodishaji wa ndege za *ATCL* na kuainisha mapungufu au kasoro katika mikataba hiyo kama zipo;

(e) Kupendekeza hatua madhubuti za kuchukua (za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu) ili kutatua matatizo yaliyobainishwa;

(f) Kupendekeza mipango na mikakati madhubuti itakayohakikisha matatizo yaliyobainika hapo juu na mengine yanayofanana na hayo hayatatokea tena katika *ATCL* kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, Kikundi Kazi kilikamilisha kazi yake na kuwasilisha ripoti yake Serikalini tarehe 29 Januari, 2009. Wizara imeshapitia ripoti hiyo na kuchambua mapendekezo yake. Serikali hivi karibuni itafanya maamuzi ya hatua za kuchukua kuhusu utatuzi wa matatizo ya *ATCL*, kwa nia ya kuiimarisha Kampuni hiyo ya Ndege.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** nakushuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa taarifa yako yenye uwazi na iliyowasilishwa kikamilifu.

## TAARIFA YA WAZIRI MKUUKUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE YA MKATABA BAINA YA *TANESCO* NA *RICHMOND DEVELOPMENT*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 37(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge (Toleo la 2007), naomba kuwasilisha Taarifa ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya Mkataba baina ya *TANESCO* na Kampuni ya *Richmond Development Company LLC.*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa 12 wa Bunge niliwasilisha Taarifa ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Maazimio 23 ya Bunge juu ya Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC*. Katika Taarifa hiyo, nilitoa ufafanuzi wa kina wa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa kila Azimio kwa kipindi cha kuanzia mwezi Februari, 2008 Bunge lilipopitisha Maazimio hayo hadi tarehe 28 Agosti, 2008, nilipowasilisha Taarifa Bungeni. Aidha, nilielezea dhamira ya Serikali ya kuendelea na utekelezaji wa baadhi ya Maazimio ambayo yalihitaji muda mrefu zaidi kukamilisha mchakato wake, hasa yale yaliyohusu marekebisho ya Sheria na Mifumo mbalimbali na pia yale yaliyohitaji kufungua Mashtaka ya Jinai au Mashtaka ya Makosa ya Nidhamu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Nishati na Madini chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shelukindo, Mbunge wa Bumbuli kwa kupitia Taarifa hii. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge yamesaidia kuboresha Taarifa ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika Taarifa niliyoiwasilisha hapa Bungeni mwezi Agosti, 2008 nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, mchakato wa utekelezaji wa Maazimio kumi kati ya 23 ambayo ni: Namba 4, 6, 10, 13, 15, 16, 19, 21, 22 na 23, ulikuwa umekamilika. Hivyo, katika Taarifa ya leo, nitaeleza hatua zaidi zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza Maazimio yaliyobaki ambayo yalihitaji muda mrefu zaidi ingawa mchakato wake ulishaanza katika kipindi kilichopita. Aidha, katika hatua hii tuliyofikia leo, Maazimio mengine mawili ambayo ni Na. 17 na 18 nayo yamekamilika. Maelezo ya utekelezaji wa maazimio yote yaliyobaki kwa ujumla wake ni kama ifuatavyo:-

Azimio la kwanza, “Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 (*Public Procurement Act*, 2004) haina nguvu ya kutosha. Sheria ipitiwe upya ili kuiboresha kwa kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* nguvu zaidi za udhibiti na uwezo wa kuchukua hatua pale Sheria na Kanuni zinapokiukwa, badala ya kutoa ushauri tu kama ilivyo sasa.”

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa, Mapendekezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004, Sura ya 410 umekamilika na Serikali inatarajia kuwasilisha Muswada huo katika Mkutano ujao wa 15 wa Bunge.

Azimio la pili, "Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* isiwajibike Wizara ya Fedha ambayo nayo ni Taasisi ya Ununuzi (*Procuring Entity*) badala yake iwe chombo huru kinachowajibika, Ofisi ya Rais na Taarifa zake kuwasilishwa Bungeni."

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa. Kulingana na Sheria ilivyo hivi sasa, *PPRA* ni Taasisi/Idara chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa msingi huo, uchambuzi uliofanyika hadi sasa umeonyesha kuwepo mapungufu ya kiutendaji ambayo yanaifanya *PPRA* isiwe Taasisi huru yenye uwezo wa kutoa maamuzi yake bila ya kuingiliwa na Chombo kingine isipokuwa katika masuala ya Kisera. Hivyo, Muundo mpya wa chombo hiki utategemea uchambuzi na mapendekezo yatakayotolewa wakati wa mchakato mzima wa Marekebisho yanayotarajiwa kufanywa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 yatakayowezesha chombo hiki kuwa huru na kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Azimio la tatu, "Mikataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC (uliorithiwa na Dowans Holdings S.A)* na ile kati ya *TANESCO* na *IPTL, SONGAS, AGGREKO* na *Alstom Power Rentals* ipitiwe upya mapema iwezekanavyo kama ambavyo Mikataba ya Madini ilivyopitiwa upya na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme utawaelemea wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania."

Mheshimiwa Spika, katika Azimio hili, nitaeleza hali ilivyo sasa kwa Mikataba baina ya *TANESCO* na *SONGAS, AGGREKO, Alstom Power Rentals, IPTL* na *Richmond Development Company LLC* uliorithiwa na *DOWANS*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa Mkataba huu, naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu historia ya Mkataba huu.

Majadiliano kuhusu Mradi wa Songo Songo yalianza mwaka 1994 kati ya Timu ya Serikali na Mwekezaji, wakati huo *Consortium* ya *Transcanada Pipelines* na *Ocelot International (OTC*), kutoka Canada. Wawekezaji hao walipatikana kwa njia ya ushindani ambao ulishirikisha Makampuni 16.

Baada ya kupata Mwekezaji, Tanzania ikiwa ni Mwanachama wa Jumuiya ya Madola, iliona ni busara kutumia Chombo Maalum cha Wataalam wa Uchumi na Sheria ambacho kiliundwa mahsusi kusaidia Nchi Wanachama kuangalia Mikataba ya Gesi na Madini. Hivyo, kabla ya kuanza utekelezaji wa Mradi huu wa Songo Songo, mwezi Julai, 1997, Mikataba ya Mradi huu hususan ile ya *Power Purchase Agreement-PPA na Production Sharing Agreement-PSA* ilidurusiwa na Wataalam wa Kitengo hicho cha *Economic and Legal Advisory Services (ELAS)* cha *Commonwealth Secretariat.* Durusu hiyo ilithibitisha kuwa, kwa ujumla Mradi ulikuwa wa manufaa kwa Serikali na kuwa Mikataba ilikuwa na uwiano *(balanced)* kati ya *TANESCO* na Wawekezaji. Hivyo, Timu

ya Serikali iliyokuwa ikiendesha majadiliano licha ya kuwa na msimamo wake, ilitumia ushauri huo wa Wataalam wa *ELAS* katika kuboresha na hatimaye kukamilisha Mikataba ya *SONGAS*.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa utekelezaji wa Mradi wa Songo Songo, kwa nyakati tofauti Serikali imekuwa ikifanya marekebisho kadhaa ili kuhakikisha kuwa Mradi huu unazingatia maslahi ya nchi yetu. Kwa mfano, kuanzia mwaka 1998 hadi 2004 kulifanyika marekebisho hususan pale palipotokea mabadiliko ya wanahisa na umiliki wa Mradi kutoka *Consortium* ya *Transcanada* kwenda Kampuni ya *CDC Globeleq* ya Uingereza.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yalifanywa mwaka 2005 kufuatia *SONGAS* kuongeza mitambo miwili yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa jumla ya MW 70. Ili kupunguza mzigo wa gharama za miradi hiyo, hasa gharama za *capacity charge*, uzoefu wa nchi mbalimbali umeonyesha kuwa zimekuwa zikigharamia baadhi ya shughuli za awali au kupata fedha kwa njia nyingine hususan kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka Taasisi za Fedha za Kimataifa. Kwa kutambua manufaa hayo, moja ya marekebisho muhimu yaliyofanywa mwaka 2005 ni pamoja na kuweka kipengele cha kuiruhusu Serikali/*TANESCO* kubadili mtaji uliotumika kwenye kulipia gharama za Mitambo hiyo kuwa mkopo, pale fursa ya *Refinancing* itakapojitokeza kwa lengo la kupunguza kiwango cha *capacity charge.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kipengele hiki, Serikali imepata mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Marekani milioni 42 ambao ni takriban shilingi bilioni 52.4 kwa ajili ya *Re-financing* ya mtaji wa mitambo ya *SONGAS*. Mkataba husika ulisainiwa Januari, 2008 kati ya Serikali na Benki ya Dunia. Taratibu za Kibenki zinatarajiwa kukamilika na fedha kupatikana kuanzia mwishoni mwa mwezi Februari, 2009. Majadiliano ya awali na *SONGAS* kuhusu Miradi ya Gesi Asilia yameanza yakilenga kupunguza mzigo wa malipo yanayotolewa na *TANESCO* kwa *SONGAS*.

Katika mchakato huo, *Refinancing* inatarajiwa kupunguza malipo ya *capacity charge* kwa takriban Dola za Marekani milioni moja au sawa na shilingi bilioni 1.2 kwa mwezi. Hivi sasa, *capacity charge* zinazolipwa na *TANESCO* kwa *SONGAS* ni wastani wa Dola za Marekani milioni saba kwa mwezi kwa Megawatt 183. Hivyo, kutokana na unafuu tulioupata, kwa miaka 15 iliyobaki ya muda wa *Power Purchase Agreement (PPA)* wa miaka 20 unaoanzia Julai, 2004, ni sawa na punguzo la Dola za Marekani zisizopungua milioni 180 takriban shilingi bilioni 224.6.

Mheshimiwa Spika, katika majadiliano hayo, Serikali inawakilishwa na Timu ya Wataalamu wetu wenyewe *(Gas Working Group)* kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *TPDC* na *TANESCO*. Aidha, Serikali inaendelea kupata ushauri wa Wataalamu wa Kimataifa wa *Hunton & Williams* wa Marekani. Serikali imeamua kuwa, Timu hiyo ya Wataalam itapanuliwa ili kushirikisha Wanasheria kutoka Sekta Binafsi kwa lengo la kuwapa uzoefu kwenye Mikataba ya Gesi Asilia.

Mheshimiwa Spika, vilevile kutokana na uzoefu tulioupata katika kupitia Mikataba ya Gesi Asilia, Serikali inaandaa hadidu za rejea pana zaidi zitakazotumika katika kutayarishwa *Model Power Purchase Agreement (MPPA)* ambazo zitatumika katika majadiliano ya Mikataba ya Sekta ya Nishati itakayotekelezwa na wazalishaji umeme binafsi nchini, *(Independent Power Producers - IPP)*. Kuwepo kwa *Model* hiyo kutapunguza muda unaotumika wakati wa majadiliano na pia kuainisha kwa uwazi vipengele vya majadiliano. Zoezi hili litaihusisha pia Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)* kwa lengo la kuhakikisha kuwa masuala yanayohusiana na udhibiti wa Sekta ya umeme yanazingatiwa. Kwa hiyo, juhudi za kupitia mikataba hii zitaendelea kila mara ili kuhakikisha mikataba hiyo inakuwa ni kwa maslahi ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mkataba baina ya *TANESCO* na *Alstom Power Rentals (APR)* ulimalizika muda wake tangu tarehe 19 Machi 2008. Aidha, Mkataba kati ya *TANESCO* na *AGGREKO* nao ulimalizika muda wake tarehe 26 Novemba, 2008. Baada ya kumalizika kwa muda wa Mikataba hiyo, Serikali kupitia TANESCO ilikataa kuongeza muda wa Mikataba hiyo.

Mara baada ya Mikataba husika kumalizika muda wake, Makampuni ya *AGGREKO* na *ALSTOM* yalianza utaratibu wa kuondoa mitambo yao. Hata hivyo, kutokana na utata wa masuala ya kodi, mitambo yote ilizuiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Eneo linalobishaniwa na Makampuni yote mawili ni tafsiri ya mikataba juu ya malipo ya Kodi. Baada ya Mitambo hiyo kuzuiliwa na *TRA*, Kampuni ya *AGGREKO* imefungua shauri la kupinga hatua hiyo katika Mahakama ya Kodi Nchini. Shauri hilo bado halijatolewa uamuzi. Kwa upande wa Kampuni ya *Alstom Power Rentals* hakuna shauri lililofunguliwa hadi hivi sasa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nimeona ni vyema nizungumzie masuala yanayohusu Mikataba kati ya *TANESCO* na *IPTL*; na Richmond uliorithiwa na *DOWANS* kwa pamoja. Hii ni kwa sababu *TANESCO* ina mashauri mbalimbali yaliyopo Mahakamani dhidi ya *IPTL* na *Richmond Development Company* uliorithiwa na *DOWANS.*

Mheshimiwa Spika**,** kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, muhtasari wa maelezo kuhusu hali ya Kimahakama kwa kila Kampuni ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kueleza suala la Mkataba baina ya *TANESCO* na Kampuni ya *IPTL*. Baada ya kutokea Mgogoro kuhusu kiwango cha *capacity charge* ambacho *TANESCO* ilipaswa kuilipa Kampuni ya *IPTL, IPTL* ilifungua Shauri la Madai Na. *07CV10366(AKH)* Mjini *New-York* - Marekani, tarehe 15 Novemba, 2007 dhidi ya Serikali ya Tanzania iliyokuwa Mdhamini wa *TANESCO* katika Mradi huu. *TANESCO* kupitia Mawakili wake ilipinga hatua hiyo kwani *IPTL* ilikiuka vipengele vya Mkataba vilivyoainisha kuwa, mgogoro wowote kati ya wahusika wa Mkataba huu, ulipaswa kupelekwa kwenye Mahakama ya Usuluhishi. Kwa kuzingatia hoja hii, tarehe 15 Aprili, 2008 Mahakama ya Mjini *New-York*, Marekani ilitoa uamuzi kuwa, mgogoro kati ya *IPTL* na *TANESCO* uwasilishwe kwenye Mahakama ya Usuluhishi kama Mkataba baina ya pande hizi mbili unavyoelekeza.

Baada ya maamuzi hayo, tarehe 20 Juni, 2008 *IPTL* ilifungua Shauri Na. ARB98/8 dhidi ya *TANESCO* kwa Msuluhishi wa Kimataifa (*International Centre for Settlement of Investment Dispute (ICSID)* Mjini London, Uingereza. Tarehe 16 Desemba, 2008 Mahakama ya Usuluhishi iliamua kusimamisha Shauri husika kufuatia Uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania katika Shauri la Madai Na. 49/2002 lililofunguliwa na Kampuni ya *VIP Engineering* (mmoja wa Wanahisa wa *IPTL*) tarehe 25 Februari, 2002 akiomba ateuliwe mfilisi wa muda wa *IPTL*. Katika Shauri hilo, Mahakama Kuu ilitoa Amri kuwa *IPTL* ni mfilisi na hivyo kuwekwa chini ya mfilisi wa muda (*Provisional Liquidator*) ambaye ni Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(The Registration Insolvency and Trusteeship Agency - RITA).* Hatua hii ilitokana na mgogoro uliokuwepo wa kutoelewana baina ya Wanahisa wa Kampuni ya *IPTL*.

Vilevile tarehe 23 Desemba 2008, Mwanahisa Mkuu wa *IPTL*, *Mechmar,* alifungua Shauri katika Mahakama ya Rufani Tanzania *(Civil Revision No. 179 of 2008)* akiomba mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu kuhusu ufilisi wa *IPTL*. Katika hatua nyingine, tarehe 22 Januari, 2009 bila ya mfilisi wa muda kuwa na taarifa, Benki ya *Standard Chartered (Hong Kong)* ilifungua Shauri la Madai Na. 5/2009 katika Mahakama Kuu ya Tanzania kwa nia ya kumteua Msimamizi *(Administrator)* wa *IPTL*. Shauri hili lilitokana na kuwa, Benki ya *Standard Chartered* ndiyo mkopeshaji mkubwa wa *IPTL*. Katika Shauri hilo, Mahakama Kuu tarehe 27 Januari, 2009 ilitoa amri ya upande mmoja *(Exparte Order)* ya kuteua Kampuni ya Mawakili wa *CRB Attorneys* kuwa Msimamizi wa *IPTL (Administrator).*

Kufuatia uteuzi huo, tarehe 4 Februari, 2009 Kampuni ya *VIP Engineering* nayo imefungua Shauri Na. 11/2009 dhidi ya *Standard Charterd Bank* na Msimamizi (*CRB Attorneys*) katika Mahakama ya Rufaa kupinga Uamuzi wa Mahakama Kuu kuteua Msimamizi wa *IPTL*.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, ni wazi kwamba suala hili la *IPTL* kwa sasa liko katika mchakato mbele ya Mahakama hapa Tanzania na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Oktoba, 2008 na 27 Novemba, 2008, Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* na *Dowans Holdings SA* na *DOWANS Tanzania Limited* walifungua Mashauri mawili Na. 15910/VRO na 15947/VRO dhidi ya *TANESCO* katika Mahakama ya Usuluhishi *(International Court of Arbitration – ICC)* iliyopo Nchini Ufaransa wakidai jumla ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 119 (takriban shilingi bilioni *150.8)* kwa madai mbalimbali yakiwemo kusitishwa kwa Mkataba isivyo halali, kuzuiwa kutekeleza Mkataba kutokana na kuchelewa kwa malipo ya *Letter of Credit*, kuharibiwa sifa ya Kampuni na kutolipwa *capacity charge* kulingana na Mkataba.

Kufuatia Shauri hilo, *TANESCO* nayo imewasilisha majibu yake dhidi ya madai hayo tarehe 30 Januari, 2009. Isitoshe pia, *TANESCO* katika majibu yao *(counter claim)* wamedai kulipwa jumla ya Dola za Kimarekani 8,980,209.17 (takriban shilingi bilioni 11.1) fedha ambayo ni sehemu ya Dola za Kimarekani 30,696,598 (takriban shilingi bilioni 39.4) zilizotolewa kama malipo ya awali kwa Kampuni ya *DOWANS* kwa

makubaliano kwamba, fedha hizo zitarejeshwa na mwekezaji kwa kukatwa kwenye malipo ya *capacity charge* kila mwezi kwa miezi 24 kuanzia tarehe 3 Oktoba, 2007 hadi tarehe 2 Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, wakati masuala ya usuluhishi yakiwa bado hayajatolewa uamuzi, *TANESCO* ilipata taarifa kuwa *DOWANS* walikuwa na mpango wa kuuza Mtambo wao wa kuzalisha umeme. Kutokana na hali hiyo, tarehe 18 Desemba, 2008 *TANESCO* ilifungua Shauri Na. 19/2008 dhidi ya *DOWANS Tanzania Limited* katika Mahakama Kuu ya Tanzania kuiomba Mahakama kuizuia Kampuni ya *DOWANS* kuuza Mitambo hiyo hadi pale suala la Usuluhishi lililopo Nchini Ufaransa litakapotolewa uamuzi. Katika Shauri hilo, tarehe 19 Desemba, 2008, *TANESCO* ilipata Amri ya Mahakama Kuu kuzuia *DOWANS* kuuza au kuhamisha Mitambo yake kutoka eneo la Ubungo Dar es Salaam hadi Shauri hili litakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya, ni dhahiri kabisa kwamba mashauri haya yote mbalimbali niliyoyaeleza hapa nayo yapo mbele ya Mahakama. Katika Mkataba kati ya *TANESCO* na *IPTL* pekee, yapo mashauri katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi Nchini Uingereza, Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

Vilevile, Wahusika Wakuu katika Shauri hili sasa wameongezeka wakiwemo Mechmar - Mwenye Hisa Mkuu wa *IPTL*, *VIP Engineering* Mwenye hisa chache katika *IPTL*, *Standard Chatered Bank* ya *Hong Kong* ambaye ni Mkopeshaji wa *IPTL*, Mfilisi wa Muda wa *IPTL* na Msimamizi wa *IPTL* badala ya wawili wa awali, yaani *TANESCO* na *IPTL*. Vilevile, kwa upande wa *Dowans*, yapo mashauri katika Mahakama ya Kimataifa nchini Ufaransa na Mahakama Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika**,** nimeona niyaeleza haya kwa kuwa kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 64 (1)(c) ambayo inaweka tahadhari kwa Bunge kujadili au kuzungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama. Kanuni hiyo inapatikana katika kifungu 64(1) na sehemu ndogo ya (c).

Kwa maoni yangu, Kanuni hii inaliweka Bunge katika hali kutozungumza masuala haya niliyoyataja ambayo ni pamoja na kesi ambazo zinaikabili Kampuni ya *Independent Power Tanzania Limited (IPTL)* na *Richmond Development Company LLC* ambayo imerithiwa na *DOWANS,* kwani masuala hayo hadi sasa hatujayafikia mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo na uelewa wangu, ndiyo maana nimetoa maelezo ya jumla jumla kuhusu mchakato wa Mashauri yaliyopo katika Mahakama yanayohusiana na Mikataba baina ya TANESCO na *Richmond Development Company LLC* na ule wa *IPTL* badala ya kutoa kwa undani mambo ambayo yanaweza kuwa ni masuala ambayo yanahitajika Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Maazimio namba 5, 7, 9 na 14. Maudhui ya Maazimiom mzima wa Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond*, pamoja na wale wa TAKUKURU waliofanya uchunguzi wa suala hili. Watumishi hao wamegawanyika katika Makundi yafuatayo:-

(i) Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wakili wa Serikali, Bw. Donald Chidowu;

(ii) Wajumbe wote wa Kamati ya Wataalam na ile ya Majadiliano *(Government Negotiating Team - GNT)* ambao ni pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Uchumi (kwa wakati ule Bwana Gray Mgonja); Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini; Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Maofisa Waandamizi wapatao 12 kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma; na

(iii) Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU pamoja na Maofisa wa TAKUKURU wapatao 9 walioshiriki katika zoezi la uchunguzi na kuandaa taarifa kuhusu mchakato wa Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC.*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za nidhamu zinazohusika na Watumishi hao wa Umma zimekamilisha uchambuzi wa maelezo ya utetezi yaliyotolewa na kila mtumishi aliyeshiriki kwenye mchakato wa zabuni ya Mkataba baina ya *TANESCO* na Richmond na wale wa TAKUKURU. Hata hivyo, kwa sasa zoezi linaloendelea ni Vyombo vya Dola kufanya uchunguzi zaidi ili kuona kama kuna Makosa yoyote ya Jinai yaliyotendwa na mtumishi yeyote wa umma katika mchakato wa Mkataba huu. Ushauri wa Vyombo hivyo ndio utakaowezesha Serikali sasa kuona ni watumishi gani watakaostahili kuingia kwenye mchakato wa hatua za kinidhamu na wale watakaoonekana kutenda Makosa ya Jinai kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Maazimio ya Bunge Namba 8 na 14 nayo yanafanana kwa kuwa yalitaka Serikali iwawajibishe Viongozi wenye dhamana ya kisiasa waliokuwa Mawaziri wa Nishati na Madini ambao ni Mheshimiwa Nazir Karamagi na Mheshimiwa Dkt. Ibrahim Msabaha.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa Bungeni kuwa Mawaziri hao walijiuzulu mwezi Februari, 2008 kwa kuwajibika kwao kisiasa kutokana na suala hili. Hata hivyo, Serikali iliona ni busara vyombo vya dola vifanye uchunguzi zaidi kwa lengo la kujiridhisha kama kulikuwa na uvunjaji wowote wa maadili katika kushughulikia mchakato wa Zabuni ya Mkataba huu baina ya *TANESCO* na *RICHMOND*. Taarifa tulizonazo ni kuwa vyombo vya dola vimefikia hatua za mwisho za uchunguzi wa suala hili tayari kwa ajili ya kuwasilisha suala hilo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na vyombo vingine vinavyohusika.

Azimio namba 11. "Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995 (*The Public Leadership Code of Ethics Act*) ifanyiwe marekebisho makubwa ili kudhibiti utaratibu unaoonekana wa kawaida sasa wa viongozi waandamizi wenye dhamana ya kisiasa kuendelea na biashara zao binafsi wakiwa madarakani, jambo ambalo lina mgongano wa kimaslahi. Serikali ianze rasmi maandalizi ya majadiliano ya kina kuhusu suala hili ndani na nje ya Bunge kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali."

Katika utekelezaji wa Azimio hili, Serikali imeunda Kikundi Kazi *(Task Force)* ambacho kinajumuisha Wajumbe kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na TAKUKURU.

Kamati hiyo, imepewa jukumu la kufanya uchambuzi wa kina wa maoni ya wananchi ambayo yamekuwa yakiwasilishwa kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhusu kuweka utaratibu wa Viongozi Waandamizi wenye dhamana ya kisiasa na Watendaji wa ngazi ya juu katika Utumishi wa Umma kutenganisha shughuli zao za biashara na Uongozi ili kuondoa mgongano wa kimaslahi. Kamati itakapokamilisha kazi hii, itawasilisha mapendekezo yake Serikalini na hatimaye yatatolewa taarifa.

Azimio namba 12: "Serikali ijiepushe kadri inavyowezekana na utaratibu wa kutumia Mawakala katika ununuzi wa Umma na kuhakikisha kuwa Wizara zote zina taarifa za bei halisi za mahitaji yao kila wakati ili kujiepusha na mchezo wa kawaida wa Mawakala kupandisha bei mara mbili au zaidi ya bei halisi."

Pamoja na hatua za awali zilizochukuliwa na Serikali za kutekeleza Azimio hili, Mtaalam Mwelekezi aliyepewa kazi na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* ya kuandaa Mfumo wa ununuzi wa pamoja *(common used items)* pamoja na kuandaa utaratibu wa kupata takwimu za Bei Dira za bidhaa mbalimbali *(Indicative Price)* kutoka kwa wazalishaji wa bidhaa na huduma, amekamilisha kazi hiyo mwezi Septemba, 2008. Taarifa ya Mtaalam mwelekezi huyo, imekwishafanyiwa uchambuzi wa awali na *PPRA* kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali wa Huduma za Ununuzi *(Government Services Agency)* na inatarajiwa kujadiliwa na Makatibu Wakuu wa Wizara zote tarehe 17 Februari, 2009. Mapendekezo yatakayotokana na majadiliano hayo yatasaidia sana kuimarisha marekebisho ya Muundo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA).*

Azimio namba 17: "Msajili wa Makampuni *(BRELA)* aifute Kampuni ya *Richmond Development Company* (T) *Ltd* mara moja kutoka kwenye orodha ya Makampuni halali Nchini."

Utekelezaji wa Azimio hili umekamilika baada ya Msajili wa Makampuni *(BRELA)* kuifuta rasmi Kampuni ya *Richmond Development Company (T) Limited* tarehe 2 Oktoba, 2008 katika orodha ya Makampuni nchini. Taarifa hiyo ilichapishwa kwenye Gazeti la Serikali, Toleo la 44 (*Government Notice* Na. 551) lililotolewa tarehe 31 Oktoba, 2008 na pia kusambazwa kwenye Magazeti mbalimbali nchini.

Azimio namba 18: "Wamiliki wa *Richmond Development Company LLC* na *Richmond Development Company* (*T) Ltd* wafunguliwe kesi ya jinai mara moja kwa udanganyifu na ujanja wa kuiibia Serikali."

Timu Maalum ya Vyombo vya Dola iliyoundwa na Serikali kushughulikia jambo hili imekamilisha Uchunguzi wake. Taarifa ya awali imewasilishwa Serikalini ili

kuwezesha kufungua Mashtaka ya Makosa ya Jinai dhidi ya Wamiliki wa Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* na *Richmond Development Company (T) Ltd* na Wawakilishi wao.

Sambamba na hatua hiyo, Bw. Naeem Adam Gire mmoja wa Wawakilishi wa Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* tarehe 13 Januari, 2009 alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam ambapo alisomewa Mashtaka matano yakiwemo: -

(1) Kutoa hati za uongo kwa Taasisi mbalimbali za Serikali;

(2) Kughushi Hati ya Wakili kuonyesha kuwa ameidhinishwa Kisheria na Bw. Mohamed Gire ambaye ni Mmiliki wa Kampuni ya *Richmond Development Company LLC* ya Texas, Marekani kufanya kazi za Kampuni hiyo nchini;

(3) Kutoa taarifa za uongo kwa Bodi ya Zabuni ya Shirika la Umeme Tanzania na Watumishi wa Umma kwamba Kampuni ya Richmond ina uwezo wa kuzalisha umeme nchini na pia kushawishi waipendekeze Kampuni hiyo kupewa Zabuni hiyo;

(4) Kutoa taarifa za uongo kwa Wajumbe ya Timu ya Majadiliano ya Serikali kwamba Kampuni hiyo ina mitambo yenye uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 105.6 ili kuwezesha kupendekezwa kuzalisha umeme huo; na

(5) Kutoa hati za uongo kuonyesha kuwa Bw. Mohamed Gire alimwidhinisha kufanya biashara za Kampuni ya Richmond Nchini Tanzania.

Azimio namba 20: "Serikali iendeshe uchunguzi maalum ili kubaini ukweli kama Taarifa rasmi ya TAKUKURU iliyotoa matokeo ya uchunguzi kuhusu mchakato wa Richmond ilikataliwa na kuharibiwa na kutolewa nyingine na kama jalada halisi linalohusu Kampuni ya Richmond lililokuwa *BRELA* liliharibiwa na kuwekwa lingine kwa lengo la kuficha ukweli."

Utekelezaji wa Azimio hili unafanyika sambamba na Azimio Na. 18 ambapo Kamati Maalum ya Vyombo vya Dola iliyoundwa na Serikali inatarajiwa kuwasilisha Taarifa yake ya uchunguzi wa suala hili Serikalini muda si mrefu kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha Mchakato wa utekelezaji wa Maazimio kadhaa kwa kiwango kikubwa. Hivi sasa, maazimio machache yaliyobaki ni yale ambayo utekelezaji wake unahitaji kukamilisha mchakato wa taratibu za marekebisho ya Sheria na Vyombo vya Dola kufanya upelelezi au uchunguzi zaidi. Taratibu hizo zinaendelea kufanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba basi kumalizia kwa kuwashukuru wewe mwenyewe na Kamati ya Uongozi ya Bunge na kuendelea kuishukuru Kamati ambayo ilitoa maoni yake na maoni ambayo yamekwishasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge

na mimi vilevile nipata fursa  ya kuona *comments* zao tutafanyia kazi na tutajaribu kuja kulielezea tena Bunge lako Tukufu namna tulivyoshughulikia hizo *additional comments*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa taarifa hiyo. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaelezeni mapema, tunafuata utaratibu wa kanuni ya 37. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini ili kupokea maoni kuhusu Taarifa hiyo ya Serikali. Mheshimiwa Marombwa kwa niaba ya Mwenyekiti.

**MHE. ABDUL J. MWAROMBWA (K.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali juu ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Taarifa ya Serikali juu ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Mkataba baina ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge pamoja na Waziri wa Nishati na Madini kwa lengo la kupokea taarifa hiyo katika kikao kilichofanyika tarehe 9 Februari, 2008 Ofisi ya Bunge Dodoma ikiwa ni kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Uongozi ya Bunge ya kuzitaka Kamati za Kudumu za Bunge kushughulikia taarifa zinazotolewa na Serikali kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia taarifa hiyo Kamati yangu ilikumbushwa kwamba maombi 10 kati ya 23 yaliyotolewa na Bunge utekelezaji wake ulikuwa umekamilika na maazimio hao ni namba 4, 6,10, 13, 15, 16, 19, 21, 22, 23. Katika kuipitia taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwezi Agosti, 2008. Kamati yangu imebaini kwamba Azimio 10, 13 na 15 hayakutekelezwa ipasavyo. Naomba nieleze juu ya utekelezaji ambao haukukamilika wa maazimio haya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Azimio hili linatamka kwamba:- “Gavana wa Benki Kuu pamoja na Bodi ya Wakurugenzi wachunguze kwa makini uhalali wa malipo ya ziada (US$ 4,865,000) yaliyofanywa kwa *Dowans Holdings* A.S iliyorithi majukumu ya *Richmond Development Company* na kuwachukulia hatua waliohusika na uzembe huo.”

Mheshimiwa Spika, kufuatia majibu yaliyotolewa juu ya utekelezaji wa azimio hili, Kamati haijaridhika na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 13.  Azimio hili linatamka kwamba:-"Serikali izihusishe Kamati za Kudumu za Bunge kwenye hatua za awali za maandalizi ya Mikataba mikubwa ya kibiashara na ya muda mrefu ili kuondokana na utaratibu uliopitwa na wakati kwamba Mikataba ya Kibiashara ni siri, hata kwa walipa kodi wenyewe.  Aidha, Serikali ihakikishe kuwa, Kamati zote za Bunge zinapitia Mikataba mikubwa ya kibiashara na ya muda mrefu chini ya Sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima."

Mheshimiwa Spika, Azimio hili limejibiwa kwamba; Nanukuu: "Serikali imeanza kufanya tafiti katika Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola ili kupata uzoefu zaidi utakaosaidia katika utekelezaji wa suala hili"

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshindwa kuelewa ni utafiti gani ambao Serikali inaufanya mpaka sasa, kwani katika utafiti uliofanywa na Kamati umebaini kwamba, nchini Afrika Kusini kazi ya kujadiliana mikataba ya kibiashara mikubwa au ya kibiashara, kimsingi ni kazi ya Serikali; iko chini ya Mamlaka ya Serikali, lakini haipati nguvu ya kisheria na kuanza kutumika bila kuridhiwa na Bunge na Baraza la Majimbo *(National Council of Provinces).*

Hivyo basi, ili mchakato wa kuridhia uwe rahisi Waziri mhusika huzieleza Kamati husika za Bunge na Baraza juu ya lengo, maudhui, faida na changamoto zilizopo kabla ya kuanza mazungumzo/majadiliano *(negotiations)* ili kupata maoni ya jumla ya Kamati ya kuzingatiwa katika majadiliano hayo.

Kabla ya majadiliano kufika mwisho, Serikali hurudi tena kwenye Kamati hizo kutoa picha halisi ya majadiliano na kupata ushauri wa mwisho wa Kamati hizo. Kamati hukaribisha wadau wa sekta husika, katika hatua hiyo. Aidha, Kamati zinaweza kushauri, kuukubali au kuukataa Mkataba kwa manufaa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, azimio hili bado halijafikia tamati ya utekelezaji. Kwa kutumia mfano tajwa hapo juu, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na utekelezaji wa azimio hili katika muda muafaka ili kuepuka madhara tuliyoshuhudia katika mikataba iliyoingiwa kati ya Mashirika ya Serikali na Kampuni za Nje ya Nchi ikileta matatizo hata kupelekea Baraza la Mawaziri kujiuzulu.

Mheshimiwa Spika, la msingi ni kuweka utaratibu mzuri wa mawasiliano na ushiriki wa Kamati husika ambao hauingilii maeneo ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 15.  Azimio hili linatamka kwamba:-"Utaratibu wa kuteua Wakurugenzi na Makamishna katika Wizara kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara zao unazua mgongano wa kimaslahi na kudhoofisha usimamizi pamoja na uwajibikaji, hivyo Serikali iupige marufuku mara moja."

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na majibu yaliyotolewa na Serikali kuwa "zipo pia faida za baadhi ya Wakurugenzi au Makamishna kuwa Wajumbe wa Bodi hasa katika kusaidia kutoa msimamo na ufafanuzi wa Sera na mipango mbalimbali ya

Serikali". Ushauri wa Kamati ni kuwa Wakurugenzi na Makamishna katika Wizara washiriki inapobidi kama *ex-officials.*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Maazimio mengine. Azimio Na. 1. Azimio hili linatamka kwamba:-"Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 *(Public Procurement Act, 2004)* haina nguvu ya kutosha.

Sheria ipitiwe upya ili kuiboresha kwa kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* nguvu zaidi za udhibiti na uwezo wa kuchukua hatua pale Sheria na Kanuni zinapokiukwa, badala ya kutoa ushauri tu kama ilivyo sasa."

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kamati inakubaliana na hatua ambazo Serikali imechukua katika utekelezaji wa azimio hili ambapo tayari Mapendekezo ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo yamekamilika. Ni matarajio ya Kamati kuwa Muswada huo utawasilishwa Bungeni katika Mkutano wa 15 wa Bunge kwa ajili ya marekebisho husika.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 2. Azimio hili linatamka kwamba:- "Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* isiwajibike Wizara ya Fedha ambayo nayo ni Taasisi ya Ununuzi *(Procuring Entity)* badala yake iwe chombo huru kinachowajibika Ofisi ya Rais na Taarifa zake kuwasilishwa Bungeni."

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kamati inakubaliana na jinsi azimio hili linavyotekelezwa. Ni matumaini ya Kamati kuwa pendekezo hili lililotolewa litazingatiwa ipasavyo katika marekebisho yanayotarajiwa kufanyika kwenye sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 3. Azimio hili linatamka kwamba:-"Mikataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC* (uliyorithiwa na *Dowans Holdings* S.A) na ile kati ya *TANESCO* na *IPTL, SONGAS, AGGREKO* na *Alstom Power Rentals* ipitiwe upya mapema iwezekanavyo kama ambavyo Mikataba ya Madini ilivyopitiwa upya na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme utawaelemea wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania".

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa azimio hili Kamati ina maoni yafuatayo:- Serikali iangalie upya muda uliobaki kwa Mkataba wa *SONGAS* kukamilika kwani ina mashaka na majibu yaliyotolewa ya miaka 15 iliyotamkwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika kuona kwamba wataalamu wanasheria kutoka sekta binafsi watahusishwa katika mchakato wa majadiliano ya awali na *SONGAS* ili kuwapa uzoefu kwenye Mikataba ya Miradi ya Gesi Asilia. Pamoja na kushirikisha Wataalamu kutoka sekta binafsi. Vilevile, Serikali iwahusishe wataalamu mabingwa katika sheria za biashara za Kimataifa kutoka katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na utaratibu unaopendekezwa wa kuwa na "*Model Power Purchase Agreemenst" (MPPA)* ambao utarahisisha shughuli za majadiliano ya mikataba mbalimbali. Hivyo, tunaiomba Serikali kuishirikisha Kamati ya

Bunge husika inayojihusisha na sekta hii katika kujifunza juu ya matumizi ya utaratibu huu wa *MPPA*.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kuwa majibu ya Taarifa ya Waziri Mkuu hayajaainisha kiasi cha Tozo ambacho Kampuni ya *Richmond/DOWANS* ilitakiwa kulipa kwa kuchelewa kuzalisha umeme katika siku zilizokubaliwa kwenye Mkataba baina yake na *TANESCO*, hivyo Kamati ingependa kufahamu kama Tozo hilo limezingatiwa katika deni ambalo *TANESCO* inaidai *DOWANS*.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 5, 7, 9 na 14. Maudhui ya Maazimio haya yanafanana ambapo yanaitaka Serikali kuwawajibisha Watumishi wote wa Umma waliohusika katika Majadiliano kwenye mchakato mzima wa Mkataba baina ya *TANESCO* na *RICHMOND*.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa maazimio hayo, Kamati ina maoni kwamba uwajibishaji wa watumishi hao upewe kipaumbele kwa kuwa wao binafsi na nafasi ambazo bado wanazishika huku wakiendelea kuchunguzwa zinatia shaka juu ya utendaji wao wakati huu wa kuchunguzwa. Hivyo, mamlaka husika zishauriwe kutumia taratibu na kanuni zilizopo ambapo mtuhumiwa anaweza kupewa likizo maalum, kusimamishwa kazi katika kipindi cha uchunguzi au kubadilishiwa sehemu ya kazi ili kumwepusha na kuingilia uchunguzi. Hizi sio adhabu bali mbinu za kiutawala na kiutumishi za kushughulikia matukio ya ukosaji kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 8 na 14. Maudhui ya Maazimio haya yanafanana kwa kuwa yanaitaka Serikali kuwawajibisha Viongozi wenye dhamana ya kisiasa waliokuwa Mawaziri wa Nishati na Madini ambao ni Mheshimiwa Nazir Karamagi na Mheshimiwa Ibrahim Msabaha.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na uwajibikaji wa Mawaziri hao kisiasa ila inaomba taarifa ya uchunguzi wa makosa yao itolewe haraka kwa kuwa uchunguzi umefikia hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 11. Azimio hilo linatamka kwamba;- "Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 1995 *(The Public Leadership Code of Ethics Act)* ifanyiwe marekebisho makubwa ili kudhibiti utaratibu unaoonekana wa kawaida sasa wa Viongozi Waandamizi wenye dhamana ya kisiasa kuendelea na biashara zao binafsi wakiwa madarakani, jambo ambalo lina mgongano wa kimaslahi. Serikali ianze rasmi maandalizi ya majadiliano ya kina kuhusu suala hili ndani na nje ya Bunge kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali."

Mheshimiwa Spika, Kamati imepokea Taarifa na kuridhishwa na hatua ambazo zinachukuliwa katika kutekeleza azimio hili. Hata hivyo, inashauri kwamba kasi iongezwe katika kufanyia marekebisho sheria husika kabla Bunge hili halijamaliza muda wake.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 12. Azimio linatamka kwamba: "Serikali ijiepushe kadri inavyowezekana na utaratibu wa kutumia Mawakala katika ununuzi wa Umma na kuhakikisha kuwa Wizara zote zina taarifa za bei halisi za mahitaji yao kila

wakati ili kujiepusha na mchezo wa kawaida wa Mawakala kupandisha bei mara mbili au zaidi ya bei halisi.”

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza azimio hili lakini inashauri kwamba Serikali iweke muda muafaka wa ukamilishaji wa kuandaa Mfumo huo wa Ununuzi wa Pamoja na utaratibu wa kupata takwimu za Bei Dira *(indicative Price)* za bidhaa mbalimbali, unaopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 17. Azimio hili linatamka kwamba: “Msajili wa Makampuni *(BRELA)* aifute Kampuni ya *Richmond Development Company (T) Ltd.* mara moja kutoka kwenye orodha ya Makampuni halali Nchini.”

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza azimio hili kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 18. Azimio hili linatamka kwamba: “Wamiliki wa *Richmond Development Company LLC* na *Richmond Development Company (T) Ltd* wafunguliwe kesi ya jinai mara moja kwa udanganyifu na ujanja wa kuiibia Serikali.”

Mheshimiwa Spika, Kamati haijaridhika na utekelezaji wa azimio hili kwani mmiliki wa Kampuni hizi ambaye alisaini Mkataba kati ya *Richmond Development Company LLC* na *TANESCO*, Bw, Mohammed Gire hajafikishwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 20. Azimio hili linatamka kwamba: “Serikali iendeshe uchunguzi maalum ili kubaini ukweli kama Taarifa rasmi ya TAKUKURU iliyotoa matokeo ya uchunguzi kuhusu mchakato wa Richmond ilikataliwa na kuharibiwa na kutolewa nyingine na kama jalada halisi linalohusu Kampuni ya Richmond lililokuwa *BRELA* liliharibiwa na kuwekwa lingine kwa lengo la kuficha ukweli”.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika kuona kwamba utekelezaji wa azimio hili umefikia mwisho na kuiomba Serikali kuwasilisha taarifa husika kwenye Mkutano wa Bunge ujao wa 15.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yanayohitaji ufafanuzi. Kamati ingependa kupata maelezo ya kina kutoka kwenye uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kuhusu dhamira halisi ya Shirika hilo kuingia kwenye mchakato wa zabuni ya kununua mitambo ya kuzalisha umeme ya Kampuni ya *DOWANS* huku ikijua kuwa, Utekelezaji wa maazimio ya Bunge ulikuwa bado haujakamilika na Serikali na Kampuni za *Richmond Development Company LLc*, *DOWANS Holdings SA* na *DOWANS Holdings (T) Ltd* zilikuwa tayari zimefungua Mashauri mawili Na. 15910/VRO na 15947/VRO dhidi ya *TANESCO* katika Mahakama ya Usuluhishi *(International Court of Arbitration – ICC*) iliyopo nchini Ufaransa wakidai jumla ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 119 kwa madai mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge Kamati imebaini mkanganyiko wa takwimu za malipo halisi ambayo *TANESCO* inaidai Kampuni ya *DOWANS* na malipo ambayo kampuni hiyo ilikuwa imeyapokea katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2007.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuishukuru Serikali kwa kutekeleza kikamilifu baadhi ya maazimio na kuiomba iendelee kutekeleza Maazimio yaliyobaki kwa kasi nzuri ili suala hili lifungwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na Wabunge wengine ambao walikuja kwenye vikao vya Kamati kutuunga mkono. Michango yao imewezesha kutoa Taarifa katika muda mfupi. Naomba niwataje Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:- Mheshimiwa William H. Shellukindo – Mwenyekiti; Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe - M/Mwenyekiti; Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Yahya K. Issa; Mheshimiwa Asha M. Jecha; Mheshimiwa Halima M. Mamuya na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya.

Wengine ni Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa - ninayesoma taarifa hii, pia ni Mjumbe, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki; Mheshimiwa Mohammed H.J. Mnyaa; Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi; Mheshimiwa Dr. James A. Msekela; Mheshimiwa Omar Shekha Mussa; Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa; Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe; Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko; Mheshimiwa Charles N. Mwera; Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa; Mheshimiwa Christopher O. Ole Sendeka na Mheshimiwa Mohammed S. Sinani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashilillah pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndugu Emmanuel Mpanda na Ndugu Lina Kitosi, kwa kuihudumia vyema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa yetu hii leo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Cheyo unasimama tu wala husemi chochote, sijui.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika. Katika ukurasa wa tatu, Azimio la 15 naona kama vile kwamba Kamati imetengua Azimio la Bunge kwa kusema Kamati inakubaliana na majibu yaliyotolewa na Serikali kuwa zipo pia faida za baadhi ya Wakurugenzi au Makamishna kuwa Wajumbe wa Bodi hasa katika kusaidia kutoa msimamo na ufafanuzi wa sera na mipango mbalimbali ya Serikali, maana yake Azimio la Bunge linasema utaratibu huu usite mara moja.

**SPIKA:** Endelea

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Naomba Mwongozo wako?

**SPIKA:** Tatizo lako lipi sasa, ni tafsiri?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Tatizo langu ni kwamba, Azimio la Bunge utaratibu usite mara moja. Kamati inasema inakubaliana na kuna faida ya kuwa na Wakurugenzi kuwa Wajumbe wa Bodi. *So this is contradiction*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ufafanuzi ni kama ifuatavyo:- Ukisoma hapa katika taarifa ya Kamati pale ukurasa wa nne, Kamati ya Nishati na Madini, nanukuu, wanasema: "Kamati inakubaliana na majibu yaliyotolewa na Serikali kuwa zipo pia faida za baadhi ya Wakurugenzi kuwa Wajumbe wa Bodi." Sasa ushauri wa Kamati ni kwamba Wakurugenzi na Makamishna hao sasa washiriki inapobidi kama *ex-officials*.

Nadhani hii ni tafsiri ya busara tu unapokuta jambo lina maelezo kwa maana ya usimamizi mzuri, kufikisha sera kwenye zile Bodi. Kamati inatushauri kwamba hoja iliyoipokea kutoka kwa Serikali ina mantiki. Tusizizuie Kamati zinapokuta jambo ni tofauti kidogo, basi ziendelee tu mpaka zigonge ukuta, hiyo itakuwa sio utekelezaji mzuri wa shughuli za Kibunge.

Kwa hiyo, sioni kwamba hapa ni mgongano wa moja kwa moja ama kukataa Azimio la Bunge, hapana. Wametupa taarifa kwamba baada ya kupata majibu wameona ipo hoja kwamba kwa baadhi ya Bodi ni vizuri washiriki na ndiyo maana wamependekeza kwamba hawa sasa wawe *ex-official* ili wafungwe katika kupiga kura. Nadhani ni utekelezaji wa busara kabisa wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Cheyo nimekwishatoa *ruling*, wewe unataka malumbano. Hairuhusiwi kwa kanuni zetu kufanya malumbano na Spika. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautoshi kwa maana ya kwamba tumetoa kwa zile taarifa za Waheshimiwa Mawaziri ni muda usiozidi dakika 30 na Waheshimiwa Wenyeviti kutoa maoni ya Kamati nimetoa muda usiozidi dakika 15. Sasa muda uliobaki hautoshi, kwa hiyo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00.

*(Saa 06.48 mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

**Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya uendeshaji Sioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania *TRL* unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India.**

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliomalizika Dodoma tarehe 25 Aprili, 2008 hoja binafsi ya uendeshaji usioridhisha wa Kampuni ya Reli Tanzania unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya India iliwasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati.

Mheshimiwa Spika, Bunge lilijadili hoja binafsi kuhusu uendeshaji usioridhisha wa usafiri wa reli unaoendeshwa na Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* na kuazimia Serikali ifanye yafuatayo ili kuondoa kasoro mbalimbali za uendeshaji katika kampuni hiyo na kuweka uwiano mzuri katika menejimenti ya kampuni utakaoleta ufanisi wa reli ya kati na kuwapunguzia adha watumiaji wa reli:-

(i) Kuangalia mkataba wa ukodishaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya *RITES* ili kuondoa dosari zote zilizopo kwa maslahi ya Taifa.

(ii) Kwa kuwa Serikali ina hisa asilimia 49 na Kampuni ya *RITES* hisa za asilimia 51, Menejimenti ya Shirika hili iwe na uwiano sawia kati ya Watanzania na Wakodishaji hao; na

(iii) Kwa kuwa stesheni na magenge mengi yamefungwa, zichukuliwe hatua madhubuti za kuhakikisha usalama wa reli na vyombo vyake vyote.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Serikali kukodisha shughuli za uendeshaji wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*, shirika lilikuwa na matatizo ya uchakavu wa njia ya reli, mabehewa ya mizigo, abiria na injini za gari moshi, yote haya yalitokana na ukosefu wa mtaji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa taarifa ya Maazimio ya Bunge, napenda kwanza kutoa historia fupi ya namna zoezi la kukodisha Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* lilivyoanza na kutekelezwa. Serikali kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 29/2006 uliweka utaratibu wa ukodishaji wa huduma za Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* ambao uliruhusu utumike utaratibu wa ubia "*Joint Concessional Financing*" katika kuendesha na kugharamia *Tanzania Railways Ltd* kati ya Serikali na *RITES* ya India.

Mheshimiwa Spika, Utendaji wa Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)*, Shirika la Reli Tanzania lilikodishwa kwa kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* ambayo inamilikiwa kwa hisa asilimia 51 za *RITES* ya India na asilimia 49 za Serikali ya Tanzania. Kampuni hii ina mkataba wa ukodishaji wa kuendesha huduma zilizokuwa zinatolewa na *TRC* kwa muda wa miaka 25. Kwa mujibu wa mkataba wa ukodishaji wa *TRC*, Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* ilikabidhiwa rasmi shughuli za uendeshaji wa reli tarehe 1 Oktoba, 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kampuni ya Reli Tanzania kukabidhiwa uendeshaji wa biashara ya huduma za reli, mapungufu na matatizo yafuatayo yalijitokeza:-

(a) Kutokurekebishwa mikataba ya ukodishaji wa Shirika baada ya Serikali ya Tanzania kununua hisa 49%.

(b) Menejimenti ya Kampuni ya Reli Tanzania kutozingatia mkataba wa ukodishaji kwa mfano, kutotoa taarifa ya mapato kwa wakati; kusitisha huduma ya treni ya Ruvu – Tanga na Moshi – Arusha bila kibali cha *RAHCO*.

(c) Mgogoro wa wafanyakazi kutokana na Menejimenti ya *TRL* kutotekeleza makubaliano ya kulipa nyongeza ya mishahara ya kima cha chini yaliyofanywa kati yake na *TRAWU*.

Mheshimiwa Spika, hatua za awali zilizochukuliwa na Serikali. Baada ya kubaini mapungufu hayo, Wizara yangu iliunda Kamati kuhakiki hesabu za *TRL* pamoja na utendaji wake tarehe 6 Aprili, 2008. Pamoja na Wizara ya Miundombinu Kamati hii ilihusisha wadau wengine kama Fedha, Kazi, *SUMATRA, TRAWU* na *RAHCO*. Kamati hiyo ilipewa hadidu rejea zifuatazo:-

(i) Kuhakiki hesabu za TRL;

(ii) Kuangalia utendaji wa *TRL* kuhusu taratibu za mapato, Mikataba ya manunuzi ya huduma na vifaa, ubora na utendaji wa injini na kushauri hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii kwa ujumla ilibaini maeneo yafuatayo ambayo yalionekana kuwa na upungufu au udhaifu katika utendaji wa *TRL*:-

(a) Kupungua kwa mapato kutokana na *TRL* kutokuwa na mikakati mizuri ya kuwarejesha wateja wadogo wadogo wanaotumia reli ambao awali walifikia asilimia 60, kutokana na wateja wadogo kuacha kutumia reli kiwango hicho kimeshuka kufikia asilimia 26.

(b) *TRL* kutozingatia misingi bora ya biashara na kutokuwa wazi kwenye sera yake ya biashara kwa wateja.

(c) Kuwa na matumizi makubwa ya mafuta kwa kukodisha injini ndogo na dhaifu za daraja la 73xx.

Taarifa ya Kamati hiyo iliwasilishwa Wizara ya Miundombinu na Wizara iliwasilisha taarifa hiyo Wizara ya Fedha kwa hatua zaidi kama msimamizi wa hisa za Serikali kwenye kampuni ya *TRL*. Wizara ya Fedha ilichambua taarifa hiyo na kupeleka maoni yake *International Finance Corporation (IFC)* wakiwa wakopeshaji wa fedha za kuendeshea *TRL*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Azimio la Bunge. Kama nilivyosema awali kwenye utangulizi Bunge liliazimia na kuiagiza Serikali kwamba iangalie mkataba wa ukodishaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya *RITES* ili kuondoa dosari zote zilizopo kwa maslahi ya Taifa. Aidha, kwa kuwa Serikali ina hisa asilimia 49 na Kampuni ya *RITES* hisa za asilimia 51, Menejimenti ya Shirika hili iwe na uwiano sawia kati ya Watanzania na wakodishaji hao na pia kwa kuwa stesheni na magenge mengi yamefungwa zichukuliwe hatua madhubuti za kuhakikisha usalama wa reli na vyombo vyake vyote.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa baadhi ya mambo muhimu yaliyobainishwa katika Azimio la Bunge Serikali ilishaanza kuyashughulikia. Azimio la Bunge la tarehe 25 Aprili, 2008 liliipa msukumo mpya Serikali wa kutekeleza wa kazi ambayo tayari ilikwishaanza na Kamati ambayo iliundwa na Serikali tarehe 6 Aprili, 2008.

Mheshimiwa Spika, kupitia Kamati ya Wataalam "*Post Diverstiture Technical Team (PDTT)*" iliyoundwa na *Consolidated Holding Corporation* ilichambua kwa kina Mikataba mbalimbali ya *TRL*. Kamati hiyo ilichambua dosari zilizopo katika Mkataba wa Ukodishwaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya *RITES*, Mkataba wa Wanahisa na makubaliano yaliyoanzisha Kampuni *(Memarts)* ya *TRL*. Lengo la Serikali la kufanya mapitio hayo ni kubaini mapungufu yaliyokuwa kwenye Mikataba hiyo kama ilivyoagizwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo ilipewa muda wa miezi miwili wa kukamilisha kazi yake. Kamati imekamilisha kupitia mikataba hiyo na kuainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake. Kamati ya Serikali imebainisha maeneo yafuatayo ambayo yanahitaji kuboreshwa:-

Kamati ilichambua Mikataba iliyotajwa hapo juu na kubaini kuwa kuna maeneo yanayohitaji kuboreshwa kama ifuatavyo:-

(i) Mkataba wa Ukodishaji "*Concession Agreement*":

Kuweka mipango ya biashara na uboreshaji wa huduma (*Business plan)* ya Kampuni kuwa sehemu ya Mkataba ili kufuatilia utekelezaji wake;

Kuwa na vigezo vya kupima utendaji na kuboreshwa kwa vigezo vya namna ya kukatisha mkataba;

Mkodishaji kutokujiingiza kwenye biashara nyingine nje ya uendeshaji na uboreshaji wa huduma za reli.

(ii) Mkataba wa Wanahisa *(Shareholders Agreement)* vipengele vifuatavyo vilianishwa:

Kuwepo na kifungu kitakachoelezea wazi utaratibu wa manunuzi ya huduma na vifaa ndani ya kampuni;

Kuongeza idadi ya Wakurugenzi wa Bodi;

Kutenganisha majukumu ya Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi; na

Mikataba ya Usimamizi wa Uendeshaji, Misaada ya kiufundi na Mikopo iamuliwe na Wanahisa.

(iii) Mkataba wa Makubaliano ya Kuanzisha Kampuni *(Memorandum and Articles of Association ya TRL)*vipengele vilivyoanishwa ni kama ifuatavyo:-

Kuongeza idadi ya Wakurugenzi wa Bodi;

Kila mwanahisa awe na haki ya kuchagua na kuondoa Wakurugenzi wa Bodi wanaomwakilisha;

Mwenyekiti wa Bodi asiwe Mwenyekiti Mtendaji;

Wanahisa wateue Wakurugenzi mbadala (*alternate directors);* na

Kuwepo na kipengele kinachowapa nguvu Wanahisa kuteua Menejimenti.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Menejimenti ya sasa kuteuliwa na *RITES* pekee, Kamati ya Serikali imependekeza kwa mwanahisa mwenza kwamba Menejimenti sasa ichaguliwe na wanahisa kwa uwiano wa hisa.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2008, jopo la Wakaguzi wa Reli walihakiki hatua za utekelezaji wa mkakati wa usalama wa reli inayoendeshwa na *TRL (Audit of safety plan)* kama ulivyoidhinishwa na *SUMATRA*. Katika ukaguzi huo ilibainika kwamba *TRL* ilikuwa haijachukua hatua za kutekeleza mkakati huo.

Katika njia za reli ya Tanga, Singida na Mpanda ambako wafanyakazi walihamishwa na Magenge na baadhi ya Stesheni kufungwa, hakuna kazi zilizofanyika kwa kipindi cha karibu mwaka mmoja. *TRL* imeamua kukabidhi kazi hizo kwa Makandarasi ambao watafanya matengenezo ya njia kwa kutumia wafanyakazi wao wenyewe. Mikataba hiyo ndiyo kwanza imeanza kukabidhiwa kwa Wakandarasi. Wizara yangu kwa kupitia vyombo vyake itakuwa inafuatilia utendaji wa Wakandarasi hao ili kuhakiki matengenezo na usalama wa reli.

Mheshimiwa Spika, huduma za safari za treni za mizigo katika reli ya Tanga zilirejeshwa kuanzia tarehe 18/6/2008. Aidha, *TRL* ilirejesha pia huduma za uchukuzi wa mizigo katika njia ya reli ya Korogwe – Tanga – Moshi kuanzia mwezi Agosti, 2008.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo. Serikali ina hisa asilimia 49 na Kampuni ya *RITES* hisa za asilimia 51, Kampuni hii ni ya ubia. Maamuzi au mchakato wowote wa kuinusuru Kampuni hiyo ni budi ufanye baada ya makubaliano ya wanahisa wote wawili.

Kutokana na matatizo mbalimbali yaliyoko *TRL,* Serikali tayari imeunda Kamati ya Majadiliano ya kurekebisha Mikataba ya Ukodishaji, Uwanahisa na *Articles of Association* kama nilivyosema hapo awali; Kamati ya Serikali imewasilisha

mapendekezo ya kurejea *(review)* vipengele mbalimbali katika Mkataba wa Ukodishwaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya RITES, Mkataba wa Wanahisa, *Memarts* zilizoanzisha Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* na mkataba wa menejimenti kati ya *RITES* na *TRL*; Kikao cha kwanza cha majadiliano ya Wanahisha kilifanyika tarehe 27 Novemba, 2008 na kingine kilifanyika tarehe 8-9 Januari, 2009 na majadiliano ya Wanahisa bado yanaendelea na Taarifa ya matokeo ya majadiliano yatawasilishwa Serikalini baada ya majadiliano hayo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, majadiliano hayo yatalenga kukubaliana kufanya marekebisho niliyoyataja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na hatua zilizokwishachukuliwa na ambazo zinaendelea kuchukuliwa, Taarifa ya Kamati ya Majadiliano itawasilishwa Serikalini kwa ajili ya hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Ikiwa haitakupa usumbufu sana kwa sababu tulichopewa sisi kina taarifa pia ya *TICTS* pengine ungeweza kuendelea na hiyo tuokoe muda ili baada ya hapo sasa, Mwenyekiti naye atoe maoni ya Kamati kwa sehemu zote mbili. Upo tayari Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Nipo tayari.

**SPIKA:** Karibu sana.

## Taarifa ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Juu ya Utendaji Kazi Usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, hoja binafsi kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)* iliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa 11 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliomalizika Dodoma tarehe 25 Aprili, 2008. Hoja hiyo iliwasilishwa na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi - Mbunge wa Mbozi Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Bunge lilijadili hoja binafsi kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS)* na kuazimia kwamba, Serikali isitishe nyongeza ya Mkataba na kufanya mapitio ya Mkataba wa awali ili vifungu vya Mkataba huo ambavyo havina manufaa kwa Taifa virekebishwe. Baada ya muda wa Mkataba wa awali wa miaka kumi kumalizika, nyongeza yoyote ya Mkataba au Mkataba mwingine mpya uzingatie Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004.

Uamuzi wa Serikali wa Kukodisha Kitengo cha Makasha. Kabla ya kutoa Taarifa ya hatua za utekelezaji wa Azimio la Bunge, napenda nianze kwa kutoa historia fupi ya namna zoezi la kukodisha Kitengo cha Makasha lilivyoanza na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha cha Bandari ya Dar - es - Salaam kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* na *International Container Terminal Services Inc*. *(ICTSI)* ya *(Philipines)* Ufilipino na *Tanzania International Container Terminal Services Ltd (TICTS)* ulitiwa saini tarehe 5 Mei, 2000. Kwa mujibu wa Mkataba, *ICTSI* ni Mwekezaji Mahiri *(Strategic Investor)* na *TICTS* ni kampuni iliyoundwa na wenye hisa kwa ajili ya kuendesha Kitengo cha Makasha *(Terminal Operator).*

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulifanyiwa marekebisho mwaka 2001, ambapo *ICTSI* ilihamisha hisa zake zote kwenda *Hutchison International Port Holdings* ya Hong Kong. Hivyo kwa mujibu wa marekebisho hayo Mwekezaji Mahiri ni *Hutchison International Port Holdings (HPH)* ya Hong Kong.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya pili ya Mkataba huu, yalifanyika mwaka 2005 ambapo maeneo yafuatayo katika Mkataba yalifanyiwa marekebisho:-

(i) Muda wa Mkataba uliongezwa kutoka miaka 10 hadi miaka 25;

(ii) Upanuzi wa eneo tengefu *(designated area)* kwa kuongezewa gati namba 8, yadi namba 8 na Kituo cha Kuweka Mizigo cha Ubungo (Ubungo *ICD*);

(iii) Ongezeko la ada ya pango kwa awamu kutoka USD 3,680,000 kwa mwaka kuongezwa kama ifuatavyo:-

Kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2006 ada ya pango ni *USD* 5 milioni kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 5;

Kuanzia tarehe 1 Oktoba 2011 ada ya pango itakuwa *USD* 6.5 milioni kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 5;

Kuanzia tarehe 1 Oktoba 2016 mpaka mwisho wa Mkataba (2025) ada ya pango itakuwa *USD* 7 milioni kwa mwaka.

*TICTS* kuendelea kuwa na ukiritimba wa kuhudumia meli za makasha *(exclusivity for handling fully cellular container vessels)* katika Bandari ya Dar es Salaam hadi hapo itakapohudumia makasha 650,000 *TEUs* kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa Sera ya Serikali kujiondoa katika shughuli za kibiashara ili kuwezesha ufanisi wa utendaji katika taasisi zilizokuwa

zinasimamiwa na Serikali, Kitengo cha Makasha katika Bandari ya Dar es Salaam kilikodishwa kuwezesha mambo yafuatayo:-

(i) Kuboresha utendaji ili kuongeza mchango wa Sekta ya Bandari katika uchumi wa Taifa;

(ii) Kupunguza gharama za kuhudumia shehena ya makasha inayopita Bandari ya Dar es Salaam;

(iii) Kuvutia shehena ya ndani na nje inayopita kwenye Bandari ya Dar es Salaam; na

(iv) Kuingiza teknolojia mpya na kuwawezesha Watanzania kupata mbinu mpya za uongozi na usimamizi wa bandari.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha, *TICTS* ilianza rasmi shughuli za uendeshaji wa Kitengo cha Makasha tarehe 10 Septemba, 2000. Katika kipindi cha awali hadi kufikia mwaka 2005, utendaji wa Kitengo cha Makasha uliongezeka na wakati huo huo, shehena ya makasha ilikuwa ikiongezeka. Kuanzia mwaka 2006, utendaji ulianza kushuka na kusababisha msongamano wa meli na mlundikano wa makasha katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kushuka kwa utendaji wa TICTS kwenye shughuli za kuhudumia makasha ilibainika kuwa kuna upungufu katika baadhi ya vipengele vya Mkataba na hivyo kusababisha Serikali kuunda kamati ya kupitia upya na kurekebisha Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha, katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 25 Machi, 2008 Serikali iliunda Kamati ya Serikali ya Majadiliano ama *GNT* ili kupitia Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha. Lengo lilikuwa ni kubaini maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho kwa maslahi ya Taifa. Kamati hiyo inahusisha Wizara na Taasisi zifuatazo; Wizara ya Miundombinu; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Viwanda; Biashara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; Msajili wa Hazina; Mamlaka ya Mapato; Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na "*Consolidated Holding Corporation*" *(CHC).*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Mkataba na nyaraka mbalimbali zikiwemo Taarifa za Utendaji na Mahesabu ya mwaka ya *TICTS (Annual Reports and Accounts).* Aidha, Kamati ilibainisha vipengele vya Mkataba vinavyotakiwa kurekebishwa au kufutwa kwa manufaa ya Taifa kama ifuatavyo:-

(i) Ukiritimba wa huduma za makasha (*Exclusivity*);

(ii) Vigezo vya kupima utendaji (*Performance Indicators*);

(iii) Eneo tengefu *(Designated Area)* ambapo mkataba unataka tarehe 1 Januari, 2009 gati Na. 8 likabidhiwe kwa *TICTS*;

(iv) Kuongeza kiwango cha pango *(Rental Fees)*, mrahaba *(royalty)* na dhamana ya utendaji *(Performance Guarantee);*

(v) Kupunguza muda wa kukodisha *(Lease period)* toka miaka 25 kuwa miaka 10;

(vi) *TICTS* kurudisha vifaa vilivyokwisha muda wake wa matumizi kwa *TPA*;

(vii) Kuweka kipengele ndani ya Mkataba kinachokataza unyofoaji wa vipuri *(Cannibalisation of Equipment)* na kuongeza kifungu kinachotoa adhabu;

(viii) Kurekebisha utaratibu wa ukusanyaji wa tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari *(Wharfage).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji kuhusu suala zima la kushughulikia kasoro zilizopo katika Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha, Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kuleta ufanisi na kuiwezesha Serikali kuongeza mapato yake kama ilivyoazimiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 25 Aprili, 2008 katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Bunge liliazimia kwamba Serikali isitishe nyongeza ya muda wa Mkataba na kufanya mapitio ya Mkataba wa awali ili vifungu vya Mkataba huo ambavyo havina manufaa kwa Taifa virekebishwe. Vilevile, Azimio la Bunge liliazimia kwamba Serikali, baada ya muda wa Mkataba wa awali wa miaka kumi kumalizika nyongeza yoyote ya Mkataba au Mkataba mwingine mpya uzingatie Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2004 *(Public Procurement Act, 2004).*

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kimsingi Azimio la Bunge liliipa msukumo mpya kazi ambayo tayari ilikwishaanza kutekelezwa na Kamati ambayo iliundwa na Serikali tarehe 25 Machi, 2008. Mambo muhimu yaliyobainishwa katika Azimio la Bunge yalishaanza kushughulikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Serikali ilianza majadiliano na *TICTS* kwa kuzingatia vipengele vinavyotakiwa kufutwa au kurekebishwa. Aidha, vikao vinne vya majadiliano vilivyoshirikisha pande zote mbili, yaani Kamati ya Serikali ya majadiliano na *TICTS* vilifanyika. Kikao cha mwisho kilifanyika tarehe 24 Oktoba, 2008.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa majadiliano, *TICTS* haikuafiki kubadili vipengele vya mkataba vifuatavyo:-

(i) Ukiritimba wa huduma za makasha *(Exclusivity)*;

(ii) Vigezo vya kupima utendaji *(Performance Indicators);*

(iii) Eneo tengefu *(Designated Area)* ambapo mkataba unataka tarehe 1 Januari, 2009 gati Na. 8 likabidhiwe kwa *TICTS*;

(iv) Kuongeza kiwango cha pango *(Rental Fees)*, mrahaba *(royalty)* na dhamana ya utendaji *(Performance Guarantee);*

(v) Kupunguza muda wa kukodisha *(Lease period)* toka miaka 25 kuwa miaka 10;

Mheshimiwa Spika, hata hivyo *TICTS* imeafiki kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kurudisha vifaa vilivyokwisha muda wake wa matumizi kwa *TPA* na kununua vifaa itakavyohitaji;

(ii) Kulipa fidia kwa vifaa vilivyonyofolewa vipuri;

(iii) Kurekebisha utaratibu wa tozo ya kutumia miundombinu ya bandari *(wharfage)* ili *TPA* wakusanye tozo hiyo kila siku wenyewe badala ya utaratibu wa *TICTS* kukusanya tozo hiyo na kuwasilisha *TPA* kila mwisho wa mwezi.

Pia *TICTS* wamekubali hoja ya kuboresha vigezo vya kupima utendaji *(Performance Indicators)* isipokuwa wamekataa vigezo hivyo kuingizwa katika Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Serikali imeainisha athari zinazoweza kujitokeza kiuchumi na kijamii kwa Taifa katika maeneo ambayo muafaka haukufikiwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza ukiritimba wa kuhudumia meli za Makasha *(exclusivity in handling fully cellular vessels)*

Mheshimiwa Spika, kipengele cha kuendeleza ukiritimba kilichopo kwenye Mkataba kinaipa *TICTS* nguvu ya kuhodhi shughuli za kuhudumia meli za makasha kwenye Bandari ya Dar es Salaam hadi kufikisha Makasha 650,000 *(TEU)* kwa mwaka, wakati uwezo wa juu zaidi wa Kitengo ni kuhudumia makasha 330,000 *(TEU)* kwa mwaka. Kutokana na hali hiyo sio tu kwamba kiwango cha Makasha 650,000 *(TEU)* hakiwezi kufikiwa katika eneo tengefu, bali pia kuendeleza ukiritimba kunazuia Wawekezaji wengine kuja kuwekeza katika kuendeleza shughuli za kuhudumia makasha kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Hali ya msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam inasababisha kupoteza biashara ya ndani na nje ya nchi ambayo inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, wakati ukiritimba huu aliopewa *TICTS* ukiendelea kudumaza uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam, bandari jirani shindani kama vile Mombasa, Walvis Bay, Beira, Maputo, na kadhalika zimeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kuboresha na kupanua miundombinu ya bandari zake. Endapo mwelekeo huu hautabadilika lengo la Serikali la kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa bandari kuu katika eneo hili *(Hub Port)* halitafikiwa, badala yake itageuzwa kuwa bandari ndogo *(feeder port).*

Aidha, kuendeleza ukiritimba hususan kwa hali iliyopo ya mlundikano wa makasha na msongamano wa meli inafanya Bandari ya Dar es salaam kuwa ghali na kuipunguzia uwezo wa kushindana katika soko.

Mheshimiwa Spika, kigezo kimoja cha kupakia na kupakua makasha kwa msemo mwingine bandarini kule wanaita *container moves per crane hour*, kilichopo kwenye mkataba hakitoshelezi kupima ufanisi wa utendaji kazi wa *TICTS*. Kuwepo kwa kigezo kimoja kinamfanya *TPA* kushindwa kupima utendaji na ufanisi wa *TICTS* katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kupima ufanisi wa kumhudimia mteja;

(b) Kupima ufanisi wa matumizi ya *Yard;* na

(c) Kupima ufanisi wa matumizi ya mitambo mingine ya kuhudumia makasha katika *Yard.*

Mheshimiwa Spika, kupunguza muda wa kukodisha: Serikali ilijadiliana na *TICTS* kuhusu kupunguza muda wa ukodishaji kutoka miaka 25 na kuwa miaka 10 kutokana na sababu za uchakavu wa miundombinu muhimu ya Bandari ambayo inahitaji ukarabati mkubwa. Kwa mujibu wa mkataba wa sasa jukumu la ukarabati huu ni jukumu la *TPA*. Hata hivyo, *TPA* haiwezi kumudu jukumu hilo chini ya mkataba uliopo.

Mheshimiwa Spika, ada ya pango na tozo ya mrahaba inayolipwa na *TICTS* hailingani na ongezeko la shehena inayopita kwenye kitengo cha makasha. Majukumu ambayo *TPA* inayo katika utekelezaji wa mkataba ni makubwa mno ukilinganishana mapato. Iwapo hali hii haitarekebishwa, Serikali italazimika kutoa ruzuku kwa ajili ya matengenezo ya kitengo cha makasha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba wa ukodishaji wa kitengo cha makasha, ruhusa ya *TPA* kutumia Gati Na. 8 ilikwisha tarehe 31 Desemba, 2008. *TPA* itakuwa imebaki na Gati moja tu lenye kina kirefu, Gati Na. 7 kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa zinazobeba shehena ya kichele kama vile; mbolea, nafaka, *clinker* na kadhalika. Hali hii itasababisha ucheleweshaji wa kuhudumia meli husika hasa wakati wa msimu wa kilimo na wakati unapotokea upungufu wa chakula nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali imepokea taarifa ya Kamati ya Majadiliano kwa ajili ya maamuzi. Aidha, Wizara ya Miundombinu imepokea ushauri wa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama vile ilivyokuwa imeombwa. Kwa sasa Wizara ya Miundombinu imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili kupata maamuzi ya juu ya Serikali kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sana naomba kuwasilisha! *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa zote hizo mbili. Sasa namwita Mwenyekiti ya Miundombinu naye aweze kuzungumzia taarifa zote mbili; ya *RITES* na ile ya *TICTS*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU (MHE. MOHAMED H. MISSANGA):** Mheshimiwa Spika, naomba kwa ridhaa yako kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge la uendeshaji usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania unaofanywa na kampuni ya *RITES* ya India.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja (11) uliofanyika mwezi Aprili, 2008, Mheshimiwa Said Amour Arfi - Mbunge wa Jimbo la Mpanda Kati, aliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu hoja binafsi iliyohusu uendeshaji usioridhisha wa Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* unaofanywa na Kampuni ya *RITES* ya nchini India.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipokea hoja hiyo na kuazimia kwa kuitaka Serikali kuisimamia Kampuni hiyo kwa kuondoa migogoro ya mara kwa mara kati ya Wafanyakazi na Menejimenti; kuweka uwiano mzuri katika Menejimenti baina ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya *RITES* na kuleta ufanisi mzuri na hatimaye kuwapunguzia na kuwaondolea kero watumiaji wa usafiri wa reli nchini.

Mheshimiwa Spika, hoja za msingi ambazo Serikali kwa kutumia vyombo vyake ilikuwa ni pamoja na kuangalia upya mkataba wa ukodishaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya *RITES* ili kuondoa dosari zote zilizopo kwa maslahi ya Taifa. Kuangalia upya uwiano wa ushiriki katika shughuli za Kiutawala na Menejimenti; pamoja na uwakilishi ndani ya Bodi ya Wakurugenzi ili kupata uwiano ulio sawa kati ya upande wa Serikali ya Tanzania na wakodishaji wa *RITES* licha ya mgawanyo wa hisa, ambapo Tanzania ina hisa asilimia 49 na Kampuni ya *RITES* ina hisa asilimia 51. Kwa kuwa, baadhi ya Stesheni na Magenge ya Shirika la Reli Tanzania yamehujumiwa kwa kung'olewa vifaa mbalimbali *(vandalised)* na mengine kufungwa kabisa, hatua madhubuti zichukuliwe ili kuhakikisha usalama wa reli na vyombo vyake vyote.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* mara baada ya kusainiwa kwa Mkataba wa Ukodishaji wa lililokuwa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* tarehe 1 Oktoba, 2007 na kuanza kufanya kazi zake; Kampuni hii ilikumbwa na matatizo lukuki ambayo baadhi yake mpaka hivi sasa hayajapata ufumbuzi. Matatizo hayo ni pamoja na:-

(i) Kupungua kwa mapato kutokana na *TRL* kutokuwa na mikakati mizuri ya kuwahudumia wateja wadogo wadogo wanaotumia reli hiyo, ambao awali walifikia

asilimia 60. Watumiaji hao wadogo wadogo wa usafiri wa reli walishuka, ambapo sasa wamefikia kiwango cha asilimia 23 tu;

(ii) Menejimenti ya *TRL* kutozingatia baadhi ya vipengele vya Mkataba wa Ukodishaji; kwa mfano:-

Kutotoa taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za mwaka husika; na

Kuchukua maamuzi mazito bila kuishirikisha Serikali kwa kusitisha huduma ya usafiri wa Reli kati ya Ruvu - Tanga - Moshi - Arusha na kudhamiria kung'oa reli ya Kahe - Taveta na kwamba reli ya kutoka Moshi – Arusha na ile ya Kaliua – Mpanda sio *(economical)* na hivyo wanataka kuzirudisha reli hizo mbili *RAHCO*/Serikalini.

(iii) Kumekuwepo na migogoro ya mara kwa mara kati ya Wafanyakazi na Menejimenti ya *TRL* hususan kutotekeleza makubaliano ya kulipa ngonyeza ya Mishahara ya kima cha chini iliyotajwa na kuafikiwa kati yake na *TRAWU*;

*(iv)* *TRL* kutozingatia misingi bora ya biashara na kutokuwa wakweli na wawazi kwenye sera yake ya biashara kwa wateja;

(v) Menejimenti ya *TRL* kujipangia na kujilipa mishahara minono na marupurupu mengi yasiyotozwa kodi yanayohamishiwa nchini kwao India; na

(vi) Kutumia injini ndogo na dhaifu za daraja la 73XX na hivyo kuwa na matumizi makubwa ya mafuta na hivyo kuliongezea Shirika mzigo wa gharama za uendeshaji bila sababu.

Mheshimmiwa Spika, katika majadiliano yetu na Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, Kamati ilibaini kuwa katika Mkataba wa Ukodishaji kuna masharti ambayo mkodishwaji alitakiwa kuyatekeleza. Hivyo Kamati imebaini kuna upungufu kadhaa katika kutimiza masharti hayo kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Mkataba *TRL* ilitakiwa iwe inalipa *Performance Bond* kiasi cha *USD 2.0* milioni kwa miaka mitano ya mwanzo kuanzia tarehe 10 Oktoba, 2008 jambo ambalo *TRL* wameshindwa kuliteleza na hivyo kwenda kinyume na kifunga 4-1(a) cha Mkataba;

Kwa mujibu wa Mkataba, *TRL* ilipaswa kulipa gharama za ukodishaji *(Fixed concession Fee)* ya USD 6.0 milioni kwa mwaka na *variable Fee* ya asilimia tano kwa miaka mitano ya mwanzo. Aidha, malipo ya *Variable Concession Fee* yanatokana na mapato ya uendeshaji *(Gross Revenue)*. Hivyo kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2008 *TRL* ilipaswa kulipa tozo hiyo jambo ambalo hadi sasa halijafanyika na hivyo kukiuka kifungu cha 18-3 (b)(a) cha Mkataba;

Kwa mujibu wa Kifungu na 6-13 (a) (iii)(a), ambacho kinaitaka TRL itumie *TRC Engineering Manual* ya 1962 ambacho kinaelezea nguvu kazi inayohitajika kutumika katika utengenzaji wa njia ya reli, ambayo haitumii mashine (*Manual Maintanance); TRL* wameshindwa kufanya hivyo na moja kwa moja kukiuka kifungu 18-3 (ii)(f) cha Mkataba; na

*TRL* kama Mwajiri, kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi wake na kulazimisha Serikali ya Tanzania kulipa mishahara hiyo kwa niaba ya Kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imechambua na kujadili kwa kina utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na kubaini kuwa:-

(i) Pamoja na kwamba Serikali ya Tanzania ina hisa ya asilimia 49, uongozi wa juu wa *TRL* haushirikishi Mtanzania hata mmoja, bali unashirikisha wageni kutoka India peke yao;

(ii) Hali ya Utendaji wa *TRL* bado hauridhishi na malalamiko bado ni mengi. Hii inasababisha kuwepo kwa hisia kutoka kwa wadau wengi kuwa hakuna jitihada zozote zinazochukuliwa katika kuboresha huduma za reli nchini;

(iii) Kutokana na ufanisi usioridhisha, hali iliyojitokeza ni kuwepo kwa msongamano wa mizigo na makasha *(Containers)* katika bandari ya Dar es Salaam kwa sababu *TRL* wanashindwa kusafirisha mizigo ya ndani ya nchi pamoja na ile inayokwenda nchi jirani. Kwa upande mwingine, kupunguza uhai wa barabara *(life span)* kutokana na kutumika zaidi kusafirishia mizigo kwa magari makubwa yaendayo mikoani na nje ya nchi;

(iv) Kushuka kwa kiwango cha kusafirisha mizigo na kujikita zaidi katika kusafirisha abiria;

(v) *TRL* kutotumia wataalam wazalendo wenye uwezo waliopo katika Karakana ya Morogoro ya kutengeza injini za treni na badala yake kujenga hoja ya kupeleka injini hizo India kwa matengenezo;

(vi) Kufanya manunuzi makubwa bila ya kufuata Sheria na Taratibu za Manunuzi kwa kutotangaza Tenda za Manunuzi na kutoishirikisha Serikali ya Tanzania, ambayo ina hisa ya asilimia 49 na badala yake kuelekeza manunuzi hayo India pekee;

(vii) Mabehewa yaliyoingizwa nchini kutoka India sio mapya, bali ni chakavu na yenye uwezo mdogo. Mabehewa hayo yamepitwa na wakati na kukosa ufanisi unaokusudiwa;

(viii) *TRL* wamewaondoa wafanyakazi katika Stesheni zilizopo kati ya Ruvu – Mnyuzi – Tanga na hivyo kusababisha Stesheni na nyumba zilizopo katika maeneo hayo kubomolewa na vifaa kuibiwa;

(ix) *TRL* wamepunguza kwa kiasi kikubwa magenge yanayotumika kwa ajili ya matengenezo ya Reli na hivyo kuhatarisha usalama wa wananchi; na

(x) Kamati ina wasiwasi kuwa taarifa ya Wizara inaeleza kuwa majadiliano ya kuangalia upya Mkataba wa *TRL* yanaendelea kwa muda mrefu bila ya kutoa muda wa kuhitimisha majadilino hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kujadili na kutafakari kwa kina hali isiyoridhisha ya utendaji wa *TRL*, sanjari na maelezo ya kina yaliyotolewa hapo juu, Kamati ina maoni yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa vipengele vingi vya Mkataba vimekiukwa na Menejimenti ya *TRL* kama ilivyoonyeshwa katika ukurasa wa 3 - 5, Kamati inaitaka Serikali ichukue mara moja hatua ya kutoa notisi ya miezi mitatu ya kurekebisha upungufu wote uliojitokeza. Kinyume na hivyo, Kamati inaitaka Serikali ichukue hatua za kuvunja Mkataba wa Ukodishaji wa *TRL* mara moja na kuanza mkakati mpya wa kumpata mwekezaji mwingine au *RAHCO* kwa niaba ya Serikali iendeshe yenyewe huduma za usafiri wa reli kama ilivyokuwa enzi za *TRC*, ili mradi Serikali inawekeza na kutoa mtaji wa kutosha. *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa mikataba mingi imedhihirika kuwa ni mibovu kama huu wa *TRL*, Kamati inaona kuwa, wakati umefika sasa wa Serikali kuwachukulia hatua wote wale wanaofunga mikataba mibovu ambayo haizingatii maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Naibu Waziri - Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, ambaye aliwasilisha Taarifa ya Serikali kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu. Aidha, natoa shukrani kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu - Mhandisi Bwana Omar A. Chambo pamoja na Wataalam wote wa Wizara na Uongozi wa Bodi na Menejimenti ya *TRL* kwa kuipa Kamati ushirikiano wa hali ya juu katika kujadili hali ya Utendaji wa Shirika la *TRL* pamoja na kutoa ufafanuzi mbalimbali kwa Kamati pale ilipohitajika.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa nafasi ya pekee niwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao mahiri iliyosaidia katika kutoa maoni juu ya uimarishaji wa Shirika letu la *TRL*. Napenda kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Alh. Mohamed Hamis Missanga – Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Paschal Costantine Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joce Martin Masunga, Mheshimiwa Mhandisi Herbet James Mntangi, Mheshimiwa Dr. Gertrude Ibengwa Mongella, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick John Mwanazila, Mheshimiwa Sigsfrid Seleman Ng'itu,

Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Phillemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kumpongeza na kumshukuru Dr. Thomas D. Kashillilah - Katibu wa Bunge kwa kuipa Kamati ushirikiano na nyenzo zote muhimu katika kushughulikia hoja hii. Aidha, napenda pia kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii Bwana James John Warburg na Bibi Justina Mwaja Shauri, kwa kuihudumia Kamati yetu wakati wote, bila kuchoka na kufanikisha kuwasilishwa kwa Taarifa hii leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Nakuomba sasa uendelee kutupa taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Mradi unaofuata, yaani ule wa *TICTS*. Ila nitakuomba tu usirejee tena kuyataja upya majina ya wanakamati kwa sababu ukishawashukuru, basi inatosha.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU (MHE. MOHAMED H. MISSANGA):** Maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu hatua za utekelezaji wa Azimio la Bunge juu ya utendaji usioridhisha wa *Tanzania International Container Terminal Services (TICTS*)

Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kifungu 114 (11) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Hoja binafsi inayohusu Utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *Tanzania Container Terminal Services (TICTS),* iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi -Mbunge wa Mbozi Mashariki. Hoja hiyo iliwasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliomalizika tarehe 25 Aprili, 2008 na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, hoja husika katika Azimio la Bunge zilikuwa ni hizi zifuatazo, ambazo Serikali ilitakiwa kuzifanyia kazi:-

(i) Serikali isitishe nyongeza ya Mkataba na kufanya mapitio ya Mkataba wa awali ili vifungu vya Mkataba huo ambavyo havina manufaa kwa Taifa virekebishwe;

(ii) Baada ya muda wa Mkataba wa awali wa miaka kumi kumalizika nyongeza yoyote ya Mkataba au Mkataba mwingine mpya uzingatie Sheria ya Manunuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha cha Bandari ya Dar es Salaam kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *TICTS* kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* na *International Container Terminal Services (ICTSI)* na Tanzania *International Container Services Ltd (TICTS)* ulitiwa saini tarehe 5 Mei, 2000 (naomba kurudia mwaka 2000) ili utekelezaji wake uwe wa miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Mkataba huu ulifanyika marekebisho yaliyohusisha baadhi ya vipengele katika maeneo yafuatayo:-

(i) Muda wa Mkataba uliongezwa kutoka miaka 10 hadi miaka 25;

(ii) Upanuzi wa eneo tengefu *(designated area)* kwa kuongezewa Gati Na. 8 na Kituo cha Kaskazini cha kuweka mizigo cha Ubungo (Ubungo *ICD*); na

(iii) Ongezeko la ada ya pango kwa awamu kutoka USD 3,080,000 kwa mwaka kama ifuatavyo:-

Kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2006 ada ya pango ni *USD* 5 milioni kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano.

Kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2011 ada ya pango itakuwa U*S*D 6.5 milioni kwa kipindi cha miaka mitano.

Kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2016 mpaka 2025 Oktoba,ada ya pango takuwa *USD* 7 milioni.

*TICTS* kuendeleza ukiritimba wa kuhudumia Meli za Makasha katika Bandari ya Dar es Salaam hadi hapo itakapokuwa na uwezo wa kuhudumia Makasha 650,000 kwa Mwaka.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa *TICTS* kwa Kipindi cha mwanzo hadi kufikia mwaka 2005 ulikuwa ni wakuridhisha licha ya ongezeko la Shehena ya Makasha Bandarini Dar es Salaam. Aidha, kuanzia Mwaka 2006, utendaji ulianza kushuka uliopelekea kuwepo kwa msongamamo wa meli na mlundikano wa makasha katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo tarehe 25 Machi, 2008, Serikali iliunda Tume maalum ya kupitia upya Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha. Kamati hiyo ilijumuisha Wataalamu kutoka Wizara ya Miundombinu Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko, Wizara ya Fedha na Uchumi, Msajili wa Hazina, Mamlaka ya Mapato, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na *Consolidated Holding Corporation.*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi huo yalibainisha kuwepo vipengere vya Mkataba vinavyotakiwa kurekebishwa au kufutwa vinavyohusiana na:-

Ukiritimba wa huduma za Makasha *(Exclusivity);*

Vigezo vya kupima Utendaji *(Performance Indicators);*

Eneo tengefu *(Designated Area)* ambapo Mkataba unataka tarehe 1 Januari, 2009 Gati Na. 8 likabidhiwe kwa *TICTS;*

Kuongeza kiwango cha pango *(Rental Fees),* Mrabaha (*royalty)* na dhana ya Utendaji *(Performance Guarantee);*

Kupunguza muda wa kukodisha *(Lease period)* toka miaka 25 kuwa miaka 10;

*TICTS* kurudisha vifaa vilivyokwisha muda wake wa matumizi kwa *TPA;*

Kuweka kipengele ndani ya Mkataba kinachokataza unyofoaji wa vipuri *(Cannibalization of Equipment)* na kuongeza kifungu kinachotoa adhabu; na

Kurekebisha utaratibu wa ukusanyaji wa tozo ya matumizi ya miundombinu ya Bandari *(Wharfage).*

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuundwa Tume kushughulikia utata wa vipengere vya Mkataba visivyotekelezwa na uongozi wa *TICTS* na kutoafiki mapendekezo ya Tume ya Serikali, Kamati imeridhika kwamba Maazimio ya Bunge lako Tukufu bado hayajatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vipengele ambavyo *TICTS* haijavikubali kufanyiwa marekebisho ni kama ifuatavyo:-

Kuondoa Ukiritimba wa Kuhudumia Meli za Makasha *(exclusivity in handling fully cellular vessels);*

Kuongeza Vigezo vya Utendaji *(Performance indicators);*

Eneo Tengefu (matumizi ya pamoja ya Gati Na. 8);

Kuongeza kiwango cha Malipo ya Pango *(Rental Fee)* na Mrahaba *(Royalty)* na dhamana ya Utendaji *(Performance Guarantee);*

Kupunguza muda wa kipindi cha ukodishaji *(Lease Period)* kubaki miaka kumi (10) ya awali;

*TICTS* kurudisha vifaa vilivyokwisha muda wake wa matumizi kwa *TPA;*

Kuweka kipengele ndani ya mkataba kinachokataza unyofoaji wa vipuri *(Cannibalisation of Equipment)* na kuongeza Kifungu kinachotoa adhabu; na

Kurekebisha utaratibu wa ukusanyaji wa tozo ya matumizi ya miundombinu ya bandari *(Wharfage).*

Mheshimiwa Spika, endapo *TICTS* wataendelea na Mkataba wa Nyongeza wa miaka kumi na tano (15) kwa kuzingatia Mkataba uliopo, Tanzania itaathirika kama ifuatavyo:-

(i) Kipengele cha kuendeleza ukiritimba kilichopo kwenye Mkataba kinaipa *TICTS* nguvu ya kuhodhi shughuli za kuhudumia Meli za Makasha kwenye Bandari ya Dar es Salaam hadi kufikisha Makasha 650,000 *(TEU)* kwa mwaka, wakati uwezo wa juu zaidi wa Kitengo ni kuhudumia makasha 330,000 *(TEU)* kwa Mwaka. Kutokana na hali hiyo, kiwango cha Makasha 650,000 *(TEU)* hakiwezi kufikiwa katika eneo tengefu. Kuendeleza Ukiritimba kunazuia Wawekezaji wengine kuja kuwekeza katika kuendeleza shughuli za kuhudumia Makasha kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

(ii) Utendaji wa *TICTS* umekuwa ukishuka mwaka hadi mwaka. Kigezo kimoja cha kupakia na kupakua Makasha *(container moves per crane hour)* kilichopo kwenye Mkataba kimeshuka kutoka kiwango cha *moves* 23.5 mwaka 2005 hadi 11.7 mwaka 2008. Matokeo ya kushuka kiwango hiki kunachangia kuongeza malundikano wa Makasha na msongamano wa meli bandarini kutokana na kasi ndogo ya kupakua na kupakia Makasha.

(iii) Katika marekebisho ya pili ya Mkataba wa Mwaka 2005, *TICTS* walipewa Gati Na. 8. Kwa mujibu wa Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha Makasha, ruhusa ya *TPA* kutumia Gati Na. 8 ilikwisha tarehe 31 Desemba, 2008. *TPA* itakuwa imebaki na Gati moja tu lenye kina kirefu (Gati Na. 7) kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa zinazobeba Shehena ya Kuchele (mbolea, Nafaka, *Clinker* na kadhalika). Hali hii itasababisha ucheleweshaji wa kuhudumia Meli husika hasa wakati wa msimu wa Kilimo na wakati kunapotokea upungufu wa chakula nchini.

(iv) Kuendelea kuwepo kwa msongamano wa Meli na Mrundikano wa Makasha bandarini.

(v) Kiwango cha pango kinacholipwa na kwa matumizi ya Bandari ni kidogo ikilinganishwa na mapato ya *TICTS*.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba:-

**KWA KUWA** utendaji wa *TICTS* umeshuka ukilinganisha na miaka ya nyuma walipopewa Mkataba huu kwa mara ya kwanza, kwani mwaka 2008 waliweza kufanya *moves* 11.7 kwa saa badala ya *moves* 25, ambazo zinatamkwa katika Mkataba na hivyo kushindwa kutimiza masharti ya Mkataba;

**NA KWA KUWA,** Mkataba unaitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* kutoa *notice* ya kusitisha Mkataba pale wanapobaini kushuka kwa utendaji wa *TICTS* kwa zaidi ya asilimia 50;

**NA KWA KUWA,** *TPA* walishawapa *TICTS notice* ya kusitisha Mkataba kutokana na utendaji duni, kama ilivyoelezwa hapo juu;

**NA KWA KUWA,** utendaji dhaifu wa *TICTS* unasababisha msongamano mkubwa wa meli nje ya Bandari hadi kufikia meli zaidi ya 15 jambo ambalo linasababisha wenye meli kukusudia kuacha kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Aidha, wenye meli wameamua kutoza malipo ya ziada *(Versel Delay Surcharge - VDS)* kutokana na meli zao kukaa bandari ya Dar es Salaam kwa muda mrefu;

**NA KWA KUWA,** *TICTS* wameshindwa kuwekeza kwa maana ya kununua vifaa *(equipment)* vinavyosaidia kurahisisha upakuzi na upakizi wa mkasha katika Kitengo hicho na kulazimika kutumia baadhi ya vifaa vya *TPA*;

**NA KWA KUWA,** hakuna mantiki kwa *TICTS* kung'ang'ania ukiritimba *(exclusivity)*, wakati uwezo wao wa kazi ni mdogo usiofikia malengo yaliyoainishwa katika Mkataba, yaani *moves* 25 kwa saa;

**NA KWA KUWA,** Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali alitamka bayana kuwa nyongeza ya Mkataba wa *TICTS* wa miaka 15 haukufuata taratibu za Sheria ya manunuzi;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali:-

Kuvunja Mkataba wa nyongeza ya miaka 15 wa *TICTS*, ulioongezwa bila kufuata taratibu za Sheria ya Manunuzi; *(Makofi)*

Kuufuta au kurekebisha kipengere cha ukiritimba *(exclusivity)* kwa vile *TICTS* wanafanya kazi chini ya kiwango kulingana na matakwa ya Mkataba;

Kuchukua hatua za kuwapata Wawekezaji *(Investor)* wengine mapema na sio Waendeshaji *(Operators)* kwa kuzingatia kuwa Mkataba wa awali wa *TICTS* unaishia mwaka 2010; na

Wakati mchakato wa kuwapata Wawekezaji wapya unafanyika na hasa kama utachukua muda mrefu, Serikali iwawezeshe Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* wasimamie Kitengo cha Makasha *(Container Terminal)*, kwa kuzingatia kuwa Sheria ya *TPA* inawaruhusu kuwa *Landlord* na pia kuwa *Operators.*

Mheshimiwa Spika, mwisho, sasa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Naibu Waziri -Mheshimiwa Hezekiel Chibulunje, aliyewasilisha Taarifa ya Serikali kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, pia natoa shukrani kwa Katibu Mkuu Mhandisi Ndugu Omar A. Chambo kwa michango na ufafanuzi mbalimbali aliotoa kwa Kamati, pamoja na wataalam wote wa Wizara na Uongozi wa Bodi na Menejimenti ya *TICTS* kwa kuipa

Kamati ushirikiano wa juu, katika kujadili, hali ya Utendaji wa Kampuni ya Tanzania *Internatinal Container Terminal Services (TICTS).*

Mheshimiwa Spika, napenda kwa nafasi ya pekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wote Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango yao mahili iliyosaidia katika kutoa maoni juu ya uimarishaji wa Kampuni ya *Tanzania international Container Terminal Services (TICTS).*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kumpongeza nakumshukuru Dr. Thomas D. Kashillilah, Katibu wa Bunge kwa kuipa Kamati ushirikiano na nyenzo zote muhimu katika kushughulikia hoja hii. Aidha, napenda pia kuwashukuru Makatibu wa Kamati Bwana James John Warburg na Bi. Justina M. Shauri, kwa kuihudumia Kamati wakati wote bila kuchoka na kufanikisha kuwasilisha Taarifa hii leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. KABWE ZUBEIR ZITTO:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE ZUBEIR ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa hizi mbili na kwa mujibu wa maelekezo yake leo asubuhi, nilikuwa naomba taarifa za Serikali na taarifa za Kamati, kwa busara yako uweze kuzipangia muda wa kuzijadili katika Bunge lijalo.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tutahitaji hoja mahsusi ya kufanya hivyo kwa mujibu wa kanuni na hoja hizo zimfikie Katibu si chini ya saa 48 kabla ya Mkutano ujao kama Kanuni inavyosema, lakini ziwe hoja mahususi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niishukuru sana Kamati hii ya Miundombinu inadhihirisha mtazamo sahihi ninaousisitiza mara kwa mara kwamba tuanze kuangalia maslahi ya Taifa, kwa kazi ya pamoja wamefanya vizuri wengine hawapendi kusikia hivyo, lakini shauri yao. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maslahi ya Taifa letu hakuna kingine kinachotangulia, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nimwite tena Waziri wa Miundombinu kwa taarifa ya utekelezaji wa maazimio kuhusu Azimio la Uuzwaji wa nyumba za Serikali.

**Taarifa ya Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Juu ya Uuzwaji wa Nyumba za Serikali**

**MHE. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa 12 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliomalizika Dodoma tarehe 29 Agosti, 2008, niliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Bunge kuhusu uuzaji wa nyumba za Serikali kufuatia hoja ya Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro - Mbunge wa Jimbo la Vunjo aliyoiwasilisha katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Mkutano huo Bunge liliazimia Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Itekeleze mara moja bila kusita agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kurejesha nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu na kwa watu ambao hawakuwa watumishi wa Serikali wakati huo na vilevile nyumba ambazo hazikupaswa kuuzwa kama zile zilizopo kwenye maeneo ya utawala wa Serikali;

(ii) Izirejeshe kwenye umiliki wake nyumba hizo zilizouzwa kinyume cha utaratibu; na

(iii) Itoe orodha ya nyumba zake ambazo ziliuzwa kwa watu ambao si watumishi wa Serikali, kinyume cha utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za watumishi wa Serikali wanaostahili kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yangu ya awali niliyowasilisha kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili, nilieleza kuwa wakati wa utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ilibaini makundi matano ya nyumba za Serikali zilizouzwa kinyume cha utaratibu:-

(a) Nyumba zilizoko kwenye Makambi;
(b) Nyumba zilizouzwa kwa watu binafsi ambao sio watumishi wa umma;

(c) Nyumba zaidi ya moja zilizouzwa kwa familia moja ya watumishi wa umma;

(d) Nyumba za Taasisi mbalimbali zilizouzwa kwa watumishi wa Serikali Kuu; na

(e) Nyumba ambazo ziko katika maeneo nyeti ya Serikali na ambazo ziliuzwa kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, nyumba zipatazo 53 zilizoko katika makambi ziliuzwa kwa makosa. Idadi hii inahusisha nyumba nane zilizoko katika maeneo ya Makambi ya Polisi, nyumba 10 za maeneo ya Magereza na nyumba 35 katika maeneo ya Hospitali (*Kiambatisho* ‘A’).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika taarifa yangu ya awali kuwa, wahusika wote wameandikiwa barua ya kusitisha mikataba na kuwataka wasiziendeleze

zaidi nyumba hizo kwa lengo la kupata thamani halisi zitakazokuwa ndiyo msingi wa kuwalipa fidia. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Mikataba ya nyumba hizo sasa imefutwa. Kufuatia hatua hii mkataba Na. SP 661 wa nyumba Na. GT/CR/RF/53 iliyoko Rufiji Pwani umerejeshwa na mhusika kwa Wakala wa Majengo. Ukaguzi na tathmini ya maendelezo yaliyofanywa kwa nyumba zote umekamilika ambapo kiasi cha Tsh. 222,867,110/= kinahitajika kulipwa kama fidia kwa wahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yangu ya awali nilieleza pia kuwa, wakati wa kutekeleza zoezi la kuuza nyumba za Serikali ilibainika kuwa nyumba nne ziliuzwa kimakosa kwa watu ambao sio watumishi wa Serikali jijini Dar es Salaam baada ya wahusika kutoa taarifa zisizokuwa sahihi. Katika hatua za kurekebisha kasoro hiyo, Serikali ilifuta mikataba yote ya mauzo ya nyumba hizo na nyumba tatu kati ya nne tayari zimerejeshwa kwenye miliki ya Serikali. Aidha, mmiliki wa nyumba Na.UC.8 mwenye mkataba Na.PF.281 (kati ya wamiliki hao watatu) amekwisharejeshewa fedha zake kiasi cha Tshs. 13,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, Mkataba (Na. FP.280) wa nyumba Na. UC 1 & 2 (nyumba ya nne katika kundi hili) iliyopo eneo la Ubungo *Camp* Jijini Dar es Salaam umeendelea kuwa na utata kwa vile baada ya kupewa barua ya kusitisha mkataba mhusika alifungua kesi Mahakama Kuu (Kesi Na.37/2008) kupinga kufutiwa mkataba. Baada ya kushindwa kesi hiyo, ameendelea kukata rufaa Mahakama ya Rufaa, Kitengo cha Ardhi ambapo kesi imepangwa kusikilizwa mwezi wa Machi, 2009, Kiasi cha Tshs.15,500,000/= kinahitajika kuwalipa fidia wahusika Wengine watatu waliobaki (*Kiambatisho* ‘B’).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa kulikuwa na kasoro nyingine iliyojitokeza ama kubainika wakati wa zoezi hili kwamba, baadhi ya familia na watumishi wa umma waliuziwa nyumba zaidi ya moja. Uchunguzi uliofanywa na Serikali ulibaini kuwa, kulikuwa na familia sita na watumishi wanne waliouziwa nyumba zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, utekelezaji wa agizo hili uko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:- (*Kiambatisho ‘C’ );* Familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na. 128 & 129 iliyoko katika maeneo ya Chang’ombe yenye Mkataba Na. 0682 na nyumba Na. 633/11 yenye Mkataba Na. SP 165 imerudisha mkataba wa nyumba mojawapo; nyumba Na.0682 iliyoko katika eneo la Chang’ombe. Hatua hii pamoja na taratibu za kuthamini maendelezo yaliyofanywa zilikamilika tangu tarehe 15 Septemba, 2008 na zinasubiri taratibu za kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, familia iliyokuwa inamiliki nyumba mbili (Na.*MS* 29/58 yenye mkataba Na. SPH 1076 iliyoko Mtaa wa Msimbazi na nyumba *Block* C6 yenye mkataba Na.*TP.TRC* 0558 iliyoko Mtaa wa Ghana/Mirambo), imebakiwa na nyumba moja tu yenye mkataba Na.*TPTRC* 0558 iliyoko makutano ya mitaa ya Ghana na Mirambo. Nyumba yenye Mkataba Na.*SPH* 1076 iliyoko Mtaa wa Msimbazi imetwaliwa kwa manufaa ya Umma (Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Kasi – *DART*).

Mheshimiwa Spika, familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na.B/PL 472/HS 66 ya Mbweni yenye Mkataba Na.SP1014 na nyumba Na.31 yenye Mkataba Na. 0251 iliyoko eneo la Kinondoni *Cottage* ilirudisha nyumba moja yenye Mkataba Na.SP 1014 iliyoko Mbweni kabla ya maagizo ya Bunge na tayari nyumba hiyo, amegawiwa mtumishi mwingine wa umma.

Mheshimiwa Spika, familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na.C/PL358/HS154 yenye mkataba Na. SP 1040 katika eneo la Mbweni Malindi Jijini Dar es Salaam na nyumba Na. GT/CR/KB/49 yenye Mkataba Na. 1768 katika eneo la Mkoani Kibaha, Mkataba wa nyumba moja (Na.1768) umefutwa. Hata hivyo, familia hiyo imefungua shauri Mahakamani na kesi inatarajiwa kusikilizwa tarehe 17 Februari, 2009 Mjini Kibaha katika Baraza la Nyumba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na. GT/CR/4A yenye Mkataba Na. 0260 iliyoko Mtaa wa Mkoani mjini Kibaha Pwani na nyumba Na. 84/34 yenye Mkataba Na. TP.THA.087 katika eneo la Msasani *Estate* jijini Dar es Salaam, (Mkataba Na. TP.THA.087) wa nyumba Na. MS. 84/34 iliyoko Msasani *Estate* Jijini Dar es Salaam ulifutwa mapema hata kabla ya maagizo ya Bunge, Nyumba hiyo alipewa mtumishi mwingine. Hata hivyo, familia iliyofutiwa Mkataba, imefungua kesi katika Mahakama Kuu ya Ardhi. Kesi hiyo, inatarajiwa kusikilizwa tarehe 24 Februari, 2009.

Mheshimiwa Spika, umejitokeza utata kwa upande wa familia zilizokuwa zinamiliki nyumba Na. 36 yenye Mkataba Na.0414 Mtaa wa Ismailia jijini Dar es Salaam na nyumba Na. 516/18 yenye Mkataba Na. SP 1282 Mtaa wa Mkadini Jijini Dar es Salaam, familia hiyo imeleta taarifa ya kuwa wametalikiana na wamewasilisha vielelezo vya talaka vilivyotolewa kisheria. Ufumbuzi wa suala hili utatolewa na Serikali baada ya kujiridhisha na vielelezo vilivyopo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiasi cha Tshs.63,250,000/= kitahitajika kulipa fidia kwa wahusika wote (i – vi).

Mheshimiwa Spika, wakati nawasilisha taarifa ya kutekeleza zoezi la kuwauzia watumishi wa umma nyumba, nilieleza kuwa jumla ya nyumba 27 zisizokuwa za Serikali kuu ziliuzwa kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, nyumba hizo ni pamoja na nyumba 21 za Serikali za mitaa, nyumba mbili za *SIDO*, nyumba mmoja ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na nyumba tatu za Shirika la Nyumba la Taifa. Nyumba hizo ziliuzwa kutokana na kuwa zimekaliwa na watumishi wa Serikali kwa miaka mingi na hivyo kudhaniwa kuwa ni nyumba za Serikali Kuu(*Kiambatisho* ‘D’).

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nyumba tano ambazo zilikuwa mali ya TAMISEMI, tatu za Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na moja ya Mamlaka ya Mapato (*TRA*) zilizopo Jijini Dar es Salaam, Serikali inaangalia uwezekano wa kujenga nyumba

mbadala ambazo zitakabidhiwa kwa Halmashauri husika, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) na Mamlaka ya Mapato (*TRA*). Hatua hii imefikiwa baada ya Serikali kufanya uchambuzi wa kina na kuona kuwa nyumba hizi zimefanyiwa maendelezo makubwa na hivyo gharama ya kufidia itakuwa kubwa kuliko kujenga nyumba mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengine, nyumba za Serikali Kuu zilizo mkabala na nyumba za Serikali za Mitaa zimeuzwa kwa watumishi wa Serikali za Mitaa wakati nyumba za Serikali za Mitaa zimeuzwa kwa watumishi wa Serikali Kuu. Katika hili, Serikali imeona siyo busara kuwanyang'anya watumishi wa *TAMISEMI* na Serikali Kuu nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, watumishi waliouziwa nyumba hizo wamemaliza kuzilipia nyumba tajwa na wote wamefanya maendelezo makubwa ambayo ni ya gharama kubwa kiasi cha kuigharimu Serikali kulipa fidia kubwa. Hivi sasa Wizara imewaandikia Halmashauri husika pamoja na TAMISEMI juu ya mapendekezo ya kuwajengea nyumba mbadala.

Mheshimiwa Spika, kwa nyumba 16 za Halmashauri zilizoko Mikoani pamoja na mbili za *SIDO*, Serikali imefuta mikataba yake na utaratibu wa kuzirudisha kwenye Halmashauri husika pamoja na *SIDO* unafanywa. Vigezo vilivyozingatiwa wakati wa kuamua kufuta mikataba ya nyumba za Mikoani/Halmashauri nje ya Dar es Salaam ni kwamba nyumba nyingi hazijafanyiwa maendelezo makubwa (kwa maana nyingine gharama ya kulipa fidia ni ndogo). Hali kadhalika, nyumba hizo ziko katika maeneo ambayo yanafaa kuendelezwa kwa matumizi ya Serikali kuliko maeneo mengine mapya.

Mheshimiwa Spika, aidha, zoezi la kutathimini maendelezo yaliyofanywa limebaini kuwa kiasi cha Tsh. 799,006,000/= zinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia husika.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yangu ya awali nilieleza pia kuwa zilikuwepo nyumba 35 zilizouzwa katika maeneo nyeti ya Serikali na ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za watumishi wa Serikali wanaostahili kuzitumia (*Kiambatisho* 'E').

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mikataba ya uuzaji wa nyumba hizo imefutwa. Aidha, watumishi waliokuwa na nyumba zenye Na. 15A, 22A, 23A, 24A, 25A, 26A, 27A na 4A karibu na makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu – Dodoma, wamepewa nyumba mbadala katika eneo la Mwangaza - Dodoma na tayari wamehamia kwenye nyumba hizo. Ukaguzi na tathmini ya maendelezao yaliyofanywa kwenye nyumba ambazo mikataba yake imefutwa, umekamilika na kiasi cha Tsh.115,315,300/= zinahitajika kulipa fidia husika. Aidha, mawasiliano yanafanywa kati ya *TBA* na watumishi hawa ili kwa hiari yao, waamue kama wako tayari kukopeshwa nyumba wanazoishi sasa kwa gharama/bei mpya au warudishiwe fedha zao. Iwapo watakataa kuzinunua nyumba hizo kwa bei mpya, basi wataendelea kuishi katika nyumba hizo kwa masharti ya upangaji na kwa mujibu wa stahili zao za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kupitia Azimio Na. 2 la Bunge, Serikali ilitakiwa izirejeshe kwenye miliki yake nyumba zote zilizouzwa kinyume cha utaratibu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Azimio hilo, Serikali imekamilisha tathmini ya maendelezo yaliyofanywa katika nyumba zote na mikataba imefutwa. Kwa nyumba zilizo kwenye makambi, kwa vile wanaoishi humo hadi sasa ni watumishi wa umma wenye stahili ya kupewa nyumba na Serikali, watumishi hao wameandikiwa barua kuwajulisha kuendelea kuishi humo kama wapangaji kwa mujibu wa stahili zao za kiutumishi. Pamoja na hatua hiyo, bado taratibu za kuwarejeshea fedha zao zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 3 liliitaka Serikali itoe orodha ya nyumba zake ambazo ziliuzwa kwa watu ambao si watumishi wa Serikali, kinyume cha utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za watumishi wa Serikali wanaostahili kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika taarifa yangu ya awali, Serikali imeandaa orodha ya nyumba za aina hiyo. Kwa kifupi, orodha hiyo bado haina mabadiliko na ni kama ilivyoainishwa hapa chini:-

(i) Nyumba 53 zilizopo kwenye Makambi ambazo hazikupaswa kuuzwa - Kiambatisho ‘A’;

(ii) Nyumba nne zilizouzwa kwa watu ambao si watumishi wa Serikali - Kiambatisho ‘B’;

(iii) Familia sita na Watumishi wanne waliouziwa nyumba zaidi ya moja - Kiambatisho ‘C’;

(iv) Nyumba 27 za Taasisi mbalimbali zilizouzwa kwa Watumishi wa Serikali - Kiambatisho ‘D’ na

(v) Nyumba 35 zilizouzwa ambazo zipo katika maeneo nyeti ya Serikali - kiambatisho ‘E’.

Mheshimiwa Spika, Azimio Na. 4 la Bunge, liliitaka Serikali ichukue hatua kwa wale ambao hawajalipa na mikataba yao ya kuuziwa nyumba irejewe kuhakikisha kuwa malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao kufutwa na nyumba kurejeshwa kwenye miliki ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yangu ya awali, nilieleza kuwa Serikali ilikuwa inachukua hatua mbalimbali kwa watumishi ambao hawajarejesha mikopo kwa mujibu wa mikataba yao ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuwakumbusha watumishi wote waliouziwa na ambao malipo yao hayaendani na mikataba kwa kutumia Vyombo vya Habari (kama vile magazeti, redio, na luninga);

(ii) Kuwaandikia barua mmoja mmoja za kuwataka walipe malimbikizo yao mara moja;

(iii) Serikali imewahamasisha na kuwashauri watumishi wanaokaribia kustaafu kukopa kwenye Mfuko wa Pensheni za Watumishi wa Umma *(PSPF)* ambao umekubali kutoa huduma hiyo ili kuwawezesha watumishi hao kumaliza mikopo yao ya nyumba kabla ya kustaafu;

(iv) Kwa watumishi wanaostaafu kabla ya kumaliza mikopo yao ya nyumba mfuko wa pensheni za watumishi wa Umma (*PSPF*) hukata salio la deni husika na kuwasilisha Serikalini kupitia Wakala wa Majengo kwa maelekezo ya watumishi wahusika;

(v) Serikali imewashauri watumishi kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa (*SACCOS*) ili kupata mikopo kwa urahisi na nafuu kwa lengo la kurejesha mikopo ya nyumba kwa wakati unaostahili na kwa mujibu wa mkataba; na

(vi) Serikali imewashauri waajiri kuwadhamini watumishi wake waweze kupata mikopo kwenye taasisi za fedha kwa lengo la kurejesha mikopo ya nyumba kwa mujibu wa mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, juhudi hizi ambazo zimeendelezwa na Serikali kupitia Wakala wa Majengo zimezaa matunda. Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2008 hadi Desemba, 2008 Wakala wa Majengo umefanikwa kukusanya kiasi cha Tshs. 2,238,028,812.70 na kufanya makusanyo yote katika kipindi cha miaka mitano hadi Desemba, 2008 kufikia Sh. 40,929,145,047.13 ikiwa ni asilimia 71.7% ya Sh. 57,057,965,241.00 zinazotarajiwa kukusanywa kutokana na mauzo yote ya nyumba katika kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa Azimio hili, Serikali ilikabiliana na changamoto kadhaa:-

Mheshimiwa Spika, nyumba zilizouzwa kwa bei ndogo inayozingatia hali ya nyumba wakati huo, watumishi wamemaliza kulipa na wamefanya maendelezo makubwa. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeamua kukubali kulipa fidia ya soko. Manufaa ya hatua hii ni kwamba Serikali itapata nyumba bora yenye hadhi ya watumishi wa Umma wa ngazi ya juu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watumishi wa umma wamefungua kesi Mahakamani. Katika hili, Serikali imeomba ushauri wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bei ya baadhi ya nyumba ni ndogo kuliko gharama ya fidia. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeamua kuzirejesha nyumba zile tu ambazo Bunge limeelekeza zirejeshwe kwa gharama yoyote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi la kuuza nyumba za Serikali yalikuwa mengi na yameonekana katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Hatua za kurekebisha kasoro hizo zinahitaji umakini wa hali ya juu

maana suala zima ni la kisheria kwa maana ya mikataba iliyopo ambayo Serikali (kupitia *TBA*) imeingia na Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, ukizingatia thamani za nyumba hizi baada ya maendelezo utaona kuwa fedha kwa ajili ya kukamilisha zoezi hili kwa ufanisi bila kuleta migogoro, ni nyingi ambazo haziwezi kupatikana kwa mara moja kwa vile hazikutengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathimini iliyofanywa, jumla ya Tshs. 1,216,118,410/= zinahitajika kwa ajili ya kuwafidia watumishi wa umma waliofutiwa mikataba yao na ambao wamefanya maendelezo katika nyumba walizokuwa wamenunua. Mchanganuo wa fidia husika ni kama ifuatavyo:-

(i) Nyumba zilizouzwa ambazo ziko maeneo ya Polisi, Magereza na Hospitali ni Tshs.222,867,110/=;

(ii) Waliouziwa ambao hawakuwa watumishi wa kudumu Serikalini Tshs.15,500,000/=;

(iii) Watumishi waliouziwa zaidi ya nyumba moja na ambao wamenyang’anywa nyumba ya ziada Tshs.63,250,000/=;

(iv) Watumishi waliouziwa nyumba za TAMISEMI na Taasisi ambazo zinatakiwa kurejeshwa au kujengwa nyumba mbadala Tshs.799,006,000/=; na

(v) Nyumba zilizouzwa ambazo ziko maeneo nyeti ya Serikali Tshs.115,495,300/=.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti katika mwaka huu wa fedha (2008/2009) na kuepukana na athari zinazoweza kutokea, Wizara ya Miundombinu imeazimia kutenga fedha katika Bajeti yake ya mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya kutekeleza maazimio ya Bunge ili zoezi hili likamilike mapema iwezekanavyo na kupunguza usumbufu kwa watumishi na wadau wengineo ambao kwa namna moja au nyingine wameathirika na mapungufu yaliyotokana na zoezi la kuuza nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa, kwa kutambua nia njema ya Serikali ya kuboresha mazingira ya kufanyia kazi nyumba na makazi bora ikiwa ni mojawapo kwa mtumishi wa umma, Wizara yangu imeendelea kujenga nyumba kwa ajili ya kuwapangisha na kuwakopesha watumishi wa umma wakiwemo watumishi wa Halmashauri (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, tangu zoezi la kuwakopesha watumishi wa umma nyumba, Wizara kupitia Wakala wa Majengo imefanikiwa kujenga jumla ya nyumba 990. Idadi hii ni ndogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya nyumba kwa Watumishi wa umma ambao idadi yao inakisiwa kufikia watumishi 300,000.

Kwa kutambua hili na kwa kuzingatia mabadiliko ya hivi karibuni katika sekta ya nyumba *(Mortgage Finance Act)*, Wizara yangu imeanza mikakati ya kuhakikisha inaongeza kasi hiyo maradufu. Moja ya mikakati hiyo ni kupata viwanja vingi pamoja na kuangalia uwezekano wa *TBA* kunufaika na sheria ya "*Mortgage Finance*" iliyopitishwa hivi karibuni. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara kupitia *TBA* ina mpango wa kupata viwanja 500 Dar es Salaam, viwanja 500 Dodoma na viwanja 2,000 katika Mikoa mingine ya Tanzania Bara. Viwanja hivi vyote vitatumika kuwajengea nyumba Watumishi wa Umma, kwa maana nyingine zoezi hili ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itaendelea kuzitambua nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu hadi hapo itakapojiridhisha kuwa, hakuna nyumba nyingine tena za aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK MWANANZILA – (k.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (11) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Azimio la Bunge juu ya uuzwaji wa nyumba za Serikali kufuatia Hoja binafsi ya Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro aliyoiwasilisha katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea hoja ya Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro na kuijadili, Bunge liliazimia kwa kuitaka Serikali ifanye yafuatayo:-

Moja, itekeleze mara moja bila kusita agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kurejesha nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu na kwa watu ambao hawakuwa watumishi wa Serikali. Vile vile nyumba ambazo hazikupaswa kuuzwa kama zile zilizopo kwenye maeneo ya utawala wa Serikali.

Pili, nyumba hizo zote zirejeshwe kwenye umiliki wa Serikali.

Tatu, Wakala wa Majengo ya Serikali *(TBA)* itoe orodha ya nyumba zote ambazo ziliuzwa kwa watu ambao sio watumishi wa Serikali kinyume cha utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za Watumishi wa Serikali waonastahili kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilibainika kuwa kuna makundi matano ya nyumba za Serikali zilizouzwa kinyume cha utaratibu. Makundi hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Nyumba zilizoko kwenye Makambi;

(ii) Nyumba zilizouzwa kwa watu binafsi ambao sio watumishi wa Serikali na wala sio watumishi wa Umma;

(iii) Nyumba zaidi ya moja zilizouzwa kwa familia moja ya watumishi wa umma;

(iv) Nyumba za Taasisi mbalimbali zilizouzwa kwa Watumishi wa Serikali Kuu; na

(v) Nyumba ambazo ziko katika maeneo nyeti ya Serikali na ambazo ziliuzwa kwa Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, nyumba zipatao 53 zilizokuwa katika makambi ziliuzwa kwa makosa. Idadi hii inahusisha nyumba nane zilizoko katika maeneo ya Makambi ya Polisi, Nyumba 10 za maeneo ya Magereza na nyumba 35 katika maeneo ya Hospitali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa katika utekelezaji wa zoezi hili, wahusika wote wameandikiwa barua ya kusitisha mikataba na kuwataka wasiziendeleze zaidi nyumba hizo kwa lengo la kupata thamani halisi zitakazokuwa ndiyo msingi wa kuwalipa fidia. Mikataba ya nyumba hizo sasa imefutwa. Hata hivyo, hadi sasa ni mkataba mmoja Na.SP 661 wa nyumba na GT/CR/RF/53 iliyoko Rufiji Pwani ambao umerejeshwa na mhusika kwa Wakala wa Majengo. Ukaguzi na tathmini ya maendelezo yaliyofanywa kwa nyumba zote umekamilika ambapo kiasi cha Tshs. 222,867,110.00 kinahitajika kulipwa kama fidia kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, wakati wa kutekeleza zoezi la uuzaji nyumba za Serikali; iligundulika kuwa nyumba nne ziliuzwa kimakosa kwa watu ambao sio Watumishi wa Serikali jijini Dar es Salaam baada ya wahusika hao kutoa taarifa zisizokuwa sahihi. Katika hatua za kurekebisha kasoro hiyo, Serikali ilifuta mikataba yote ya mauzo ya nyumba hizo na nyumba tatu kati ya nne tayari zimerejeshwa kwenye miliki ya Serikali. Aidha, kati ya wamiliki hao watatu mmiliki wa nyumba na *UC 8* mwenye mkataba Na. PF 281 amekwisha rejeshewa fedha zake kiasi cha Tshs. 13,000,000/=.

Hata hivyo Mkataba na FP 280 wa nyumba Na UC 1 & 2 iliyopo eneo la *Ubungo Camp* Jijini Dar es Salaam, umeendelea kuwa na utata kwa vile baada ya kupewa barua ya kusitisha Mkataba mhusika alifungua kesi Mahakama Kuu (Kesi Na. 37/2008) kupinga kufutiwa mkataba. Baada ya kushindwa kesi hiyo, ameendelea kukata rufaa Mahakama ya Rufaa, Kitengo cha Ardhi ambapo kesi imepangwa kusikilizwa Machi, 2009 mbele ya Mheshimiwa Jaji Ngwada. Kiasi cha Tshs.15,500,000.00 kinahitajika kuwalipa fidia wahusika wengine watatu waliobaki.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza zoezi la kutathmini uuzaji wa nyumba za Serikali kulijitokeza pia kasoro ambazo baadhi ya familia na Watumishi wa Umma waliuziwa nyumba zaidi ya moja. Uchunguzi uliofanywa na Serikali ulibaini kuwa, kulikuwa na familia sita na watumishi wanne waliouziwa nyumba zaidi ya moja.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa hebu subiri kidogo. Kwa kuwa kwa kiasi kikubwa kamati sasa yale yaliyokwishasemwa na Waziri ningeomba sasa uache sehemu hiyo uende kwenye mapendekezo ya Kamati. *(Makofi)*

Hivi sasa, utekelezaji wa agizo hili uko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na. 128 & 129 iliyoko katika maeneo ya Chang'ombe yenye Mkataba Na. 0682 na nyumba Na. 633/11 yenye Mkataba Na. SP 165 imerudisha Mkataba wa nyumba mojawapo, ambayo ni nyumba Na. 0682 iliyoko katika eneo la Chang'ombe. Hatua hii pamoja na taratibu za kutathmini maendelezo yaliyofanywa zilikamilika tangu tarehe 15 Februari, 2008 na zinasubiri taratibu za kulipa fidia.

(ii) Familia iliyokuwa inamiliki nyumba mbili (Na. MS 29/58 yenye Mkataba na SPH 1076 iliyoko Mtaa wa Msimbazi na nyumba Block C 6 yenye Mkataba Na. TP.TRC 0558 iliyoko Mtaa wa Ghana/Mirambo), imebakiwa na nyumba moja tu yenye Mkataba Na. TPTRC 0558 iliyoko makutano ya Mitaa ya Ghana na Mirambo. Nyumba yenye mkataba Na. SPH 1076 iliyoko Mtaa wa Msimbazi imetwaliwa kwa manufaa ya Umma (Mradi wa Mabasi yaendayo kwa Kasi – *DART*).

(iii) Familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na. B/PL 472/HS66 ya Mbweni yenye Mkataba Na. SP1014 na nyumba Na.31 yenye Mkataba Na. 0251 iliyoko eneo la *Kinondoni Cottage* ilirudisha nyumba moja, yenye Mkataba Na. SP 1014 iliyoko Mbweni kabla ya maagizo ya Bunge na tayari nyumba hiyo, amegawiwa Mtumishi mwingine wa Umma.

(iv) Familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na. C/PL358/HS154 yenye Mkataba Na. SP. 1040 katika eneo la Mbweni Mlindi Jujini Dar es Salaam na nyumba Na. GT/CR/KB/49 yenye Mkataba Na. 1768 katika eneo la Mkoani Kibaha, Mkataba wa nyumba moja (Na.1768) umefutwa. Hata hivyo, Familia hiyo imefungua shauri Mahakamani na kesi inatarajiwa kusikilizwa tarehe 17 Februari, 2009 mjini Kibaha katika Baraza la Nyumba.

(v) Kuhusu familia iliyokuwa inamiliki nyumba Na GT/CR/4A yenye Mkataba Na. 0260 illiyoko Mtaa wa Mkoani Mjini Kibaha, Pwani na Nyumba Na. 84/34 yenye Mkataba Na. TP.THA.087 katika eneo la *Msasani Estate* Jijini Dar es Salaam, (Mkataba Na.TP.THA.087) wa nyumba Na. Ms 84/34 iliyoko *Msasani Estate* Jijini Dar es Salaam ulifutwa mapema hata kabla ya maagizo ya Bunge. Nyumba hiyo alipewa Mtumishi mwingine. Hata hivyo, familia iliyofutiwa Mkataba imefungua kesi katika Mahakama Kuu ya Ardhi. Kesi hiyo inatarajiwa kusikilizwa tarehe 24 Februari, 2009.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi hili umejitokeza utata kwa upande wa famili zilizokuwa zinamiliki nyumba Na. 36 yenye mkataba Na. 0414 Mtaa wa Isamilia Jijini Dar es Salaam na nyumba Na. 516/18 yenye mkataba Na SP 1282 Mtaa wa Mkadini Jijini Dar es Salaam, familia hiyo imeleta taarifa ya kuwa wametalikiana na

wamewasilisha vielelezo vya talaka vilivyotwa kisheria. Ufumbuzi wa suala hili utatolewa na Wizara baada ya kujiridhisha na vielelezo vilivyopo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, kiasi cha Tshs. 63,250,000/= kitahitajika kulipa fidia kwa wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa jumla ya nyumba 27 zilizokuwa za Serikali Kuu ziliuzwa kwa Watumishi wa Umma. Nyumba hizo ni pamoja na nyumba 21 za Serikali za Mitaa, nyumba mbili za SIDO, nyumba moja ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na nyumba tatu za Shirika la Nyumba la Taifa. Nyumba hizo ziliuzwa kutokana na kuwa zimekaliwa na Watumishi wa Serikali kwa miaka mingi na hivyo kudhaniwa kuwa ni nyumba za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nyumba tano ambazo zilikuwa mali ya TAMISEMI, tatu za Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* na moja ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* zilizopo Jijini Dar es Salaam, Serikali inaangalia uwezekano wa kujenga nyumba mbadala ambazo zitakabidhiwa kwa Halmashauri husika, Shirika la Nyumba la Taifa na *TRA*. Aidha, Wizara imewaandikia Halmashauri zilizoko Mikoani pamoja na mbili za SIDO, Serikali imefuta mikataba yake na utaratibu wa kuzirudisha kwenye Halmashauri husika pamoja na SIDO unafanywa. Aidha, zoezi la kutathimini maendelezo yaliyofanywa limebaini kuwa kiasi cha Tshs. 799,006,000/= zinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, zilikuwepo nyumba 35 zilizouzwa katika maeneo nyeti ya Serikali na ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za Watumishi wa Serikali wanaostahili kuzitumia. Aidha, hivi sasa mikataba ya uuzaji wa nyumba hizo imefutwa. Watumishi waliokuwa na nyumba zenye Na. 15A, 22A, 23A, 24A, 25A 26A, 27A na 4A karibu na makazi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu – Dodoma wamepewa nyumba mbadala katika eneo la Mwangaza – Dodoma na wamekwishahamia kwenye nyumba hizo. Ukaguzi na tathmini ya maendelezo yaliyofanywa kwenye nyumba ambazo mikataba imefuta, umekamilika na kiasi cha Tshs.115,315,300.00 zinahitajika kuwalipa wahusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Azimio Na. 2 la Bunge, utekelezaji wa Azimio hilo ni kwamba, Serikali imekamilisha tathmini ya maendelezo yaliyofanywa katika nyumba zote na mikataba imefutwa. Kwa nyumba zilizo kwenye makambi, kwa vile wanaoishi humo hadi sasa ni Watumishi wa Umma, Watumishi hao wameandikiwa barua kuwajulisha kuendelea kuishi humo kama wapangaji kwa mujibu wa stahili zao za kiutumishi, wakati taratibu za kuwarejeshea fedha zao zinaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Azimio linaloitaka Serikali ichukue hatua kwa wale ambao hawajalipa na mikataba yao ya kuuziwa nyumba irejewe kuhakikisha kuwa malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao kufutwa na nyumba kureshwa katika miliki ya Serikali. Serikali imechukuwa hatua zifuatazo:-

(i) Kuwaandikia barua mmoja mmoja za kuwataka walipe malimbikizo yao mara moja;

(ii) Serikali imewahamasisha na kuwashauri Watumishi wanaokaribia kustaafu kukopa kwenye Mfuko wa Pensheni za Watumishi wa Umma *(PSPF)*, ambao umekubali kutoa huduma hiyo ili kuwawezesha Watumishi hao kumaliza mikopo yao ya nyumba kabla ya kustaafu.

(iii) Serikali imewashauri Watumishi kujiunga na vyama vya kuweka na kukopa *(SACCOS)* ili kupata mikopo kwa urahisi na nafuu kwa lengo la kurejesha mikopo ya nyumba kwa wakati unaostahili na kwa mujibu wa mkataba;

(iv) Serikali imewashauri Waajiri kuwadhamini Watumishi wake, waweze kupata mikopo kwenye taasisi za fedha kwa lengo la kurejesha mikopo ya nyumba kwa mujibu wa mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali kupitia Wakala wa Majengo Tanzana, katika kipindi cha mwezi Agosti, 2008 hadi Desemba, 2008 imefanikiwa kukusanya kiasi cha Tsh. 2,238,028,812.70 na kufanya makusanyo yote (katika kipindi cha miaka mitano hadi Desemba, 2008), kufikia Sh. 40,929,145,045,047.13 ikiwa ni sehemu ya Sh. 57,057,965,241/= zinazotarajiwa kukusanywa kutokana na mauzo ya nyumba katika kipindi cha mika kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa busara zako naomba niende kwenye hatua ya maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imepokea taarifa ya utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu zoezi la uuzwaji wa nyumba za Serikali na kuridhika na zoezi hilo kuwa limetekelezwa kwa ukamilifu unao fikia zaidi ya asilimia themanini (80%) . Pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

Moja, awali ya yote Kamati imeipongeza Wizara na Wakala wa Majengo Tanzania kwa kazi nzuri iliyofanya kwa kuwajengea na kuwauzia nyumba Watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mbili, Kamati inashauri kuwa, katika kutekeleza zoezi la kurejesha nyumba kwenye umiliki wa Serikali, fedha zitakazotumika kulipia fidia zitokane na Bajeti ya Wizara kwa kuombwa kutoka Serikalini.

Tatu, Serikali iachane na utaratibu wa kuuza nyumba za Serikali zilizopo na badala yake ijenge nyumba na kuwauzia au kuwapangisha Watumishi wa Serikali.

Nne, Kamati imebaini kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika zoezi hili, bado zipo nyumba za Serikali ambazo hazijaratibiwa na kuingizwa katika zoezi hili hasa kutoka Mikoani maana nyumba zilizoratibiwa nyingi ni za Dar es Salaam, Tanga na Miji michache. Lakini nyingi katika Mikoa mingine bado hazijaratibiwa. Kamati imeshauri Wizara na Wakala wa Majengo Tanzania kuendeleza zoezi hili ili kupata uhakika wa umiliki wa nyumba zote zilizo chini ya himaya ya Serikali.

Tano, wakala uendelee kufuatilia  Watumishi wote ambao hawajamaliza mikopo yao na kuwachukulia hatua za kisheria pale inapobidi.

Sita, vipengere vya mikataba ya mauziano vifanyiwe mapitio na marekebisho ya mara kwa mara ili kuondoa mianya ya wakopaji kuipeleka  Serikali Mahakamani mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Waziri Dr. Shukuru J. Kawamba na Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Katibu Mkuu - Ndugu Omar A. Chambo pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umakini mkubwa wa kupitia na kujadili taarifa hii ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa busara zako, kwa sababu wajumbe walitajwa na Mheshimiwa Mohamed Missanga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, naomba nisirudie ila naomba niseme kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwananzila kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Shughuli ya  tano sasa, Katibu.

## HOJA ZA KAMATI

**MHE. MUSA ZUNGU AZZAN – K.n.y MHE. WILSON M. MASILINGI- MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na pia namshukuru Katibu wa Bunge kwa msaada aliotupa. Moja kwa moja kabla ya Azimio ningeomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati ambao walioshughulikia Azimio hili. Naomba kumtambua Mheshimiwa Wilson Masilingi ambaye ndiyo Mwenyekiti wa Kamati.  Naomba kumtambua Musa Azzan Zungu - Makamu Mwenyekiti, naomba kumtambua Mheshimiwa Kanali Saleh Farah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ali

Ameir Mohamed, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Thomas Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud Abdallah, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Magale John Shibuda, Mheshimiwa Mohamed Sanya, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, pamoja na Katibu wa Bunge - Ndugu Athumani Hussein.

**SPIKA:** Katibu wa Kamati siyo Katibu wa Bunge.

**MHE. MUSA ZUNGU AZZAN – k.n.y MHE. WILSON M. MASILINGI- MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Katibu wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa azimio la Bunge la mwaka 2009 ambalo linadai mauaji ya Albino nchini Tanzania.

**KWA KUWA**, katika siku za karibuni nchini Tanzania kumejitokeza wimbi la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, yaani Albino, kutokana na imani za kishirikina;

**NA KWA KUWA,** vyombo vya habari vimejitahidi kutoa taarifa za mauaji hayo ya kikatili na kinyama yanayotokea karibu kila sehemu ya nchi yetu;

**NA KWA KUWA,** vitendo vya ubaguzi, unyanyasaji na mauaji ya kinyama ya Albino vimekuwa ni tatizo kubwa na ilisilovumilika nchini Tanzania;

**NA KWA KUWA,** katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria husuan Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara na Tabora Albino wengi wameuawa na wengine wamenyofolewa baadhi ya viungo vyao vya mwili;

**NA KWA KUWA** katika Mikoa hiyo kuna taarifa zinaoonyesha kuwa, kuna ongezeko hata makaburi yanayozikwa Albino hufufuliwa, kwa lengo la kunyofoa baadhi ya viungo vya maiti za Albino waliozikwa;

**NA KWA KUWA,** mauaji hayo yamechochewa kwa kiasi kikubwa na baadhi ya waganga wa kienyeji ambao, kutokana na imani za kishirikina wanawapa wateja wao ushauri potofu kwamba viungo vya Albino vinapotumika katika shughuli za uchimbaji wa madini na uvuvi vinaweza kumtajirisha mtu kwa haraka sana;

**NA KWA KUWA,** mauaji hayo ya kinyama yamesababisha hofu kubwa kwa jamii ya Albino hapa nchini, ambapo kwa sasa hawana amani mioyoni mwao na pia hawana tena uhakika wa usalama wao na wanaogopa hata kukaa mahali, kutembelea au kusafiri mmoja mmoja kwa kuhofia hatarini inayoweza kuwakabili;

**NA KWA KUWA,** mauaji hayo ya kinyama yanapoteza maisha ya raia wa nchi hii wasio na hatia na pia yanaitia aibu kubwa nchini yetu mbele ya macho ya jamii ya Kimataifa;

**NA KWA KUWA,** mauaji hayo ni uvunjaji na ukiukaji wa Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za makundi madogo katika jamii *(The United Nation Declaration on the Rights of Minorities)*, na pia Mkataba wa Baraza la Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Makundi ya watu kwenye Jamii, *(The African Charter on Human and Peoples);*

**NA KWA KUWA,** kwa mujibu wa Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Albino kama watu wengine katika jamii ya Watanzania, wanayo haki ya msingi ya kuishi na kupata kutoka katika jamii, hifadhi ya maisha yao, kwa mujibu wa sheria; *(Makofi)*

**NA KWA KUWA,** Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alikwishatangaza msako wa kuwakamata na kuwafikisha mbele ya vyombo vya utoaji haki na sheria, wale wote wanaojihusisha kwa njia moja ama nyingine, katika mauaji ya Albino.

**NA KWA KUWA,** Jeshi letu la Polisi, kwa kutambua kwamba, suala la kuzuia na kufuatilia mbali vitendo vya kijinai vinavyohusu mauaji ya Albino nchini lina umuhimu wa kipekee, limechukua hatua za haraka za kuendesha operesheni za kuwasaka wahalifu wanaojihusisha na mauaji hayo;

**NA KWA KUWA**, tatizo la mauaji ya Albino nchini ni mtambuka na linahitaji kuwashirikisha wadau wote kwenye jamii ya Watanzania ili kufanikisha juhudi za kupambana na uhalifu huo;

**NA KWA KUWA,** kwa kutambua hilo Jeshi la Polisi nchini, kwa kutumia dhana ya ulinzi shirikishi, wamefanikiwa kuwakamata watu wanaohusika na mauaji ya Albino na kuwafikisha kwenye vyombo vya utoaji haki;

**NA KWA KUWA,** hatua mbalimbali zimechukuliwa na Serikali pamoja na vyombo vyake vyote vinavyohusika, katika kuhakikisha usalama wa Albino nchini;

**NA KWA KUWA,** Wabunge wakiwa ndio sauti ya wananchi, wamechukizwa na wamesononeshwa sana na pia Bunge likiwa ndicho chombo cha uwakilishi wa wananchi, limeguswa sana na mauaji ya Albino nchini na linataka kuona kwamba uhalifu huo unatokomozwe mara moja nchini mwetu*; (Makofi)*

**KWA HIYO BASI,** Bunge hili la Kumi na Nne linaazimia kwamba:-

(1) Linalaani kwa nguvu zote, mauaji ya Albino yanayofanyika nchini kutokana na imani za kishirikina; *(Makofi)*

(2) Linawapongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kauli zao walizozitoa kwa nyakati mbalimbali, kulaani mauaji ya Albino nchini; *(Makofi)*

(3) Linatambua na kupongeza jitihada za Serikali katika kutetea na kulinda haki za kuishi na pia katika kutoa hifadhi ya maisha ya raia wote wa nchi hii, ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu wa ngozi – Albino. *(Makofi)*

(4) Linaipongeza Serikali na Jamii ya Watanzania, kwa juhudi kubwa wanazozifanya kukabiliana na mauaji hayo;

(5) Linatoa wito kwa Jeshi la Polisi kuongeza kasi katika uchunguzi wa watuhumiwa wa mauaji ya Albino na kuwafikisha Mahakamani ili sheria iweze kuchukua mkondo wake; *(Makofi)*

(6) Linatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama, hususan Polisi, chini ya dhana ya ulinzi shirikishi, katika juhudi zinazofanywa na Serikali yetu kukomesha mauaji ya Albino nchini, kwa kujitokeza na kuwataja wanaoshukiwa kuhusika na mauaji hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kulaani Mauaji ya Albino Nchini Tanzania)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Katibu kwa hatua inayofuata na kwa sababu sina hakika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inaweza kuchukua muda gani, basi namwomba kwa mujibu wa kanuni ya 28(3) Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu atoe hoja ya Bunge kuendelea na shughuli zake hadi Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapomaliza hotuba yake.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa kutumia masharti ya kanuni ya 28 naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liendelee hadi Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokamilisha hoja yake jioni hii ya kuahirisha Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Kutengua Kanuni za Bunge)*

Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningependa Waheshimiwa Wabunge tutambue uwepo pale kwenye *Speakers Galley* wa mama Tunu Pinda na wadogo zake wawili. Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwenye Rehema nyingi na kutuwezesha kumaliza mwaka 2008 na kuanza mwaka 2009 Salama. Binafsi nawatakia nyote Waheshimiwa Wabunge, kheri na fanaka za mwaka mpya wa 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, nachukua nafasi hii tena na kwa niaba ya Serikali, kutoa rambirambi kwako wewe, kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba wa aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Richard Nyaulawa aliyefariki dunia mwezi Novemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Januari, 2009, kulifanyika Uchaguzi Mdogo kule Mbeya Vijijini ambapo Wananchi wa Jimbo hilo waliweza kumchagua Mbunge wao. Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Richard Nyaulawa. Tunamkaribisha hapa Bungeni na kumuahidi ushirikiano ili aweze kutekeleza majukumu yaliyo mbele yake kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Lakini vile vile napenda kuwapongeza vyama vilivyoshiriki katika kinyang'anyilo hicho kwa kuimarisha demokrasi kwa kukubali ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Sophia Mnyambi Simba kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi Tanzania – *UWT* (CCM). Vilevile, nawapongeza viongozi wote wa Jumuiya mbalimbali za Vyama vyote vya Siasa nchini kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika vyama vyao. Wote nawatakia kazi njema katika kulijenga Taifa letu. *(Makofi)*

Nichukue fursa hii pia kumpongeza Dr. Thomas Kashililah kwa Kuteuliwa kwake kuwa Katibu wa Bunge. Uteuzi wake utaongeza Kasi na Viwango katika utendaji wa shughuli za kila siku za Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hapa nilipokuja leo asubuhi nikakuta hotuba yangu imeshachapishwa kwenye kitabu leo asubuhi kwa kweli nilifarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 Januari, 2008, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja

wa Afrika na tarehe 3 Februari, 2009. Mheshimiwa Rais alimaliza kipindi chake na kukabidhi rasmi Uongozi huo kwa Mheshimiwa Kanali Muammar Gaddafi - Rais wa Libya. Nitumie fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuongoza Umoja huu kwa ufanisi, umahiri na mafanikio makubwa. Sisi sote ni mashahidi kuwa katika kipindi cha Uenyekiti wake, Umoja wa Afrika umeweza kupiga hatua kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama, uchumi na siasa, masuala ya jamii na utamaduni na kuimarisha Maslahi ya Wafanyakazi wa Umoja wa Afrika na Taasisi zake. Vile vile, katika kipindi chake cha Uenyekiti, sote tumeshuhudia alivyosimamia usuluhishi wa migogoro kwenye nchi mbalimbali na hasa zile za Kenya, Zimbabwe, Comoro, Burundi na kwingineko. *(Makofi)*

Vilevile, nampongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ya kukabidhi Uenyekiti kwa Mheshimiwa Rais wa Libya. Uzuri wa hotuba hiyo siyo tu kuwa ilikuwa imesheheni masuala mazito yanayolikabili Bara la Afrika, lakini aliitoa kwa Lugha ya Kiswahili. Lugha hii ni kubwa kwa sasa na inaanza kupanda kwa kasi kubwa sana katika njanya za kimataifa. Hongera Mheshimiwa Rais kwa kukipandisha Kiswahili chati Kimataifa**.** Changamoto iliyopo ni kwa Viongozi wengine na Watanzania wote kuendeleza kazi hii nzuri. Kukua kwa lugha ya Kiswahili sio tu kutaitangaza nchi yetu, lakini vilevile itatoa ajira kwa walimu wa Kiswahili na wataalam wa kutafsiri. Naomba tuitumie fursa hii vizuri ili Watanzania wengi wapate ajira katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha shughuli za Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu. Katika Mkutano huu, jumla ya Maswali 162 yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mengine mengi ya nyongeza. Serikali kupitia Mawaziri iliweza kujibu maswali yote kwa ufasaha na kwa umakini wa hali ya juu. Vilevile, katika Mkutano huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliulizwa Maswali 17 na mengine saba ya nyongeza kupitia utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo. Nimeambiwa nilijitahidi kujibu kwa umahiri mkubwa sana. Nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliopata nafasi ya kuuliza Maswali. Kupitia Maswali yenu, wananchi tunaowawakilisha wameweza kupata ufahamu wa masuala mbalimbali na msimamo wa Serikali kwa mambo mengi yanayogusa mustakabali wa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya Miswada saba imesomwa na kujadiliwa. Miswada hiyo ni:-

(i) Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii wa Mwaka 2008 *[The Public Health Bill 2008]*;

(ii) Muswada wa Sheria ya Viwango wa Mwaka 2008 *[The Standards Bill, 2008];*

(iii) Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho kwenye Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2008 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Bill, 2008];*

(iv) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania wa Mwaka 2008 *[The Tanzania Trade Development Authority Bill, 2008];*

(v) Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008 *[The Wildlife Conservation Bill, 2008];*

(vi) Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2008 *[The Political Parties (Amendment) Bill, 2008];* na

(vii) Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makadirio ya Nyongeza ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 *[The Supplimentary Appropriation For Financial Year 2008/2009, Bill, 2009].*

Mheshimiwa Spika, vilevile, wakati wa Mkutano huu, Miswada ifuatayo ilisomwa kwa Mara ya Kwanza:-

(i) Muswada wa Sheria *DNA* ya Binadamu wa Mwaka 2008 *[The Human DNA Regulation Act, 2008];*

(ii) Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008 *[The Fertilizer Act 2008]*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilijadili na kuridhia Maazimio yafuatayo:-

(i) Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki; *[Protocol on the Establishment of the East African Science and Technology Commission];*

(ii) Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu kuanzishwa kwa Chombo cha Kusimamia Usalama na Ulinzi wa Anga – 2007 *[The Protocol on the Establishment of the East African Community Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency];*

(iii) Maazimio matatu yaliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya Umoja wa Afrika, Kupeleka Majeshi ya Tanzania ya Kulinda Amani katika Jimbo la Darfur, Nchini Sudan na Azimio la Kulaani Mauaji ya Albino Nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipokea Kauli za Serikali na Taarifa za Kamati mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Februari, 2009, ilifanyika Semina kuhusu Msukosuko wa Masoko ya Fedha Duniani. Katika Semina hiyo, Waheshimiwa Wabunge walipata maelezo ya Kitaalam kuhusu Chimbuko la Msukosuko huo, madhara

yanayoweza kuikumba Tanzania na namna ambavyo Serikali imejiandaa kukabiliana na athari zake. Mapendekezo ya Serikali kuhusu ilivyojiandaa kukabiliana na Msukosuko huu yameelezewa vizuri katika Mpango wa Serikali wa Mwaka 2009/2010 ambao tulipata nafasi ya kuujadili hapa Bungeni baada ya kuwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Naamini kwamba Semina tuliyoipata na mapendekezo yaliyomo kwenye mpango yatasaidia sana katika kupata ushauri mzuri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mtikisiko huu wa uchumi unaonekana kuzitikisa sana nchi zilizoendelea zikiwemo za Ulaya, Marekani na Japan. Hata hivyo, kutokana na uchumi wa dunia nzima kuunganika kwa kiasi kikubwa kupitia UTANDAWAZI, uchumi wa nchi moja hasa zile kubwa ukiyumba ni nadra kwa Uchumi wa Nchi changa kama yetu kubaki bila kuyumba.

Mheshimiwa Spika, Sekta moja ambayo Tanzania inaonekana kuathirika ni Sekta ya Biashara ya Nje. Sote tumeshuhudia bei ya zao la pamba ikiwa inashuka kwa kasi katika Soko la Dunia. Taarifa zinaonyesha kuwa bei ya pamba imeshuka kwa asilimia 19.4 kati ya Januari, 2008 na Januari, 2009. Hii inasababishwa na uzalishaji Viwandani kupungua katika Nchi za Ulaya na Marekani ambazo tunazitegemea sana kwa Soko. Takwimu zinaonyesha kwamba uzalishaji viwandani katika nchi hizi ambao ulikua kwa asilimia 2.9 mwaka 2007, umeshuka kwa kasi kubwa mwishoni mwa mwaka 2008. Hii ina maana kwamba mahitaji ya malighafi toka nchi changa yalipungua.

Mheshimiwa Spika, hali hii itaathiri mizania yetu ya Biashara ya Nje. Benki ya Dunia inakadiria kwamba nchi za Tanzania, Kenya na Malawi zitakabiliwa na mtikisiko wa Mizania ya Biashara ya Nje (*Terms of Trade Shocks*) wa zaidi ya asilimia tano ya pato la Taifa. Huu si mtikisiko mdogo kwani ina maana kwamba, pato la wakulima wetu wanaozalisha mazao kama ya pamba litashuka sana.

Mheshimiwa Spika, athari nyingine ambayo inaweza ikaikumba nchi yetu ni kupungua kwa mitaji kutoka nje ambayo imekuwa ikiongezeka nchini katika miaka ya hivi karibuni. Hali hii inatokana na kuwa wawekezaji wengi wameanza kuwa na hofu ya kuwekeza kufuatia mtikisiko huu ambao unaweza ukawasababishia kupoteza mitaji yao. Hali hii pia inachangiwa na wawekezaji wengi kutoweza kupata mikopo kutoka kwenye Benki za Nje ambazo zimeathirika kwa kiasi kikubwa na mtikisiko huu wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, upo pia uwezekano wa Sekta ya Utalii kuathirika kutokana na watalii wengi ambao wanatoka katika nchi tajiri kuahirisha baadhi ya safari zao au kupunguza siku za kukaa nchini. Athari zote hizo zitasababisha uchumi wetu kukua kwa kasi ndogo zaidi ya makadirio ya awali. Tusisahau pia kwamba, misaada na mikopo ya gharama nafuu kutoka katika baadhi ya nchi zilizoathirika na mtikisiko wa uchumi huenda ikashuka kwa kuwa wenyewe wanahitaji kuyaokoa Makampuni yao ambayo yameanza kuonyesha dalili za kufilisika.

Mheshimiwa Spika, hayo niliyoyaeleza hapo juu yanatupa picha ya yale ambayo kama Taifa inabidi tujitayarishe kukabiliana nayo. Kwanza kabisa, hatuna budi kutumia kile kidogo tutakachokipata kwenye vyanzo vyetu vya mapato kwa uangalifu mkubwa. Kwa maoni yangu, Sekta ya Kilimo inabidi ipate fedha za kutosha ili tuweze kuzalisha na kujitosheleza kwanza kwa chakula. Kwa maana, hata kama hali itakuwa mbaya, tukishakuwa na chakula cha kutosha, basi tunaweza kuamka na kufanya kazi nyingine za uzalishaji mali. Sekta za Mifugo na Uvuvi nazo hazina budi kupewa kipaumbele pia katika Bajeti inayokuja ili tuweze kujihadhari na madhara niliyoyaeleza hapo juu. Ni matumaini yangu kwamba, Waheshimiwa Wabunge watashirikiana na Serikali katika kipindi cha mchakato wa kuandaa Bajeti ya mwaka 2009/2010 ili kushauriana namna nzuri ya kupanga vipaumbele vyetu kwa nia ya kutumia kile kidogo tulichonacho kwa uangalifu na kwa manufaa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtikisiko huo wa uchumi duniani unatupa changamoto ya kuimarisha misingi ya ushirikiano wa Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine. Tanzania tunalo jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itifaki zake ikiwa ni pamoja na maamuzi mbalimbali yahusuyo Jumuiya. Mtangamano wa kuanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki kwa mujibu wa Mkataba unaendelea hatua kwa hatua. Katika kipindi cha mwaka 2004 - 2007, kumekuwapo na mafanikio katika mauzo ya Tanzania katika Soko la Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, mauzo ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mauzo ya bidhaa za Tanzania katika Soko la Afrika Mashariki yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani Milioni 95.4 mwaka 2004 hadi Dola milioni 208.9 mwaka 2007. Hili ni ongezeko la asilimia 54.3. Wakati huo huo, mwaka 2007 manunuzi kwa bahati nzuri yalishuka toka Dola za Kimarekani milioni 174.6 mwaka 2006 hadi Dola milioni 106.5 mwaka 2007, ikiwa ni upungufu wa Asilimia 39. Mafanikio hayo yalipunguza nakisi katika Urari wa Biashara baina ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa maana hiyo, uwezo wetu wa kuuza bidhaa katika Nchi hizi upo na unaweza kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mchakato unaoendelea kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, yapo maeneo ambayo bado yanaonyesha hofu kubwa kwa Watanzania. Maeneo hayo yanahusu mambo ya Ardhi; Demokrasia; na Hali ya Usalama, Amani na Utulivu. Vilevile, ipo hofu kwa Watanzania kupoteza fursa za ajira kwa wageni na kutoweza kuajiriwa kwenye Soko la Ajira la Afrika Mashariki. Inabidi sote tuondoe hofu tulizonazo na kujizatiti kikamilifu kukabiliana nazo, kwani umoja huu utakuwa na manufaa makubwa kwa kizazi hiki na vizazi vile vinavyokuja.

Mheshimiwa Spika, Sekta binafsi ni miongoni mwa mihimili mikuu ya kuendeleza Ushirikiano katika Afrika Mashariki. Katika kutafuta fursa zilizopo nchi nyingine za Jumuiya, wafanyabiashara 30 wa Tanzania walitembelea nchi zote za Afrika ya Mashariki ili kuona na kubaini maeneo yanayofaa kwa biashara. Kwa kuwa Sekta Binafsi bado ni changa, nchi wanachama zimejiwekea utaratibu wa kuandaa maonyesho ya Kikanda ya Sekta Isiyo Rasmi kila mwaka, maarufu kama “Maonyesho ya Nguvu Kazi” au “Jua Kali”. Madhumuni ya Maonyesho hayo ni kujenga Sekta Isiyo Rasmi ili

hatimaye ikue na kufikia ngazi ya Sekta Rasmi. Wito wangu kwa Watanzania wote ni kujiandaa vizuri bila hofu kutumia fursa zilizopo na zitakazojitokeza katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha takriban miezi 10, nchi yetu imekabiliwa na tatizo la upungufu wa mvua na hivyo kusababisha Ukame na maeneo mengi nchini kukabiliwa na upungufu wa chakula. Katika baadhi ya maeneo, kilimo cha vuli hakikufanyika kabisa kutokana na mvua za vuli kutokunyesha kabisa miezi ya Oktoba, Novemba na Desemba. Taarifa zinaonyesha kuwa, hadi sasa jumla ya Mikoa 10 yenye Wilaya 21 inahitaji msaada wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo ya Ukame wa muda mrefu, bei za wastani za mazao ya chakula zinaonyesha kupanda zikiashiria kupungua kwa uingizaji wa mazao katika Soko. Kwa mfano, bei ya mahindi imepanda kutoka wastani wa Sh. 30,927/= kwa gunia la kilo 100 mwezi Oktoba, 2008 hadi Sh. 36,612/= mwezi Januari, 2009. Bei ya Januari iko juu kwa asilimia 14 ikilinganishwa na wakati kama huo mwaka jana. Bei ya gunia la Kilo 100 la mchele katika kipindi hicho iliongezeka kutoka wastani wa Sh. 99,736/= mwezi Oktoba, 2008 hadi Sh. 110,517/= mwezi Januari, 2009. Bei za Januari, 2009, ziko juu kwa Asilimia 49 ikilinganishwa na wakati kama huo mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani, bei za vyakula zimeendelea kuwa juu kwa takriban asilimia 25 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka jana. Vile vile, katika baadhi ya Mikoa, hususan maeneo ya mipakani, bei za mazao ya nafaka kama mahindi zipo juu kutokana na kuwepo kwa upungufu mkubwa wa chakula katika nchi jirani. Pamoja na hali hiyo, hatua ya Serikali ya kusitisha uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi hususan nafaka imesaidia sana kwa kiasi fulani kudhibiti kupanda zaidi kwa bei za vyakula nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya upungufu wa chakula, pamoja na kuongezeka kwa bei za vyakula, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

Serikali imetenga jumla ya tani 7,128 za chakula katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* ambapo tani 359 zitasambazwa bure kwa walengwa 12,027 wasio na uwezo wa kununua chakula. Kiasi cha tani 6,769 kilichobaki kitauzwa kwa bei nafuu kwa walengwa waliobaki. Kiasi hiki cha chakula kimeanza kugawiwa katika Wilaya zenye upungufu. Naomba kutoa wito kwa Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya kusimamia vizuri zoezi hilo la mgawo wa chakula.

Serikali imetenga pia jumla ya Shilingi bilioni 1.76 kwa ajili ya kununua jumla ya tani 991 za mbegu zinazostahimili ukame hasa mtama na muhogo kwa ajili ya kuzipatia kaya za wakulima zisizo na uwezo au mazao yao yalikauka na kulazimika kurudia kupanda. Mbegu hizi ni kwa ajili ya kupanda wakati wa Mvua za Msimu wa Masika za 2008/2009 ambazo zimeanza hivi sasa.

Tayari fedha hizo zimekwishatumwa kwa Katibu Tawala wa Mikoa ambao kwa kushirikiana na Halmashauri watasimamia ununuzi na usambazaji wa mbegu hizo. Napenda kuiagiza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kusaidia na kuisimamia Mikoa

katika upatikanaji wa mbegu ili kuharakisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu hizo kwa wakulima haraka na kwa wakati.

Serikali imeendelea kusitisha utoaji wa vibali vya kuuza mazao ya chakula nje ya nchi hadi hapo itakapodhihirika kuwa hali ya chakula nchini ni nzuri. Zoezi hili linahusu zaidi mazao ya nafaka hasa mahindi, ngano na mpunga. Mazao mengine kama aina ya Matunda na Mbogamboga pamoja na Mikunde, isipokuwa Maharage yanaruhusiwa kuuzwa Nje bila ya kibali. Mazao mengine kama Muhogo yamekuwa yanaombewa kibali ili kuyauza nje kutegemeana na hali ya chakula katika Mikoa husika. Zoezi hilo linawahusu hata wale ambao walikuwa na Mikataba ya kuuza vyakula nje ya nchi, hasa wenye Mikataba baada ya kuanzisha zoezi hilo, mwezi Januari, 2008.

Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imeendelea kupokea taarifa za hali ya chakula kwa vipindi vya kila wiki na mwishoni mwa mwezi kutoka Wilaya zote nchini na kuzifanyia uchambuzi na kutoa mapendekezo ya namna ya kuboresha hali ya chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa Nchi inajitosheleza kwa chakula na hata kuwa na ziada, Serikali katika Bajeti ya Kilimo ya mwaka 2008/2009 iliongeza Bajeti ya Pembejeo na mbegu bora kutoka Shilingi bilioni 19.5 mwaka 2007/2008 hadi Shilingi bilioni 31.5 kwa lengo la kuwapatia wakulima pembejeo kwa gharama nafuu. Vilevile, Serikali imeongeza Shilingi bilioni 40 kwa ajili ya kuongeza usambazaji wa mbolea na mbegu bora. Tarehe 10 Februari, 2009, Hazina wametoa Shilingi bilioni 15 ili ziendelee kulipia Vocha za Mbolea ya Ruzuku. Hivyo, kuanzia tarehe 12 Februari, 2009 Benki ya *NMB* itaendelea kuzipokea na kuzilipa Vocha za Ruzuku ya Mbolea kutoka Mfuko wa *EPA* kwa ajili ya kuongeza ruzuku.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 10 Februari, 2009, jumla ya Shilingi bilioni 27.35 zilikuwa zimetumika katika ununuzi wa tani 132,550 za aina mbalimbali za Mbolea ya Ruzuku pamoja na Tani 5,640 za mbegu bora zilikuwa zimesambazwa kwa wakulima. Lengo ni kusambaza jumla ya tani 150,000 za mbolea ya ruzuku katika msimu wa mwaka 2008/2009 na jumla ya tani 6,000 za mbegu bora. Lengo hili litafikiwa kwa kuwa usambazaji unaendelea katika Mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro, Arusha na Manyara ambayo kilimo cha msimu kitaanza mwezi Machi, 2009. Mfumo huo utawezesha pembejeo zenye ruzuku kumfikia mkulima moja kwa moja kwa gharama nafuu. Takriban wakulima 700,000 katika Mikoa mbalimbali nchini wamelengwa kufaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 29 Januari, 2009, akiba ya chakula katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*National Food Reserve Agency - NFRA*) ilikuwa jumla ya tani 128,759 za nafaka, zikiwemo tani 121,334 za mahindi na tani 7,425 za mtama. Akiba hii iko katika Kanda mbalimbali za Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2008/2009, Wakala *(NFRA)* walitengewa jumla ya Shilingi bilioni 30.4 kwa ajili ya ununuzi wa chakula. Hadi

Januari, 2009, jumla ya Shilingi bilioni 23.9 zilikuwa zimetolewa kununulia chakula. Aidha, tarehe 10 Februari, 2009, Hazina walitoa Shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuendelea kununua chakula kwenye maeneo yaliyokuwa yamesimamishwa. Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula wamenunua jumla ya tani 60,285.9 za nafaka zikiwemo tani 59,232.8 za Mahindi na tani 1,053.1 za Mtama. Lengo ni kununua jumla ya tani 100,000 za Mahindi na tani 5,000 za Mtama.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Desemba, 2008, Wafanyabiashara wakubwa wa mazao ya chakula nchini walikuwa na akiba jumla ya tani 123,909 za mazao ya nafaka zikiwemo tani 38,811 za mahindi, tani 1,888 za mchele, tani 82,118 za ngano na tani 1,092 za mtama. Kwa takwimu hizo hali ya akiba ya mazao ya nafaka ambayo ndiyo chakula kikuu cha Wananchi wetu siyo mbaya bado ni ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, uzoefu katika nchi yetu unaonyesha kwamba mojawapo ya njia inayoweza kulihakikishia Taifa aUsalama wa chakula ni kuhimiza kilimo cha umwagiliaji. Hivyo, Serikali itachukua hatua za Kibajeti ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa lengo la kujihakikishia usalama wa chakula. Jukumu kubwa la wataalam wa kilimo ni kuwaelekeza wakulima walioko katika maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji ili wayatumie kikamilifu hata kwa teknolojia za asili wakati Serikali inaongeza uwezo wake wa kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo hayo. Ni wajibu vile vile wa Halmashauri kuhakikisha kuwa wanatenga fedha za kuiwezesha Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa Taifa katika kuongeza kipato kwa Watanzania hasa katika kuzalisha chakula, kutoa ajira pamoja na kuhifadhi rasilimali za Taifa. Utumiaji wa Rasilimali za nyanda za malisho kwenye maeneo yaliyo wazi ni jambo la kawaida katika maeneo ambayo yana ardhi ya kutosha. Hata hivyo, uchungaji wa mifugo inayomilikiwa kijumuiya huchangia kuwepo ufugaji wa kuhamahama kutafuta malisho na maji. Uhamaji huu husababisha kuenea kwa magonjwa ya mifugo, migogoro baina ya wafugaji na wakulima pamoja na uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ipo migogoro mingi itokanayo na uhamaji wa wafugaji na mifugo yao kutoka baadhi ya maeneo kwenda kwenye maeneo mengine hususan Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Morogoro. Wakati nikijibu swali la Mheshimiwa John Momose Cheyo - Mbunge wa Bariadi Mashariki tarehe 5 Februari, 2008 nilieleza kuwa ni vyema wadau wote wakakutana na kujaribu kutafuta suluhisho la kudumu la matatizo yanayowakabili wafugaji wanaohama na mifugo yao. Katika kufanya hivyo, yapo mambo ambayo Wadau wote muhimu wa Sekta hii hatuna budi kuyatafakari. Naomba nitaje tu baadhi ya hayo:-

(i) Kuangalia taratibu zinazotawala mfugaji anapotaka kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine;

(ii) Kiwango cha ushirikishwaji wa wakazi katika eneo analokwenda mfugaji kuhusu kujiridhisha endapo wanamjua na wanajua idadi ya mifugo;

(iii) Matumizi ya ardhi ya Kijiji yana eneo lililotengwa kwa ajili ya wafugaji na kama eneo hilo lina huduma kwa ajili ya mifugo na huduma nyingine za jamii zinazotosheleza kama vile maji, afya na elimu;

(iv) Je, kama mfugaji aliweza kuishi muda mrefu vizuri na mwenzake mkulima, ni sababu zipi sasa zinazowafanya wanakijiji wengine wafikie uamuzi wa kumtaka kuhama?

(v) Utaratibu wa kumhamisha mfugaji unazingatia muda alioishi katika eneo pamoja na utoaji elimu na uhamasishaji au uamuzi wa kuwatoa umechukuliwa tu bila kufikiria. Je, uamuzi wa kuhamisha umetolewa wakati mwafaka. Vile vile lipo suala la muda wa kupewa notisi: Je, unatosha na wameelekezwa wanakokwenda na wanasafirishaje mifugo?

(vi) Utaratibu wa kutoza faini kubwa umetumia misingi ipi na je, Sheria Ndogo zilizotumika zimewekwa vizuri?

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu tunayo Mikoa ambayo jamii za wakulima na wafugaji zinaishi kwa amani bila migogoro. Katika Mikoa hiyo, jamii zote zinaheshimu Sheria na Taratibu na wameweza kutatua migogoro pale inapotokea. Migogoro kati ya wakulima na wafugaji nchini inatokea kwa wingi katika Mikoa ile ambayo wafugaji wamehamia na kuwakuta wakulima.

Jukumu la Serikali ni kuhakikisha kuwa makundi haya yote ya Watanzania yanaishi kwa amani na kwa kuzingatia Sheria na Taratibu za nchi. Mkoa wa Morogoro hivi karibuni ulianza zoezi la kutekeleza Operesheni ya Kuwahamisha baadhi ya Wafugaji waliohamia Mkoani kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania. Kutokana na zoezi hilo, Wilayani Kilosa yamejitokeza malalamiko mengi dhidi ya Viongozi wanaoendesha zoezi hilo. Malalamiko hayo naomba nitaje machache:-

(i) Kutozwa faini ya Sh. 30,000/= kwa kila Mfugaji na Sh. 5,000/= kwa kila Mfugo unaokamatwa kwa siku;

(ii) Mifugo kukamatwa na kuwekwa katika Vituo ambapo hakuna maji na wala malisho;

(iii) Ili kulipa faini mbalimbali, wafugaji walilazimika kuuza ng’ombe kwa bei ya dhuluma wakati mwingine hadi Sh. 40,000/=;

(iv) Utaratibu wa kusafirisha mifugo kwa magari ni wa gharama kubwa na baadhi ya wafugaji wamepoteza mifugo yao chini ya utaratibu huu;

(v) Kukosekana kwa maandalizi mazuri kabla ya zoezi hili kuanza;

(vi) Kutopewa taarifa mapema juu ya kuhamisha Mifugo; na

(vii) Kutokuwepo kwa maeneo maalum yenye miundombinu yaliyotengwa kwa ajili ya wafugaji ambao wanahamishwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko haya, Serikali imemtaka Mheshimiwa John Pombe Magufuli - Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wataalam wa Sekta ya Mifugo, waende mara moja Mkoani Morogoro kutathmini hali ya migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Hivi sasa ninavyozungumza, Mheshimiwa Waziri na Timu yake wako Kilosa na baadaye watakwenda Ulanga na Kilombero kwa lengo la kutathmini hali ya zoezi hilo linavyoendeshwa katika Mkoa wa Morogoro.

Wakiwa huko, tumewaasa wazungumze na wadau mbalimbali na kuwasilisha taarifa yao Serikalini mapema iwezekanavyo. Hivyo baada ya kushauriana na Serikalini, tumeona ni vizuri kwanza kupata taarifa ya Wizara kabla ya kufanya maamuzi kuhusu zoezi la kuhamisha wafugaji Wilayani Kilosa linaloendelea. Hivyo Serikali inawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wavute subira kidogo wakati tunamsubiri Mheshimiwa Waziri kuleta taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kujenga Sekta ya Mifugo iliyo endelevu ni muhimu tufanye maamuzi magumu na muhimu. Hatuna budi kutoa elimu kwa wafugaji ili wajue thamani ya kupunguza Mifugo na kutumia walichopata kujiletea maendeleo. Serikali inakusudia kuwawezesha wafugaji kuondokana na mfumo wa kuchunga na kuingia katika mfumo wa kufuga ili kujibu hoja ya kupunguza Mifugo na kuiboresha. Serikali inasisitiza kuwa ufugaji wa kuhamahama hauna tija.

Katika mazingira tuliyonayo ya kuongezeka kwa mahitaji ya ardhi kutokana na ongezeko la watu na shughuli mbalimbali za kijamii, ni lazima sasa wafugaji nao watambue kuwa wana dhamana ya kubadilika ili waweze kutumia rasilimali tulizonazo kwa ufanisi na tija zaidi. Serikali inaelewa kuwa changamoto bado ni nyingi katika Sekta hii. Kwa mfano, bado hatuna utaratibu mzuri wa soko la mifugo na ngozi zenye mvuto, mfano viwanda vya kusindika nyama na ngozi. Bado utaratibu wa Ranchi ndogo ndogo haujakomaa na kutupa jibu kama ni utaratibu unaowezakana katika mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuchukua hatua za muda wa kati na muda mrefu, Mheshimiwa Rais ameagiza viongozi na baadhi ya wataalam wa Mikoa yote yenye makundi ya jamii za wafugaji na wakulima wakutane mara moja ili kwa pamoja wakubaliane na kufikia maamuzi ya kukabiliana na tatizo hili la kuhamahama kwa wafugaji. Natarajia kuitisha kikao hicho mapema iwezekanavyo. Makubaliano hayo yatatupa mwongozo ambao itabidi wadau wote wakubaliane nao. Aidha, Serikali imeamua kuwakutanisha wakuu wa Mikoa yote yenye matatizo, hasa ya wafugaji na wakulima ili kubadilishana mawazo ya namna bora ya kutatua matatizo yanayotokana na migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi za uvuvi na pande zote zimezungukwa na bahari, maziwa, mito na mabwawa ambayo yamesheheni aina

mbalimbali za samaki na viumbe wengine wa majini. Takwimu zinaonyesha kuwa, kati ya Januari, 2006 na Desemba, 2008, inakadiriwa jumla ya tani 1,014,877 za samaki zenye thamani ya Shilingi bilioni 783.3 zilivunwa. Kati ya tani hizo, jumla ya takribani tani 189,272.6 ziliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 597.5.

Kutokana na mauzo hayo, Serikali ilipata mapato yanayokadiriwa kufikia Shilingi bilioni 25.8, zikiwa ni ushuru na ada za leseni mbalimbali. Kwa mwaka 2007/2008, mavuno ya samaki wa Ziwa Viktoria peke yake yalikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 220. Kiasi hicho cha mapato kiliingizia Serikali maduhuli ya jumla ya Shillingi bilioni 8.1. Hii haijumuishi kodi zilizotozwa na mamlaka nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na utajiri huo mkubwa wa rasilimali za majini na mapato yanayoonekana kuwa makubwa, nchi yetu haijanufaika ipasavyo na rasilimali hizo kwani Sekta ya Uvuvi imekuwa ikichangia pato la Taifa kwa asilimia 1.6 tu. Kwa mtizamo wangu, kutokana na ukubwa wa bahari na wingi wa maziwa, mito na mabwawa tuliyonayo, Sekta ya Uvuvi ilitakiwa iwe na mchango mkubwa zaidi kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu nyingi zinazochangia nchi kupoteza mapato yake mengi katika Sekta ya Uvuvi. Sababu kubwa zaidi ni uvuvi haramu, utoroshaji wa rasilimali na ujangili uliokithiri sehemu mbalimbali za uvuvi, hasa eneo la baharini. Taarifa za tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa, kutokana na uvuvi usiokuwa endelevu, mazao ya majini yamepungua sana.

Kwa Mfano, kwenye Ziwa Victoria, samaki aina ya sangara wamepungua kutoka tani 750,000 mwaka 2006 hadi tani 375,000 mwezi Februari, 2008. Hiki ni kipindi cha takribani miaka miwili, ambapo samaki aina ya sangara wamepungua kwa kiasi cha ssilimia 50. Vilevile, mwezi Agosti, 2008, takribani miezi sita tu, sangara walipungua zaidi na kufikia takribani tani 227,365, ikiwa ni pungufu zaidi kwa asilimia 39.4. Tafsiri ya takwimu hizo ni kwamba kwa kipindi cha takriban miaka miwili na miezi 6, samaki aina ya sangara, Ziwa Victoria walipungua kwa asilimia 89.4. Hivyo haishangazi kwamba baadhi ya viwanda sasa vinasuasua na vingine kufungwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye bahari ya Hindi, samaki aina ya Kambamti nao wamepungua kutoka tani 1,320.1 mwaka 2003 hadi tani 202.1 tu mwaka 2008. Kwa kipindi hiki cha takribani miaka mitano, aina hiyo ya samaki wa Kambamti wamepungua kwa Asilimia 85. Hali hii ilisababisha kufungwa kwa msimu wa uvuvi wa kambamti kwa mwaka 2008 kwa meli kubwa za uvuvi ingawa wavuvi wadogo wadogo bado waliendelea na uvuvi wa samaki hao. Mifano hii miwili ya Ziwa Victoria na Bahari ya Hindi, inadhihirisha ukubwa wa tatizo la uvuvi haramu na ujangili wa maliasili za majini. Hali hii ipo kwenye maeneo yote ya Maziwa, Mabwawa, Mito na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kukaa kimya na kutazama rasilimali zetu za majini zikinufaisha watu wa Mataifa mengine. Vilevile, Serikali haiwezi kufumbia macho vitendo vya uvuvi haramu, utoroshaji wa rasilimali na ujangili ambavyo vinahatarisha rasilimali hizo kwa vizazi vijavyo. Kutokana na hali hiyo inayotishia uchumi wa nchi yetu na wananchi wake, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali

kukabiliana na uvuvi haramu, magendo ya mazao ya uvuvi na ujangili katika Sekta ya Uvuvi. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Kuanzisha Vituo 12 vya Doria na usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika maeneo ya Kipili na Kasanga Mkoa wa Rukwa; Tunduma Mkoa wa Mbeya na Horohoro Mkoa wa Tanga. Maeneo mengine ni Sirari na Sota Mkoa wa Mara; Kanyigo, Rusumo na Kabanga Mkoa wa Kagera; Kilwa Mkoa wa Lindi; Kisiwa cha Mafia Mkoa wa Pwani na maeneo ya Mkoa wa Mtwara;

(ii) Kuongeza Ushirikiano wa Kikanda kwa kupitisha Mpango wa Kikanda kwa ajili ya udhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Victoria;

(iii) Kukamilisha na kuanza kutumia mwongozo wa Kitaifa wa Uboreshaji na Uendeshaji wa Vikundi vya Ulinzi wa Rasilimali ya Uvuvi;

(iv) Kukamilisha na kuanza kutumia Kanuni za Sheria ya Uvuvi Bahari Kuu Sura Na. 388; na

(v) Kupiga vita matumizi ya zana haramu za uvuvi ikiwa ni pamoja na kuzisaka na kuziharibu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wananchi na wadau mbalimbali wa Sekta ya Uvuvi wanaelewa vizuri madhara ya uvuvi haramu, nawasihi Viongozi na Wataalam wa Wizara husika kuanzisha vipindi maalum vya kwenye Luninga na vyombo vingine vya habari, kuonyesha madhara ya kutumia zana haramu katika uvuvi. Hii itawasaidia wananchi kwa ujumla kuona hali halisi ya uharibifu na madhara yake kwa mazalio ya samaki. Wote tukumbuke kuwa uzao wa Samaki sio kama wa mihogo ambayo ukivunja kijiti na kusimika kwenye ardhi kinaota. Ukiharibu mazalio ya samaki, wanatoweka kabisa.

Hata hivyo, Serikali inasisitiza kuwa katika zoezi hili la kupambana na uvuvi haramu Watendaji wote na Viongozi watakaohusika hawana budi kuzingatia Sheria na Taratibu za nchi. Lazima wahakikishe kuwa hawanyanyasi wananchi kwa njia za kuwapiga, kuwatukana, kuwatunishia misuli na lugha za matusi na matumizi ya nguvu yasiyo ya lazima. Uongozi wa Mikoa yote inayohusika naagiza walisimamie zoezi hili ili malengo yake yaweze kufikiwa bila malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niseme kidogo kuhusu elimu ya msingi. Katika Mikutano ya Bunge iliyopita, Serikali imekuwa ikieleza mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye Sekta ya Elimu. Mafanikio katika Elimu ya Msingi na Sekondari yametokana na utekelezaji mzuri wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM)* na ule Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES).*

Kutekelezwa kwa *MMEM* kumesababisha ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba na wanaofaulu ili kujiunga na Elimu ya Sekondari.

Takwimu zinaonyesha kuwa, idadi ya wanafunzi waliofanya Mtihani wa Darasa la Saba imeongezeka kutoka 494,504 mwaka 2002 hadi 1,017,967 mwaka 2008. Idadi ya wanafunzi waliofaulu imeongezeka kutoka 133,674 mwaka 2002, sawa na asilimia 27.1 ya waliofanya mitihani mwaka 2002 hadi 536,672 sawa na asilimia 52.8 ya waliofanya mtihani mwaka 2008. Kwa kipindi hicho cha takriban miaka saba, kumekuwepo na ongezeko la ufaulu la asilimia 25.7.

Tafsiri ya takwimu hizo ni kuongezeka kwa mahitaji ya madarasa, maabara na vifaa vyake, madawati, matundu ya vyoo, vitabu, walimu na vifaa vingine vya kufundishia. Lakini kubwa zaidi ni kuongezeka kwa mahitaji makubwa kwenye Elimu ya Vyuo vya Juu nchini. Hizo zote ni changamoto ambazo Serikali inabidi kukabiliana nazo na hapa tunaomba ushirikiano wa karibu na Watanzania. Hapa tunahitaji nguvu ya pamoja hasa kutoka kwa mtu mmoja mmoja, vikundi vya Kijamii, Taasisi zisizo za kiserikali, Mashirika ya Kidini, Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanafunzi waliofanya mtihani wa Darasa la Saba mwaka 2008 ilikuwa 1,017,967. Kati yao, waliofaulu na waliotakiwa kujiunga na Kidato cha Kwanza ni 536,672. Hii ni sawa na asilimia 52.8 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani. Mikoa mitano iliyoongoza kwa kufaulisha wanafunzi ni Dar es Salaam asilimia 73.9, Arusha asilimia 66.2, Iringa asilimia 64.1, Kagera asilimia 63.5 na Kilimanjaro asilimia 57.1. Mikoa iliyofanya vibaya ni Shinyanga asilimia 34.0, Lindi asilimia 40.7, Mara asilimia 42.6, Tabora asilimia 43.2 na Mtwara asilimia 45.1.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo ya wanafunzi kufaulu kwa asilimia 52.8, bado kuna tatizo la idadi kubwa ya wanafunzi kukosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza. Taarifa za Mikoa zilizopatikana zinaonyesha kwamba, kati ya wanafunzi 535,570 waliofaulu, ni wanafunzi 439,154, sawa na asilimia 82.0 ndio waliochaguliwa Awamu ya Kwanza na kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya Kidato cha Kwanza. Mikoa iliyofanikiwa kupeleka wanafunzi Sekondari kwa asilimia 100 ni Dodoma, Kilimanjaro, Lindi, Mwanza, Shinyanga, Singida na Tanga. Hapa utaona kwamba kati ya Mikoa Mitano iliyofanya vibaya katika ufaulishaji bado wameshindwa kupeleka asilimia 100 ya wanafunzi waliofaulu katika awamu ya kwanza, isipokuwa Mkoa wa Lindi na Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mikoa ambayo inatarajia kupeleka wanafunzi wote Sekondari kwa asilimia 100 baada ya Uchaguzi Awamu ya Pili ni Mikoa ya Tabora, Ruvuma, Rukwa, Morogoro, Mara, Kigoma na Mtwara. Mikoa ambayo itabakiza wanafunzi wengi bila kujiunga na Sekondari hata baada ya Uchaguzi wa Awamu ya Pili, kwanza ni Dar es Salaam wanafunzi 11,563, sawa na asilimia 24.2; Kagera wanafunzi 7,325, sawa na asilimia 22.5; Iringa wanafunzi 3,556, sawa na asilimia 10.3; Arusha wanafunzi 850, sawa na asilimia 3.1; na Pwani wanafunzi 198, sawa na asilimia 1.2. Kwa takwimu hizo, jumla ya wanafunzi watakaobaki bila kupata nafasi ni 23,492, sawa na asilimia 4.4 ya wanafunzi wote waliofaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Mikoa iliyopeleka wanafunzi waliofaulu Sekondari kwa asilimia 100, nawapongeza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wao.

Hawa wameitikia wito wa Serikali wa kutambua kuwa zoezi la kuwapeleka Sekondari wanafunzi wote wanaofaulu ni la kudumu na endelevu. Hongereni sana! Mikoa ambayo imeahidi kupeleka wanafunzi katika Awamu ya Pili, watekeleze jukumu hilo na nipate taarifa mapema. Kwa Mikoa ambayo imepanga kutowapeleka Sekondari Wanafunzi wote waliofaulu, nasema hali hii haikubaliki. Kwa hiyo, tulipokutana Dar es Salaam na Wakuu wa Mikoa wote, wote walioahidi kufanya kazi kufa na kupona kuhakikisha watoto wote wanachukuliwa awamu ya pili. Naomba ahadi hiyo itekelezwe na niletewe taarifa kujulishwa kwamba imetekelezwa. *(Makofi)*

Sitarajii kutumia fedha za Serikali kuitisha Vikao na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya au Wakurugenzi wa Halmashauri kuzungumzia suala ambalo linaeleweka kwa kila mmoja wetu. Nahitaji tu kupata taarifa Mikoa hiyo kuwa wanafunzi wote waliofaulu wamepelekwa Sekondari kama tulivyoahidiwa. *(Makofi)*

Viongozi wa Mikoa itakayoshindwa kupeleka wanafunzi waliofaulu Sekondari kwa asilimia 100, watakuwa wameshindwa katika kigezo mojawapo cha kupima uwezo wao wa kupokea maagizo, kuyapangia mikakati na kutekeleza. Suala la watoto wetu kusoma halihitaji mjadala wala vikao. Hili ni la utekelezaji tu. Kwa hiyo, Viongozi wote wa Mikoa na Wilaya wajenge tabia ya kutekeleza majukumu yao bila kusubiri Viongozi wa Kitaifa wala mtu mwingine yeyote ama kumkumbusha au kumsukuma kila wakati ili aweze kutekeleza jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuongelea kidogo juu ya Elimu ya Walemavu wa Ngozi nchini. Takwimu zinatuonyesha kuwa katika mwaka 2008 kulikuwa na walemavu wa ngozi 206; wavulana 98 na wasichana 108 katika Shule za Awali, 3,107 ambapo wavulana 1,713 na wasichana 1,394 katika Shule za Msingi na 62 wavulana 39 na wasichana 23 katika Shule za Sekondari. Takwimu hizo pia zinatuonyesha kuwa kwanza, ni idadi ndogo sana ya walemavu wa ngozi wanapata nafasi ya kuendelea na Sekondari, iwe kwa kufaulu Elimu ya Msingi au kujiunga na Sekondari Binafsi.

Pili zinatuonyesha kuwa idadi ya wasichana wenye ulemavu wa ngozi inapungua kwa kasi kubwa kuliko ya wavulana wenye ulemavu wa ngozi kadri wanavyopanda ngazi za elimu. Hivyo, wasichana wenye ulemavu wa ngozi wanakosa elimu zaidi ya wavulana. Napenda kurudia agizo langu nililolitoa wakati wa ziara yangu Kanda ya Ziwa, kwamba kila Halmashauri ihakikishe kuwa watoto wote wenye ulemavu wa ngozi wanakwenda shule kwa kuwaondolea vikwazo vinavyowazuia kufanya hivyo na hasa vile vinavyotokana na hofu ya kuuwawa kutokana na imani potofu za ushirikina.

Ni matumaini yangu kwamba hatutasikia mlemavu wa ngozi yeyote aliyeshindwa kwenda shule kutokana na matatizo yanayoweza kutatuliwa na Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2008, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sehemu ya Mlimani, Chuo Kikuu cha Ualimu Chang’ombe *(DUCE);* Chuo Kikuu cha Ualimu Mkwawa *(MUCE);* na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo *(SUA);* vilifungwa kufuatia migomo, vurugu na maandamano ya wanafunzi yaliyotokea katika Vyuo hivyo.

Kwa upande wa Chuo cha Ardhi ambacho kilifungwa Septemba, 2008, kilifunguliwa tarehe 9 Februari, 2009 na udahili unaendelea. Baada ya tukio hilo, Mabaraza ya Vyuo Vikuu na yale ya Uongozi wa Vyuo Vikuu Vishiriki yalikutana na kuweka utaratibu na muda wa kufunguliwa kwa Vyuo hivyo. Ilikubalika kwamba, kwa wale wanafunzi watakaopenda kurejea Vyuoni, lazima wajaze Fomu Maalum za maombi ya kujiunga na Vyuo na wawe wamezirejesha Vyuoni ifikapo tarehe 31 Desemba, 2008. Hata hivyo, muda huo wa kurejesha Fomu za Maombi uliongezwa mpaka tarehe 29 Januari, 2009.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia tarehe 09 Februari, 2009, hali ya udahili ilikuwa kama ifuatavyo:-

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(UDSM),* Sehemu ya Mlimani, wanafunzi waliotarajiwa kurejea Chuoni walikuwa 11,259. Wanafunzi 9,934, sawa na asilimia 88 walioomba na kutimiza masharti ya kurejea Chuoni walirejea. Wanafunzi 138, sawa na asilimia 1 ya waliotarajiwa kurejea Chuoni hawakuwasilisha maombi ya kudahiliwa upya. Wanafunzi 577 walioomba, lakini hawakutimiza masharti na wanafunzi 610 walihamia Vyuo vingine.

Chuo Kikuu cha Ualimu Dar es Salaam, *(DUCE),* wanafunzi waliotarajiwa kurejea Chuoni ni 3,560. Walioomba kurejea ni 3,435, sawa na asilimia 96. Wanafunzi 125 hawakuomba, sawa na asilimia nne. Kati ya walioomba, wanafunzi 3,218 walitimiza masharti na wanafunzi 217 hawakutimiza masharti.

Chuo Kikuu cha Ualimu Mkwawa, *(MUCE),* waliotarajiwa kurejea ni wanafunzi 1,949. Walioomba na kutimiza masharti na kurudi walikuwa 1,889, sawa na asilimia 97. Wanafunzi ambao hawakuomba kurudi ni 60.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo *(SUA),* waliotarajiwa kurejea ni wanafunzi 2,243. Walioomba na wakatimiza masharti ya kurudi ni 2,227, sawa na asilimia 99. Wanafunzi ambao hawakuomba ni 16 tu.

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi *(MUCCOBS),* waliotarajiwa kurejea ni wanafunzi 1,254. Walioomba kurejea ni 1,204. Waliotimiza masharti na kurudi ni 1,154, sawa na asilimia 92 ya waliotarajiwa kurejea. Wanafunzi 50 kati ya walioomba kurejea walipatikana na vyeti vya kughushi. Wanafunzi 50, sawa na asilimia nne hawakuomba kurudi.

Mheshimiwa Spika, kwa Vyuo vilivyotajwa hapo juu, idadi ya wanafunzi waliotarajiwa kurudi Vyuoni ni 20,265 na waliofanikiwa kutimiza masharti na hivyo kudahiliwa walikuwa 19,032, sawa na asilimia 94. Idadi hii inajumuisha wanafunzi 610 waliohama na kudailiwa katika Vyuo vingine. Kwa ujumla wanafunzi 389, sawa na asilimia mbili hawakuomba kurejea Vyuoni. Wanafunzi 844, sawa na asilimia nne waliomba, lakini hawakutimiza masharti au walikutwa na vyeti vya kughushi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, mikopo ya Elimu ya Juu iliyotolewa kwa mwaka wa masomo 2008/2009 ilikuwa imefikia Shilingi bilioni 80.6. Kati ya Shilingi bilioni 117 zilizotengwa. Wanafunzi waliopata mikopo hiyo ni 56,071, wakiwemo 998 wa Vyuo vya Nje ya Nchi. Idadi hii ni asilimia 93.5 ya lengo la kukopesha wanafunzi 60,000. Wanafunzi ambao wameshakopeshwa hadi sasa kwa kila daraja ni kama ifuatavyo:- Daraja "A" waliokopeshwa Asilimia 100 ni 8,342, Daraja la "B" asilimia 80 ni 29,647, Daraja "C" waliokopeshwa asilimia 60 ni 12,778, Daraja "D" waliokopeshwa asilimia 40 ni 1,558, Daraja "E" waliokopeshwa asilimia 20 ni 74 tu na hakuna wasiopata mkopo ambao wanastahili kuwa katika Daraja "F".

Mheshimiwa Spika, Mikopo inayotolewa imegawanyika katika sehemu mbili. Kwanza, ni mikopo inayotolewa kwa asilimia 100 kwa wanafunzi wote ambayo ni mikopo ya chakula na malazi, vitabu na viandikwa na utafiti. Pili, kuna Mikopo inayotolewa kwa mwanafunzi ili na yeye achangie sehemu ya gharama. Mikopo hiyo inahusisha ada ya mafunzo (*Fee*), mahitaji maalum ya Kitivo na Mafunzo kwa Vitendo. Utaratibu wa kupata viwango vya mikopo kwa kundi hili la pili unaotumika ni wa *means testing* na ulianza kutumika kuanzia mwaka 2006/2007 ambapo wanafunzi wote walikopeshwa asilimia 60 ya gharama na wao kuchangia asilimia 40. Katika mwaka 2007/2008 na 2008/2009 wanafunzi wamekuwa wakiwekwa kwenye madaraja mbalimbali ya kukopeshwa ambayo ni *A, B, C, D, E* na *F*.

Kwa muda wa miaka hiyo miwili 2007/2008 na 2008/2009 wanafunzi ambao wameshakopeshwa kwa ujumla wake ni 107,963 kama ifuatavyo: Daraja 'A' ni 30,749, sawa na asilimia 28.5; Daraja 'B' ni 48,913, sawa na asilimia 45.3; Daraja 'C' ni 25,696, sawa na asilimia 23.8; Daraja 'D' ni 2,464, sawa na asilimia 2.3; Daraja 'E' ni 141, sawa na asilimia 0.1 na Daraja 'F' ni '0' (hakuna). Idadi hii inahusisha Wanafunzi wa Mwaka wa 'I' na wanaoendelea na masomo Vyuoni. Daraja linaloongoza kwa kupata mikopo ni Daraja 'B' ambalo wanafunzi wanakopeshwa asilimia 80 likifuatiwa na 'A' ambalo wanafunzi wake wanakopeshwa asilimia 100. Huu ni uthibitisho kwamba tukidhamiria na kushirikiana wote kwa dhati kwa maana ya Serikali, wazazi na wanafunzi, tunaweza kuwapatia wanafunzi wengi zaidi Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa utaratibu huo wa *means testing,* bado Wadau wa Elimu hasa wanafunzi wamekuwa hawaridhiki na utaratibu huu. Serikali kwa kushirikiana na wadau hao imefanya marekebisho na kuuboresha utaratibu huo na sasa kuanzia mwaka 2009/2010. Serikali katika ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya zitashirikishwa katika kuthibitisha ukweli wa maombi ya wanafunzi, madaraja ya mikopo pia yataongezeka kutoka 6 (A – F) hadi 11 (A – K). Hii itatoa nafasi nyingi zaidi kwa ajili ya watu kuweza kukopeshwa kwa viwango mbalimbali kwa maana ya 'A' watapewa mkopo asilimia 100, 'B' asilimia 90, 'C' Asilimia 80 na kadhalika.

Vilevile, utaratibu huo utaweza kubainisha vizuri zaidi watoto wale wote wenye uwezo na elimu ya kutosha itatolewa kwa wadau wote juu ya utaratibu huu mpya. Ni matarajio yangu kuwa utaratibu huo mpya utapunguza malalamiko ya Wadau wa Elimu ya Juu nchini ambayo yamekuwa yakijitokeza muda wote. Hata hivyo, Serikali bado

itaendelea kufanya juhudi za kuboresha mfumo ili tuweze kufika mahali tukawa na utaratibu ambao ni mzuri na unaokubalika na kila mtu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Januari, 2009, nilitembelea Chuo Kikuu cha Dodoma ili kukagua maendeleo ya ujenzi wa majengo mbalimbali, miundombinu na uendeshaji wa Chuo hicho. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naye amekitembelea Chuo hicho tarehe 05 Februari, 2009. Hatua zilizofikiwa katika ujenzi ni nzuri sana. Katika mwaka wa masomo 2008/2009 Chuo kimechukua jumla ya Wanafunzi 6,948 na zoezi la kuajiri wafanyakazi bado linaendelea.

Napenda kutumia nafasi hii, kumshukuru sana Makamu Mkuu wa Chuo na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri yenye kuonyesha kuwa Watanzania tunaweza. Hakika wamewezesha mambo mengi kufanyika kwa wakati mmoja lakini kwa mpangilio unaoonekana na kueleweka. Vilevile, nawashukuru na kuwapongeza Viongozi wote katika ngazi zote walioshiriki na wanaendelea kushiriki katika kuwezesha Chuo hicho kujengwa na kufanya kazi kwa nguvu zaidi. Nawashukuru Wakandarasi wote, mafundi na watoa huduma wote wanaowezesha kazi zinazoendelea Chuoni hapo kufanyika katika kiwango cha hali juu. *(Makofi)*

Hata hivyo, bado kuna matatizo yanayokikabili Chuo na hasa kutokana na kasi ya ukuaji wake. Tunaendelea kukabiliana nayo. Katika kufanya hivyo, niwatake wale wote wanaohusika kwa njia yoyote ile katika kufanikisha kuwepo kwa Chuo hicho washiriki kikamilifu katika kutimiza lengo letu la kuwa na Chuo Kikuu kikubwa hapa nchini. Wale wote wanaohusika na maji, umeme, barabara, majengo, ufadhili, uendelezaji wa maeneo yanayokizunguka Chuo, waunge mkono juhudi zilizopo ili tuweze kupiga hatua katika maendeleo ya Elimu ya Juu nchini. *(Makofi)*

Manispaa ya Dodoma washirikiane na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma ili kuhakikisha kwamba ujenzi wa Miundombinu wa Mji wa Dodoma inajengwa kwa mpangilio mzuri.

Mheshimiwa Spika, tarehe 19 hadi 24 Januari, 2009, nilifanya ziara katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Tabora na Shinyanga kujionea hali halisi ya mauaji ya walemavu wa ngozi na vikongwe. Katika ziara hiyo, nilipata fursa ya kusikia kutoka kwa wananchi, viongozi wa Serikali, Asasi zisizokuwa za Serikali na Taasisi za dini kuhusu chanzo cha matatizo ya mauaji hayo. Vilevile, niliongea na waathirika wa mauaji hayo na kupanga mikakati ya pamoja ya jinsi ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu ambazo zimetolewa na ambazo inaaminika ndizo zinazosababisha mauaji hayo. Baadhi ya Sababu hizo ni pamoja na ukosefu wa Elimu ya kawaida; jamii kuwa na uelewa mdogo wa Sheria; ukosefu wa imani ya kiroho na kuwepo kwa Waganga wa Kienyeji ambao huchochea suala la ushirikina katika kutaka kupata utajiri wa haraka. Sababu hizi kwa asilimia kubwa ndizo zinazosababisha mauaji hayo.

Vilevile, sababu hizi ndizo ambazo jamii inaamini kwamba vikongwe ni wachawi baada ya kupata matokeo ya ramli ambapo Waganga wa Kienyeji husema kwamba vijana, watoto wadogo na ndugu wengine huuawa kwa imani za kishirikina. Ni kwa sababu hii jamii huamua kulipiza kisasi kwa kuwaua Vikongwe hawa wakiwatuhumu kwamba ni wachawi.

Nimetumia neno “Waganga wa Kienyeji” na siyo Waganga wa Jadi/Tiba Asili kwa makusudi. Waganga wa Jadi/Tiba Asili tunaowafahamu wote ni wale wenye uwezo au waliorithi taaluma ya kutumia miti shamba kutoa huduma za matibabu. Waganga wa kundi hili hawapigi ramli wala hawashauri mtu kupata kiungo cha binadamu mwenzake kupata utajiri. Hawa wanaodanganya wengine kutafuta viungo vya wenzao ndiyo nimewaita “Waganga wa Kienyeji”. Bahati mbaya sana hata Waganga wengine wachache ambao kwa tafsiri niliyotumia nao wameingia katika kundi la Waganga wa Kienyeji. Naomba na nawasihi sana bado Taifa linaheshimu sana mchango unatolewa na Waganga Tiba ya Asili au Waganga wa Jadi, naomba tushirikiane kuhakikisha kwamba taaluma hiyo inalindwa na inakuwa na Waganga wa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba tatizo la mauaji ya vikongwe ni kubwa. Takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2003 hadi 2008, jumla ya vikongwe 2,870 waliuawa. Mikoa inayoongoza kwa mauaji haya ni Mwanza Vikongwe 697; Shinyanga 525; Tabora 508; Iringa 256; Mbeya 192; Kagera 186; Singida 120; na Rukwa 103. Kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba Mauaji ya Wazee hawa ambao ni Ndugu zetu na Wazazi wetu ni makubwa na yanasikitisha.

Mheshimiwa Spika, mauaji mengine ya kutisha ni ya walemavu wa ngozi, yaani Albino. Naomba nieleze kidogo hili kwa kifupi. Mauaji haya yanaongezeka kwa kasi kubwa. Tuombe Mungu atunusuru yasiendelee zaidi. Takwimu zinaonyesha kwamba tangu tatizo hilo lianze mwezi Julai, 2007 hadi Januari, 2009, jumla ya walemavu wa ngozi 38 wameuawa. Mikoa inayoongoza kwa kuua walemavu wa ngozi tena kwa ukatili mkubwa ni Mwanza Watu 20; Kagera 6; Shinyanga 4; Mara 4; Kigoma 3; na Mbeya 1.

Mheshimiwa Spika, katika hali kama hii, napenda Waheshimiwa Wabunge wenzangu mnielewe kwamba, hali hii inatisha na ni wajibu wetu kulaani mauaji haya kwa nguvu zote. Kwa hali ya mauaji kama haya, naomba wanaharakati wa Haki za Binadamu nao watusaidie kupambana na mauaji haya.

Kama tunataka kuweka Mizania ya Haki za Binadamu sawa tuhamasishe kila mmoja kulinda uhai wa wenzetu kwanza. Mtu anayeuawa alikuwa na haki ya kuishi kama aliyeua. Tukiweza kuona uhai wa wenzetu kama wakwetu kwanza, tutakuwa tumepiga hatua moja kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu na niwapongezeni sana kwa kupitisha Azimio jioni hii kwa ajili ya kulaani mauaji haya ya kikatili. Tuondoke hapa na Kauli Mbiu ya “THAMINI UHAI WA MWENZAKO KWANZA”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunakabiliwa na changamoto kubwa ya kuzuia mauaji hayo inabidi kufanya yafuatayo:-

(i) Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa Mikoa yote na hasa ile ambayo mauaji yamekithiri na yenye waathirika na wananchi wote kwa ujumla kuhusu mauaji haya;

(ii) Viongozi wa dini wasaidie katika kuwajenga waumini wao kukua kiroho ili kuachana na imani potofu za ushirikina;

(iii) Vyombo vya Dola navyo sasa wajidhatiti, wajipange upya kusimamia vizuri mapambanao hayo; washirikishe jamii kwa kiasi kikubwa kupitia vikundi vya ulinzi wa jadi, uimarishwe ikiwa ni pamoja na kurejesha Ulinzi wa Sungusungu na vishirikiane kutimiza wajibu wao vizuri. Vilevile, Mahakama zitoe kipaumbele katika kushughulikia kesi za mauaji ya walemavu wa ngozi na vikongwe; pale panapostahili, adhabu kali zitolewe ili iwe fundisho kwa wahalifu hawa wa Mauaji;

Nimepata faraja kubwa kusikia kauli ya Jaji Mkuu, Mheshimiwa Augustino Ramadhani aliyoitoa Siku ya Sheria Nchini, tarehe 6 Februari, 2009 kuwa, Mahakama zitaharakisha kesi za watuhumiwa ili haki itendeke kwa wote; *(Makofi)*

(iv) Naomba vilevile Vyombo vya Habari vishiriki kikamilifu katika kupiga vita mauaji hayo ya kinyama. Vilevile, vitumie taaluma ya uandishi wa habari kuwafikishia wananchi taarifa muhimu bila kuchochea kasi ya mauaji; *(Makofi)*

(v) Usajili wa Waganga wa Jadi/Tiba Asili ufanyiwe mapitio kwa makini ili kuwatambua Waganga Wababaishaji. Vilevile Serikali katika ngazi zote iweke utaratibu wa kupima kila mara Utendaji wao wa Kazi;

(vi) Tuamshe ari ya wananchi kushiriki katika ulinzi wa watu wenye ulemavu wa ngozi na vikongwe. Viongozi wa Mkoa, Wilaya kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama nao wajipange upya kuhakikisha wanakuwa na ajenda ya kudumu juu ya mauaji katika maeneo yao;

(vii) Viongozi wote wakiwemo wa Serikali na Vyama vya Siasa washirikiane katika Vita hii dhidi ya mauaji ya walemavu wa ngozi na vikongwe na mimi naamini tutashinda; na

(viii) Halmashauri zote Nchini zifanye utaratibu wa kuwatambua watu wote wenye ulemavu wa ngozi katika maeneo yao na hasa wale ambao sasa wako mashuleni wakisubiri kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze eneo lingine ambalo nalo kwa Watanzania lina masikitiko mengi. Inaniwia vigumu sana kuongelea suala la ajali za barabarani na hasa ukichukulia ajali za hivi karibuni zilivyoyachukua maisha ya Watanzania wengi kwa mara moja wasiokuwa na kosa wala hatia. Ajali za barabarani zinasababisha upotevu wa maisha ya binadamu pamoja na uharibifu mkubwa wa mali, vifaa na bidhaa mbalimbali. Vilevile, ajali hizi zinawaacha wananchi wengi wakiwa walemavu wa maisha kwa kupoteza baadhi ya viungo vyao. Inasikitisha sana. Mbali na madhara hayo, Taifa linapoteza nguvu kazi kubwa hasa ikizingatiwa kwamba wengi wa wasafiri ni watu walio kwenye umri mzuri wa kuelekeza nguvu zao kwenye Ujenzi wa Taifa. Hali hii inachangia kudumaza ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

Takwimu zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2008 kulikuwa na jumla ya ajali za barabarani 20,148, ikiwa ni wastani wa ajali 55 kila siku au ajali 1,679 kwa mwezi. Ajali hizo zilisababisha jumla ya vifo vya watu 2,924 na kujeruhi wengine 17,825. Jamani! Idadi hii inatisha!

Mheshimiwa Spika, niruhusu nitaje idadi ya ajali zilizotokea katika kila Mkoa kwa Mikoa 21 ya Tanzania Bara katika mwaka 2008, ili tujionee ukubwa wa tatizo na zilivyoenea kila mahali hivyo kujipanga kuisadia Serikali kukabiliana na tatizo hili la kuongezeka kwa ajali. Dar es Salaam (ajali 9,027); Wilaya ya Kinondoni iliongoza kwa kuwa na ajali 4,557, Ilala ajali 2,534 na Temeke ajali 1,936. Arusha (ajali 1,700); Morogoro (1,464); Pwani (999); Kilimanjaro (906); Mbeya (852); Shinyanga (779); Mwanza (655); Tabora (564); Kigoma (384); Ruvuma (384); Rukwa (342); Mtwara (339); Dodoma (295); Mara (268); Kagera (231); Iringa (215); Singida (208); Tanga (205); Manyara (190); na Lindi (ajali 144).

Mheshimiwa Spika, kwa mwezi Januari, 2009, kumetokea jumla ya ajali 252 ambazo zimesababisha vifo vya Watu 185 na Majeruhi 387. Mikoa inayoongoza kwa mwaka huu hadi sasa ni Arusha ajali 69, Morogoro ajali 37, Kagera 30, Mbeya 25, Tanga 17, Kigoma 14, Dar es Salaam ajali 13, Mtwara 11 na Kilimanjaro nane. Mikoa mingine ni Manyara, Mara, Ruvuma na Shinyanga ambayo ina ajali nne kila Mkoa, Mikoa ya Dodoma na Lindi yenye ajali tatu kila mmoja. Mwanza na Tabora ajali mbili kila mmoja na mwisho Mikoa ya Pwani na Rukwa yenye ajali moja kila mmoja. Mikoa ya Iringa na Singida bado ni shwari. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu hapajatokea ajali zilizowasilishwa kwa kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtu anaweza kufikiria kuwa ajali ikitokea Madereva wana uhakika hawatakufa wala kuumia. Kumbe na wao wanakufa na kuacha Watoto wao Yatima, kuacha mke kuacha wake zao Wajane na kuacha matatizo mengi kwa familia zao. Kati ya abiria 2,924 waliopoteza maisha yao katika ajali mwaka 2008, madereva waliopoteza maisha ni 152.

Vilevile, wapo wapanda Pikipiki 282 na wapanda Baiskeli 515 ambao wote walipoteza maisha mwaka huo. Hawa pia ndiyo Madereva wenyewe. Kwa maana hiyo, naweza kuhitimisha kwa kusema kuwa Madereva waliopoteza maisha ni 949. Hii ni idadi kubwa ya Watu wanaopoteza maisha kwa kufanya mzaha tu katika uendeshaji. Nawasihi

Madereva mjionee huruma kwanza wenyewe, Watoto wenu, Wake zenu na Familia zenu kwa ujumla kabla hata hamjawaonea huruma Abiria wengine mnaowaendesha. Hali hiyo itawalazimisha na kuwafanya muwe waangalifu na waoga na muwe makini na muwe waungwana na watu wenye kuthamini utu wa wenzenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limetoa takwimu zinazoonyesha vyanzo vya ajali nchini na kwamba uendeshaji wa hatari unachangia kwa asilimia 41; ubovu wa magari, asilimia 11; uzembe wa watembea kwa miguu, asilimia 9; mwendokasi, asilimia 7; uzembe wa wapanda pikipiki, asilimia 7; uzembe wa wapanda baiskeli, asilimia 7; hali ya barabara, asilimia 5; kupitwa kwa ghafla asilimia 4.5; kukataa kupitwa, asilimia 4; ulevi, asilimia moja na sababu nyinginezo zinachukua asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa umakini sababu hizi za ajali utagundua kwamba, ajali nyingi zinatokea kwa kuwa mifumo yetu haijaweka mikakati ya kupunguza ajali hizi. Baadhi ya mambo ambayo inabidi kuyatazama upya ni:-

(i) Adhabu ndogo zinazotolewa ikiwa ni pamoja na faini kwa madereva wanaosababisha ajali na hivyo kuwafanya wasiwe waangalifu na kufuata sheria za barabarani; *(Makofi)*

(ii) Kutokuwepo na adhabu kwa wamiliki wa magari na hivyo kuwapa mwanya wa kuajiri madereva wasio na uzoefu wa kutosha kuendesha magari ya abiria. Vilevile, wengine wanaajiri madereva ambao hawakusomea kazi ya udereva, lakini walijifunza kuendesha gari wakiwa utingo au wakiwa wanafanya kazi ya kuosha magari; na

(iii) Vyombo vya dola kutokusimamia Sheria zilizopo ili zifanye kazi kikamilifu na hivyo kuwapa mwanya madereva kufanya wanavyotaka. Kwa mfano, nimeambiwa kila gari hata kama ni la Serikali linatakiwa liwe na *‘Triangle Reflectors’* mbili ambazo huwekwa nyuma na mbele ya gari linapoharibika njiani ili kuonyesha kuna gari bovu mbele. Bado Madereva wanatumia majani, mawe na magogo kama alama za kuonyesha kuwa mbele kuna gari bovu au ajali. Jamani hapa alaumiwe nani? Tunakwenda wapi? Ni jukumu la Askari wa Usalama Barabarani kuhakikisha kuwa utaratibu huu unazingatiwa kwa sababu unachangia katika ajali barabarani. Kuna ugumu gani wa kusimamia kuhakikisha kila mwenye gari anakuwa na hivyo vibao vya kuonyesha alama, yaani *reflectors*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali ambalo nimekuwa nikijiuliza, hivi nchi nyingine zimewezaje kupunguza ajali za barabarani? Tafiti za haraka zinaonyesha kuwa, jambo kubwa kwa nchi hizo ni kwa Kikosi cha Askari wa Usalama Barabarani na Askari wengine kuhakikisha madereva wote wanafuata Sheria na anayekiuka hupewa adhabu kali zikiwemo:-

(i) Kufungiwa leseni kwa kipindi kirefu na kama umesababisha ajali mara nyingi unanyang'anywa kabisa;

(ii) Faini kali za papo kwa papo hutolewa dereva anapovunja Sheria. Faini hizi hutakiwa kwenda kulipa Kituo cha Polisi ndani ya siku saba. Dereva asipolipa kwa wakati kiwango alichoadhibiwa, faini huendelea kuongezeka kila mwezi na akikamatwa hupelekwa Mahakamani moja kwa moja na Hakimu humtoza faini kubwa sana na wakati mwingine kifungo; na

(iii) Gari linapopata ajali, Bima yake huongezeka sana. Kwa mfano, kama Bbima ilikuwa inalipiwa Sh. 100,000/=, basi ukipata ajali, Bima inaongezeka na kuwa Sh. 150,000/= au zaidi. Ni kila wakati unapopata ajali Bima itakuwa inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba Jeshi la Polisi hasa Askari wa Usalama Barabarani waongeze Kasi na Nguvu zaidi ya kushughulikia tatizo hilo, kwani linahusu maisha ya watu.

Suala la ukaguzi wa magari na leseni za madereva liwe la kudumu. Hivyo, ni jukumu la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia upya Sheria zote za Usalama Barabarani, kuangalia upungufu wake na kuishauri Serikali nini cha kufanya. Kama kuna Sheria inayohitaji kurekebishwa au kuongeza adhabu, basi Bunge lipo, ni wajibu wetu Serikalini kuharakisha kuwasilisha mabadiliko Bungeni na kupata ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge. Zoezi hili lianze mara moja bila kuchelewa ili kuokoa maisha ya Watanzania wanaokufa bila kuwa na hatia.

Aidha, Wizara ianzishe utaratibu wa kudumu wa kukagua mabasi yote yakiwemo ya daladala. Vilevile, mapendekezo na mikakati yote iliyotolewa ya kupunguza ajali barabarani sasa ianze kutengewa utaratibu wa namna ya kutumia. Hatuwezi kuishi na Mikakati inayotajwa kila wakati, huku wananchi wasiokuwa na hatia wakiendelea kupoteza maisha kwa Uzembe wa Watendaji wachache. Napenda nipewe taarifa ya utekelezaji wa zoezi hili kila baada ya miezi mitatu na jinsi zoezi lilivyochangia kupunguza ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo utanishangaa nimeandama maeneo yenye matatizo tu, lakini nia yangu ni kutaka Watanzania wenzangu waone matatizo tuliyonayo na kwa pamoja tusaidiane kutafuta namna ya kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, tatizo la dawa za kulevya limekuwepo hapa nchini kwa miaka mingi hasa nchi yetu kutumiwa kama Kituo cha kupitishia dawa hizo kwenda nchi nyingine. Vilevile, wapo watu wengi wanaotumia dawa za Kulevya, wakiwemo vijana wenye nguvu za kufanya kazi, wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Vikuu. Miji ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga, Zanzibar, Mwanza na Mbeya ina watumiaji wengi wa dawa za kulevya.

Matumizi na Biashara Haramu ya dawa za kulevya yana athari kubwa kwa Taifa, kiuchumi, kiafya na kijamii ikiwemo kuchangia maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa njia ya Kudunga Sindano na watumiaji kushindwa kufanya maamuzi sahihi ya ngono salama. Utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Muhimbili mwaka 2006 unaonyesha kuwa asilimia 42 ya watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano wameambukizwa Virusi vya UKIMWI. Halikadhalika matumizi ya dawa hizi huchangia kuporomoka kwa maadili na kuongezeka kwa uhalifu. Kwa upande mwingine, Mikoa ya Morogoro, Arusha, Mara, Iringa na Tanga hulima bangi kwa wingi sana na matokeo yake ni kuathiri uzalishaji wa mazao mengine yenye tija zaidi. Sambamba na hilo, uvutaji bangi husababisha kupotea nguvu kazi ya Taifa kwa kuwa watumiaji hushindwa kufanya kazi zenye tija kwa maendeleo. *(Makofi)*

Serikali inafanya jitihada za kupambana na tatizo hili kubwa la dawa za kulevya ikiwemo kukamata wahalifu wanaojihusisha na dawa hizo pamoja na kuteketeza mashamba ya bangi. Kwa mfano, mwaka 2008 jumla ya watuhumiwa 6,606 walikamatwa ndani ya nchi kwa kujihusisha na dawa za kulevya. Vilevile, katika kipindi hicho watanzania wengine 21 walikamatwa nje ya nchi kwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya na ekari zipatazo 72 za mashamba ya bangi ziliteketezwa. Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu athari zinazotokana na dawa za kulevya. Wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla wakiwemo Viongozi wa Dini na Viongozi wengine wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali tusaidie kupambana na tatizo hili la dawa za kulevya ili kuliepusha Taifa letu na janga hili ambalo linaharibu kizazi cha Taifa la Kesho.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu ni kwamba, tukiandamwa na majanga mengi kiasi hiki, mwisho wa Taifa hili utakuwa ni nini?

Mheshimiwa Spika, wakati nakaribia mwishoni, basi naomba nieleze tu taarifa fupi ya ziara yangu huko Visiwani Zanzibar Kuanzia tarehe 13 – 15 Januari, 2009. Nilifanya ziara Tanzania Zanzibar, kuanzia tarehe 13 hadi 15 Januari, 2009 ambapo niliweza kutembelea Mikoa miwili ya Visiwa vya Pemba na mitatu ya Visiwa vya Unguja ambayo ni Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Kusini Unguja, Kaskazini Unguja na Mjini Magharibi. Katika ziara hiyo, nilijionea mwenyewe hatua mbalimbali zilizofikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Mkakati wa Kupunguza Umaskini Zanzibar *(MKUZA)*, Malengo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa, pamoja na mikakati na malengo mengine ya maendeleo. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Aman Abeid Karume - Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha - Waziri Kiongozi, Mawaziri na Viongozi wengine wote kwa mapokezi mazuri yaliyonipa nafasi ya kuona utekelezaji wa Ilani ya CCM huko Visiwani.

Mheshimiwa Spika, natoa changamoto kwa Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wawakilishi na Waheshimiwa Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kubadilishana ziara za kikazi ili kujifunza yale mazuri tunayoweza kuyaiga katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Yako mazuri niliyoyaona Zanzibar ambayo huku hayapo hasa katika gharama ndogo za ujenzi

wa majengo. Mambo mengine yanawezekana kama tukishauriana na kuelekezana na tukapiga hatua kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mpango wake Kabambe wa kupeleka Umeme wa Uhakika Visiwani Pemba. Hotuba ya Mheshimiwa Karume kwenye Sherehe za Mapinduzi Zanzibar, tarehe 12 Januari, 2009, ilifafanua kwa kina Mradi wa kupeleka Umeme Pemba kutoka Pangani, Tanga. Mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2009 na utagharimu kiasi cha Dola za Marekani Milioni 60 zitakazotolewa kwa pamoja na Serikali ya Norway, itakayochangia Dola milioni 37.5**,** Serikali ya Mapinduzi Zanzibar – Dola Milioni 15 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dola milioni 7.5. *(Makofi)*

Utekelezaji wa Mradi huu muhimu unadhihirisha azma ya Serikali zetu mbili za kulimaliza kabisa tatizo la upatikanaji wa Umeme wa uhakika katika Visiwa vya Pemba. Napenda kuwahakikishia Watanzania wote kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya kazi nzuri ya kuleta maendeleo Visiwani Zanzibar. Yatosha kusema ni Serikali makini na inayojali wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Nchi yetu bado ni nchi nzuri na yenye amani. Wananchi wake ni waelewa kama wakielimishwa. Vilevile, nchi yetu ina fursa ambazo zikitumika vizuri, wananchi wake wataweza kujijengea maisha bora. Kwa maana hiyo, napenda kukamilisha hoja yangu kwa kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Tunalo tatizo la upungufu wa chakula lililoanza kujitokeza. Dalili zinajionyesha katika baadhi ya Wilaya hivi sasa. Wananchi wote tuwe tayari kutunza chakula kidogo tulichonacho kwa tahadhari ya matumizi ya baadaye;

(ii) Kuna hatari ya kupoteza rasilimali zetu za majini kutokana na uvuvi haramu. Tushirikiane kuwabaini wote wanaohusika na uvuvi haramu ili kuokoa rasilimali zetu;

(iii) Kiwango cha ufaulu katika Shule za Msingi kimeshuka. Aidha, wanafunzi wengi waliofaulu bado hawajapata nafasi ya kuendelea na masomo pamoja na kwamba wamefaulu. Wananchi wa Mikoa yenye Watoto waliobaki washirikiane na Serikali katika kuhakikisha wanafunzi wote wanapata nafasi ya kuendelea na masomo;

(iv) Mauaji ya walemavu wa ngozi na vikongwe bado ni tatizo na ni unyama ambao haukubaliki kuendelea kwa hali yoyote ile katika Taifa letu la Tanzania. Tushirikiane kumaliza kabisa tatizo hili bila kujali rangi, kabila au itikadi za Kisiasa; na

(v) Suala la ajali za barabarani ni tishio kwa maisha ya wananchi wote. Tushirikiane na Jeshi la Polisi kuwabana madereva wabovu wanaochangia katika kusababisha ajali za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Nakushukuru wewe Mwenyewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri katika Mkutano huu wa Kumi na Nne.

Vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mbalimbali wakati wa mijadala iliyofanyika hapa Bungeni hadi kupitishwa kwa Miswada yote iliyowasilishwa na kupitishwa katika Mkutano huu. Naomba kumshukuru kwa namna ya pekee Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah kwa kazi nzuri akisaidiwa na wasaidizi wake pamoja na Wataaalam wa Wizara zote walioshiriki katika kufanikisha Mkutano huu.

Navishukuru Vyombo vya Habari kwa kazi nzuri katika kuwasilisha yote yaliyojadiliwa hapa Bungeni kwa wananchi kwa wakati na kwa usahihi. Nawashukuru madereva wote kwa kuendesha kwa uangalifu na kujali maisha ya Viongozi na Watendaji wote wa Serikali hasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Nawaomba muwe waangalifu zaidi mnapowarejesha nyumbani. Wote nasema asanteni sana.

Mwisho, nawatakia wote safari njema mnaporudi katika maeneo yenu ya kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 21 Aprili, 2009 hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA :** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba hiyo nzuri ya kuwasilisha hoja ya kuahirisha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimalize kabisa matangazo yafuatayo machache tu. Kwanza, tulighafilika katika Mkutano wa *SADC PF* ambao sisi tulikuwa wenyeji Arusha, viongozi wapya waliochaguliwa ni kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Mtoto wa Mfalme Price Guduza Lamini Mbunge na Spika wa Bunge wa Swaziland alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *SADC PF* kwa miaka miwili ijayo. *(Makofi)*

Lakini raha inakuja pale ambapo Mheshimiwa Anne S. Makinda Naibu Spika wa Bunge la Tanzania alichaguliwa kwa kauli moja kuwa Makamu wa Mwenyekiti wa *SADC PF. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la pili, Semina ya Kanuni za Bunge iliyopangwa ifanyike Dar es Salaam Ijumaa tarehe 13 na Jumamosi nusu siku yaani tarehe 14 imeahirishwa ili tujiandae vizuri. Tutawatumia taarifa wakati muafaka ambao ungefaa semina ifanyike.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mbele yetu ni ya kuliahirisha Bunge hadi tarehe ambayo imetamkwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hoja hiyo imetolewa na imeungwa Mkono.

Basi kabla sijatamka kuikariri hiyo, naomba niwarejeshe kwenye Kanuni ya 29(3) inasema hivi : “Mara tu baada ya kupitisha hoja ya kuahirisha Mkutano wa Bunge, Wimbo wa Taifa utapigwa na kuimbwa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Bunge.’

Kwa hiyo, nawaomba sasa tusimame kwa wimbo wa Taifa.

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

*(Saa 02 :14 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 21 Aprili, 2009 Saa 03 :00 Asubuhi)*